

## JE, SHERIA YA MUNGU INAPINGANA NA INJILI?

Somo hili nyeti sana limeleta utata mkubwa mno na kuchanganyikiwa miongoni mwa sehemu kubwa sana ya Wakristo tangu wakati ule wa Matengenezo ya Kanisa (Reformation of the Church) ya karne ile ya kumi na sita mpaka hivi leo. Mpendwa, hii ni nafasi yako ya pekee kuweza kujua ukweli juu ya somo hili lenye utata. Kulipuuza ni kujiweka katika hali ya kupoteza wokovu wako.

## SHERIA [AMRI KUMI] NI YA UHURU

Waalimu wengi wa dini wanadai kwamba Kristo kwa kifo chake aliiondolea mbali Sheria [Amri Kumi] na kwamba tangu sasa watu wako huru hawafungwi na masharti yake. Kuna baadhi yao wanaoieleza [sheria hiyo] kama kongwa zito, nao wanahubiri uhuru unaoweza kufurahiwa chini ya INJILI kinyume na utumwa wa kuwa chini ya SHERIA hiyo.

Lakini hivyo sivyo Manabii na Mitume walivyoiona Sheria takatifu ya Mungu. Daudi alisema: "Nami nitakwenda panapo nafasi [KWA UHURU], Kwa kuwa nimejifunza MAUSIA [AMRI] yako." Zaburi 119:45. Mtume Yakobo, aliyeandika baada ya kifo cha Kristo, anaitaja SHERIA ILE YA AMRI KUMI kama "SHERIA YA KIFALME" na "SHERIA KAMILIFU ILIYO YA UHURU." Yakobo 2:8; 1:25. Na mwandishi wa kitabu cha Ufunuo, nusu karne baada ya kusulibiwa [kwake Kristo], anatoa baraka juu ya wale "WAZISHIKAO AMRI ZAKE, wawe na HAKI kuuendea huo mti wa uzima, na kuingia mjini kwa milango yake." Ufunuo 22:14 (Tafsiri ya King James Version).

Madai ya kwamba Kristo kwa kifo Chake aliiondolea mbali Sheria ya Baba Yake hayana msingi wo wote. Laiti ingaliwezekana kwa Sheria hiyo kubadilishwa au kuwekwa kando, basi Kristo ASINGALIHITAJI KUFA ili kumwokoia mwanadamu kutoka katika adhabu ya dhambi zake [kuvunja Sheria]. Kifo chake Kristo, mbali kabisa na kuiondolea mbali Sheria hiyo, KINATHIBITISHA kwamba [Sheria hiyo] HAIBADILIKI. Mwana wa Mungu alikuja "KUITUKUZA Sheria, na KUIADHIMISHA." Isaya 42:21. Alisema: "MSIDHANI ya kuwa nalikuja kuitangua torati [Sheria];" "mpaka MBINGU NA NCHI ZITAKAPOONDOKA, yodi moja wala nukta moja ya torati [Sheria] HAITAONDOKA." Mathayo 5:17,18. Na kumhusu Yeye Mwenyewe anatangaza hivi: "KUYAFANYA mapenzi Yako Ee Mungu, ndiyo furaha yangu; Naam, SHERIA Yako imo MOYONI mwangu." Zaburi 40:8.

## SHERIA HAIBADILIKI

Sheria ya Mungu, kwa asili yake halisi, HAIBADILIKI. [Sheria hii] ni ufunuo wa MAPENZI na TABIA ya Mwasisi wake. Mungu ni UPENDO; na Sheria yake ni UPENDO. Kanuni zake kuu mbili ni UPENDO KWA MUNGU na UPENDO KWA MWANADAMU. "Pendo ndilo utimilifu wa Sheria." Warumi 13:10. Tabia ya Mungu ni HAKI na KWELI; hiyo ndiyo tabia ya Sheria Yake. Asema Mtunga Zaburi: "SHERIA Yako ni KWELI;" "Maana MAAGIZO [AMRI] Yako yote ni ya HAKI." Zaburi 119:142,172. Naye Mtume Paulo anatangaza hivi: "Basi, torati [sheria] ni TAKATIFU, na ile amri ni TAKATIFU, na ya HAKI, na NJEMA." Warumi 7:12. Sheria hiyo, ikiwa ni ufunuo wa moyo [mawazo] na mapenzi ya Mungu, basi, ni lazima iwe ya kudumu kama alivyo Mwasisi wake.

Ni kazi ya UONGOFU na UTAKASO kuwapatanisha wanadamu na Mungu kwa kuwaleta katika mwafaka kamili na kanuni za Sheria Yake. Hapo mwanzo, mwanadamu aliumbwa kwa sura ya Mungu. Alikuwa anapatana kabisa na tabia na Sheria ya Mungu; kanuni hizi za haki ziliandikwa MOYONI mwake. Walakini DHAMBI [UVUNJAJI WA SHERIA] ilimtenga mbali na Muumbaji wake. Hakuakisi tena tabia ya Mungu. Moyo wake ukawa vitani ukipigana na kanuni za Sheria ya Mungu. "Kwa kuwa ile nia ya mwili ni UADUI juu ya Mungu, kwa maana HAITII Sheria ya Mungu, wala HAIWEZI KUTII" Warumi 8:7. Lakini "Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee," ili kwamba mwanadamu apate KUPATANISHWA na Mungu. Kwa njia ya WEMA wake Kristo [mwanadamu] anaweza kurejeshwa katika MWAFKA [MAPATANO] na Muumbaji wake. Moyo wake sharti ufanywe kuwa MPYA kwa NEEMA yake Mungu; sharti apate UZIMA MPYA kutoka juu. BADILIKO hili ndiko KUZALIWA UPYA [au Kuzaliwa mara ya pili, au Kuongoka], na pasipo [badiliko] hilo, asema Yesu, "[mtu huyo] hawezi kuuona ufalme wa Mungu." [Yohana 3:3].

Hatua ya kwanza katika kupatanishwa na Mungu ni KUTAMBUA DHAMBI. "Dhambi ni uvunjaji wa Sheria [Amri Kumi]." "KUTAMBUA dhambi huja kwa njia ya SHERIA [AMRI KUMI]." 1 Yohana 3:4, AJKK; Warumi 3:20. Hicho ni KIOO [Yakobo 1:22-25] kinachoonyesha UKAMILIFU WA TABIA YA HAKI na kumwezesha [mwenye dhambi] KUTAMBUA kasoro alizo nazo katika TABIA yake.

## HURU MBALI NA HUKUMU YA ADHABU

Sheria inamwonyesha mtu dhambi zake, bali HAITOI DAWA yo yote ya kuonya dhambi zake. Wakati inaahidi kumpa UZIMA yule ANAYEITII, papo hapo inatangaza ya kwamba MAUTI ndio mshahara wake mvunja sheria. INJILI yake Kristo PEKE YAKE ndiyo iwezayo kumweka [mtu huyo] HURU mbali na hukumu ya adhabu au kunajisiwa na dhambi. Inampasa kuwa na TOBA kwa Mungu, ambaye Sheria Yake IMEVUNJWA; na kuwa na IMANI kwa Kristo, [aliye] kafara yake ya UPATANISHO. Kwa njia hiyo anapata "MSAMAHA WA [KUACHILIWA KWA] dhambi zilizotangulia kufanywa," naye anakuwa mshirika wa TABIA ya Mungu. Yeye [sasa] ni

mwana [binti] wa Mungu, akiisha kuipokea roho ile ya kufanywa mwana [binti], ambayo kwa hiyo analia: "Aba, yaani, Baba!" [Warumi 8:15].

Je, sasa mtu huyo ana uhuru wa KUIVUNJA Sheria ya Mungu [Amri Kumi]? Asema Paulo: "Basi, je! TWAIBATILISHA Sheria kwa IMANI hiyo? HASHA! kinyume cha hayo TWAITHIBITISHA Sheria." "HASHA! Sisi tulioifia dhambi tutaishije tena katika dhambi [kuvunja Sheria]?" Na Yohana naye anatangaza hivi: "Kwa maana huku ndiko KUMPENDA Mungu, kwamba TUZISHIKE AMRI ZAKE; wala amri Zake si nzito." Warumi 3:31; 6:2; 1 Yohana 5:3. Katika kuzaliwa upya moyo unapatanishwa na Mungu, na kuletwa katika mwafaka na SHERIA Yake. Badiliko hilo kubwa linapotokea ndani ya mwenye dhambi huyo, basi, anakuwa amepita dhambini kuingia katika UTII na UAMINIFU. Maisha yake ya zamani ya KUFARAKANA na Mungu yamekoma; maisha mapya ya upatanisho, imani na upendo, yameanza. Hapo ndipo "HAKI YA SHERIA" itakapotimizw[a] ndani yetu sisi, TUSIOENENDA kwa kufuata mambo ya MWILI, bali mambo ya ROHO." Warumi 8:4. Na lugha ya roho [mtu] hiyo itakuwa ni hii: "SHERIA Yako NAIPENDA MNO AJABU, Ndiyo kutafakari kwangu mchana kutwa." Zaburi 119:97.

"SHERIA ya BWANA ni KAMILIFU; Huiburudisha [Huiingoa] nafsi." Zaburi 19:7. Pasipo Sheria, watu hawana dhana [fikara] sahihi juu ya USAFI na UTAKATIFU wa Mungu au juu ya dhambi zao wenyewe na uchafu. Hawana uthibitisho wa kweli wa dhambi zao wala HAWAJISIKII KUWA NA HAJA YA KUTUBU. Bila kuiona hali yao ya kupotea kama WAVUNJAJI wa Sheria ya Mungu, hawaitambui haja yao ya kutegemea damu ya Kristo ya Upatanisho. Tumaini la WOKOVU linapokelewa pasipo kuwa na BADILIKO KUBWA la moyo au kufanya MATENGENEZO katika MAISHA yao. Hivyo kuongoka kwa juu juu tu kunaenea kila mahali [wengi hudai wameokoka], na watu wengi wanajiunga na kanisa ambao HAWAJAUNGANISHWA kamwe na Kristo

Nadharia [mafundisho] potofu juu ya UTAKASO, hizo pia zikiwa zimechipuka kutokana na KUIPUZIA au KUIKATAA Sheria ya Mungu, zina sehemu muhimu sana katika makundi ya kidini ya SIKU HIZI. Nadharia hizo ni za uongo kimafundisho na za hatari katika matokeo yake kama zikiwekwa katika vitendo; na ukweli kwamba kwa kawaida ZINAPENDWA na watu wengi, hulifanya jambo hili liwe la muhimu maradufu kwamba wote wapate KUJUA KWA WAZI kuhusu Maandiko yanavyofundisha juu ya jambo hili.

## UTAKASO NI NINI?

Utakaso wa kweli ni fundisho la Biblia. Mtume Paulo katika Waraka wake kwa kanisa la Wathesalonike, anawatangazia hivi: "Maana haya ndiyo mapenzi ya Mungu, KUTAKASWA kwenu." Tena anaomba ya kwamba: "Mungu wa amani mwenyewe AWATAKASE kabisa." 1 Wathesalonike 4:3; 5:23. Biblia inafundisha wazi maana ya utakaso na jinsi unavyoweza kupatikana. Mwokozi aliwaombea Wanafunzi wake, akisema: "UWATAKASE kwa ile KWELI; NENO lako ndiyo KWELI." Yohana 17:17,19. Na Paulo naye anafundisha ya kwamba WAUMINI wanapaswa "KUTAKASWA na ROHO MTAKATIFU." Warumi 15:16. Roho Mtakatifu anafanya

kazi gani? Yesu aliwaambia Wanafunzi wake: "Lakini Yeye atakapokuja, huyo ROHO WA KWELI, atawaongoza awatie kwenye KWELI YOTE." Yohana 16:13. Naye Mtunga Zaburi asema hivi: "SHERIA Yako ni KWELI." [Zaburi 119:142]. Kwa njia ya NENO na ROHO WA MUNGU kanuni zile kuu za HAKI ambazo zimo ndani ya Sheria [Amri Kumi] Yake zinafunuliwa kwa watu. Na kwa kuwa Sheria ya Mungu ni "takatifu, na ya haki, na njema," tena ni CHAPA [MFANO HALISI] ya UKAMILIFU wa Mungu, inafuatia ya kwamba TABIA ile inayojengwa kwa njia ya UTII kwa Sheria hiyo [Amri Kumi] nayo itakuwa ni TAKATIFU. Yeye asema: "Ni[me]zishika AMRI [KUMI] za Baba Yangu." "Nafanya sikuzote yale Yampendezayo." Yohana 15:10; 8:29. Wafuasi wake Kristo wanapaswa kuwa kama Yeye alivyo ----- KWA NEEMA YA MUNGU kujenga TABIA zinazopatana na kanuni za Sheria Yake Takatifu [Amri Kumi]. Huu ndio UTAKASO wa Biblia.

### KWA NJIA YA IMANI PEKE YAKE

Kazi hiyo inaweza kutimizwa tu kwa njia ya IMANI KATIKA KRISTO, kwa UWEZA wa Roho wa Mungu anayekaa NDANI [yetu]. Paulo anawaonya waumini: "UTIMIZENI WOKOVU wenu wenyewe kwa kuogopa na kutetemeka. Kwa maana ndiye MUNGU atendaye kazi NDANI yenu, KUTAKA kwenu na KUTENDA kwenu, kwa KULITIMIZA kusudi lake jema." Wafilipi 2:12,13. Mkristo atasikia HISIA za dhambi [ndani yake], bali ataendelea daima KUPAMBANA nazo. Hapa ndipo unapohitajika MSAADA WAKE KRISTO. Udhaifu wa kibinadamu UNAUNGANISHWA na nguvu za Mungu, kisha IMANI inashangilia: "Mungu na ashukuriwe ATUPAYE KUSHINDA kwa Bwana wetu Yesu Kristo." 1 Wakorintho 15:57

Maandiko yanaonyesha wazi kwamba kazi ya UTAKASO inaendelea SIKU KWA SIKU. Wakati wa KUONGOKA mwenye dhambi anapokuwa na amani na Mungu kwa njia ya damu ile ya upatanisho, MAISHA YA KIKRISTO NDIO KWANZA YANAANZA. Sasa ndipo anatakiwa kusonga mbele "hata kuwa mtu MKAMILIFU;" na kukua "hata kufika kwenye cheo cha UTIMILIFU wa Kristo." [Waefeso 4:13]. Asema hivi Mtume Paulo: "Natenda neno moja tu; nikiyasahau yaliyo nyuma [baada ya kuyaungama nakuyaacha], NIKIYACHUCHUMILIA yaliyo mbele; NAKAZA MWENDO, niifikilie MEDE ya thawabu ya mwito mkuu wa Mungu katika Kristo Yesu." Wafilipi 4:13,14. Naye Petro anaweka mbele yetu HATUA ambazo kwazo UTAKASO wa Biblia unaweza kufikiwa: "Mkijitahidi sana kwa upande wenu, katika IMANI yenu TIENI na WEMA, na katika wema wenu MAARIFA, na katika maarifa yenu KIASI, na katika kiasi chenu SABURI, na katika saburi yenu UTAUWA, na katika utauwa wenu UPENDANO WA UNDUGU, na katika upendano wa undugu, UPENDO.... maana MKITENDA HAYO hamtajikwaa kamwe." 2 Petro 1:5-10..

Wale wanaopata UTAKASO wa Biblia wataonyesha moyo wa UNYENYEKEVU. Kama Musa, wameona utukufu wa kutisha wa UTAKATIFU wake Mwenyezi, nao WANAJIONA KUWA HAWAFAI KABISA wakijilinganisha na utakatifu na ukamilifu wa hali ya juu wa Mungu.

Nabii Danieli alikuwa KIELELEZO cha UTAKASO wa kweli. Maisha yake marefu yalijazwa na huduma yake bora kwa Bwana wake. Alikuwa ni "mtu [a]pendwaye sana" (Danieli 10:11) na Mbingu [Mungu]. Lakini badala ya KUDAI KUWA YEYE YU SAFI NA MTAKATIFU, nabii huyu aliyeheshimika alijiweka PAMOJA na Israeli WENYE DHAMBI HASA alipoomba mbele za Mungu kwa ajili ya watu wake: "Hatukutolei maombi yetu kwa sababu ya HAKI yetu, lakini kwa sababu ya REHEMA zako nyingi." "Tumefanya DHAMBI, tumetenda MAOVU." Anatutangazia hivi: "Basi hapo nilipokuwa nikisema, na kuomba , na KUIUNGAMA DHAMBI YANGU, na dhambi ya watu wangu [Israeli]." Baadaye Mwana wa Mungu [Kristo] alipoonekana kwake ili kumpa maagizo fulani, Danieli anasema: "UZURI WANGU [WEMA] uligeuzwa ndani yangu kuwa UHARIBIFU, wala sikusaziwa nguvu." Danieli 9:18,15,20; 10:8.

## HAKUNA KUJISIFU

AYUBU aliposikia sauti ya Bwana katika upepo ule wa kisulisuli, akalia: "Najichukia nafsi yangu, na KUTUBU katika mavumbi na majivu." Ayubu 42:6. Ilikuwa ni wakati ule ISAYA alipouona utukufu wa Bwana, na kuwasikia wale makerubi wakisema, "Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu, ni BWANA wa majeshi," ndipo alipolia, "Ole wangu! kwa maana NIMEPOTEA." Isaya 6:3,5. Paulo naye, baada ya kunyakuliwa juu mpaka MBINGU YA TATU [aliko Mungu] na kusikia MANENO YASIYOTAMKIKA, ambayo haijuzu mwanadamu ayanene, anajieleza mwenyewe kuwa yeye "ni mdogo kuliko yeye aliye mdogo wa WATAKATIFU wote." 2 Wakorintho 12:2-4, pambizo[margin]; Waefeso 3:8. Alikuwa ni yule Yohana mpendwa, aliyeegama kifua pa Yesu na kuuona utukufu Wake, ambaye alianguka kama mtu aliyekufa chini ya miguu ya Malaika [Mjumbe] yule [Kristo]. Ufunuo 1:17.

HAPAWEZI KUWAPO NA KUJISIFU WENYEWWE, wala madai ya KUJISIFU KWAMBA MTU HANA DHAMBI YO YOTE, kwa upande wa wale WANAOTEMBEA katika kivuli kile cha MSALABA wa Kalvari. Wanajisikia ya kwamba ilikuwa ni DHAMBI YAO [KUVUNJA SHERIA YA MUNGU] iliyomletea MAUMIVU MAKALI SANA yaliyovunja moyo wa Mwana wa Mungu, na wazo hilo litawafanya KUJITWEZA [KUJINYENYEKEZA] wenyewe. Wale wanaoishi karibu sana na Yesu wanatambua kwa wazi sana UDHAIFU na UOVU wa kibinadamu [walio nao] na TUMAINI lao tu ni katika WEMA wa Mwokozi yule aliyesulibiwa na kupaa [mbinguni].

Utakaso unaotukuka sana katika ulimwengu wa Kikristo leo una roho ya KUJIKWEZA [KUJISIFU] ndani yake na KUIDHARAU SHERIA ya Mungu, jambo ambalo linaonekana kuwa ni GENI kwa dini ile ya Biblia. Wanaolitetea fundisho hilo wanafundisha kwamba utakaso ni kazi ya papo kwa papo [mara moja], ambao kwa huo, kwa njia ya IMANI PEKE YAKE, wanapata UTAKATIFU ULIOKAMILIKA. "Amini tu," wanasema, "na mbaraka huo ni wako." Hakuna JUHUDI yo yote ya ziada inayohitajika kwa upande wa yule anayepokea [utakaso huo]. Wakati uo huo wanakana MAMLAKA ya Sheria ya Mungu, wakisisitiza ya kwamba wao wameachiliwa wasiwajibike kuzishika amri [kumi]. Lakini, je! yawezekana kwa watu kuwa watakatifu, kupatana na mapenzi na tabia ya Mungu, pasipo kuletwa katika mwafaka na kanuni zile ambazo zinafunua

TABIA na MAPENZI Yake [yaani, Amri Kumi], na kuonyesha yale YAMPENDEZAYO [Mungu]?

## DINI RAHISI

Tamaa ya kuipata DINI RAHISI isiyowataka watu KUJITAHIDI, KUJIKANA NAFSI, KUACHANA NA UPUZI ULIOMO ULIMWENGUNI HUMU, imelifanya fundisho hili la IMANI, na IMANI PEKE YAKE, kuwa fundisho linalopendwa sana na watu wengi; lakini, basi, Neno la Mungu linasemaje? Asema Mtume Yakobo: "Ndugu zangu, yafaa nini, mtu akisema ya kwamba anayo IMANI, lakini hana MATENDO. Je, ile IMANI yaweza KUMWOKOA?... Lakini wataka kujua, wewe mwanadamu usiye kitu, kwamba IMANI PASIPO MATENDO HAIZAI? Je! baba yetu Ibrahimu hakuhesabiwa kuwa ana HAKI kwa MATENDO, hapo alipomtoa Isaka mwanawe juu ya madhabahu? Waona kwamba IMANI ILITENDA KAZI PAMOJA NA MATENDO yake, na ya kwamba IMANI ILE ILIKAMILISHWA KWA NJIA YA MATENDO yale.... Mwaona kwamba mwanadamu huhesabiwa kuwa ana HAKI kwa MATENDO yake; si kwa IMANI PEKE YAKE." Yakobo 2:14-24.

Ushuhuda wa Neno la Mungu uko kinyume na fundisho hili la IMANI PASIPO MATENDO ambalo limewanasa watu wengi. Ile siyo IMANI [ya kweli] inayodai MIBARAKA ya Mbinguni BILA KUTIMIZA MASHARTI yake ambayo kwayo REHEMA inatolewa, [imani] hiyo ni KIBURI SUGU [presumption]; kwa maana imani ya kweli ina msingi wake katika AHADI na MASHARTI ya Maandiko.

Hebu mtu ye yote asijidanganye mwenyewe kwa kusadiki kwamba anaweza kuwa mtakatifu wakati KWA MAKUSUDI KABISA anaivunja mojawapo ya kanuni [amri] hizi za Mungu. Kutenda dhambi moja tu inayofahamika KUNAINYAMAZISHA sauti ya Roho anayetushuhudia na kumtenga mtu huyo mbali na Mungu. "DHAMBI NI UVUNJAJI WA SHERIA." Na "kila ATENDAYE DHAMBI [avunjaye mojawapo ya Amri Kumi] hakumwona Yeye [Kristo], wala hakumtambua." 1 Yohana 3:6. Ijapokuwa katika Nyaraka zake Yohana anazungumzia kikamilifu juu ya UPENDO, hata hivyo hasiti kuifunua tabia halisi ya kundi lile linalodai kwamba LIMETAKASWA wakati linaishi katika UASI na KUVUNJA SHERIA YA MUNGU. "Yeye asemaye, NIMEMJUA [KRISTO], wala HAZISHIKI AMRI ZAKE [KUMI], ni MWONGO, wala kweli haimo ndani yake. Lakini yeye alishikaye neno lake, katika huyo upendo wa Mungu umekamilika kweli kweli." 1 Yohana 2:4,5. Hapa kipo KIPIMO [TEST] cha

IMANI ya kila mtu. Hatuwezi kumhesabia utakatifu mtu ye yote pasipo kumleta kwanza kwenye kipimo cha Mungu cha pekee cha UTAKATIFU kinachowapima wale walioko mbinguni na waliomo duniani. Kama watu hawaoni kuwiwa na MZIGO [KUWAJIBIKA] wo wote kuhusu Sheria ile ya Maadili [Amri Kumi], kama wanazirahisisha na kuzidharau amri hizi za Mungu, na kuwafundisha watu hivyo, basi, HAWATAHESHIMIWA Mbinguni, na tunaweza kujua kwamba madai yao hayana msingi wo wote.

Tena lile DAI LA KWAMBA MTU HANA DHAMBI yo yote, dai hilo lenyewe, ni ushahidi kwamba mtu anayetoa dai hilo YUKO MBALI NA UTAKATIFU. Ni kwa sababu hana picha [wazo] sahihi ya USAFI na UTAKATIFU alio nao Mungu ama kile wanachotakiwa kuwa nacho wale watakaopatana na TABIA Yake; kwa sababu hana picha halisi ya USAFI na UZURI uliotukuzwa alio nao Yesu, wala hajui UBAYA na UOVU wa dhambi zake, mtu kama huyo anaweza kujiona mwenyewe kuwa ni mtakatifu. Kadiri umbali unavyozidi kuongezeka kati yake na Kristo, na upungufu mkubwa sana wa mawazo yake kuhusu TABIA aliyo nayo Mungu na mambo anayotaka, ndivyo kadiri yeye anavyojiona kuwa ni mwenye haki machoni pake mwenyewe.

"Heri mtu yule asiyekwenda katika shauri la wasio haki;

Wala hakusimama katika njia ya wakoaji...

Bali Sheria [Amri Kumi] ya BWANA ndiyo impendezayo,

Na Sheria Yake huitafakari mchana na usiku.

Naye atakuwa kama mti uliopandwa kandokando ya vijito vya maji,

Uzaao matunda yake kwa majira yake,

Wala jani lake halinyauki;

Na KILA ALITENDALO LITAFANIKIWA."

Zaburi 1:1-3.

----- E.G. White, in THE TRIUMPH OF GOD'S LOVE, uk.275-279,282;

The Law and the Gospel.

OR, THE GREAT CONTROVERSY, Sura ya 26, uk.465-473.

## PIGA VITA VILE VIZURI VYA IMANI

"Piga vita vile vizuri vya imani; shika uzima ule wa milele ulioitiwa, ukaungama maungamo mazuri mbele ya mashahidi wengi. Nakuagiza mbele za Mungu anayevihifadhi hai vitu vyote, na mbele za Kristo Yesu, aliyeyaungama maungamo mazuri mbele ya Pontio Pilato, kwamba ulinde amri hii pasipo mawaa, pasipo lawama, hata kufunuliwa [kuja] kwake Bwana wetu Yesu Kristo" (1 Timotheo 6:12-14).

"Roho [watu] zinapoongoka [kuzaliwa mara ya pili], WOKOVU wao HAUJAKAMILIKA bado. Hapo ndipo wanapaswa KUPIGA MBIO; mapambano magumu yako mbele yao ku'piga vita vile vizuri vya imani!... Vita hivyo ni vya MAISHA YOTE [ya mtu], na ni lazima viendelezwe mbele kwa NGUVU THABITI zinazolingana na kitu kile unachokitafuta, ambacho ni UZIMA WA MILELE" (OHC 163). "Basi,... na tuweke kando kila mzigo mzito, na dhambi ile ituzingayo kwa upesi; na TUPIGE MBIO kwa saburi katika yale mashindano yaliyowekwa mbele yetu, tukimtaazama Yesu, mwenye kuanzisha na mwenye kutimiza IMANI yetu" (Waebrania 12:1,2). "MIZIGO hiyo... ni TABIA na MAZOEYA YA UPOTOVU [UOVU] ambayo tumejenga kwa njia ya kufuata MWELEKEO wetu [wa dhambi] wa asili" (7BC 934). Kwa hiyo "KILA SIKU [mtu] anapaswa KUJITOA WAKF upya, KILA SIKU anapaswa KUPIGANA na maovu. Tabia zile za zamani, mwelekeo ule wa kufanya mabaya tuliourithi [kutoka kwa wazazi wetu] vitapigana kutaka KUMTAWALA mtu huyo, naye DAIMA anatakiwa kuwa macho kupambana navyo [tabia na mazoea hayo mabaya], AKIJITAHIDI SANA KATIKA NGUVU ZILE ANAZOPEWA NA



KRISTO KUPATA USHINDI" (AA 477). "Hakuna atakayechukuliwa juu [mbinguni] BILA KUFANYA JUHUDI KALI YA KUDUMU kwa upande wake mwenyewe. Wote hawana budi [lazima] kuingia katika vita hii wenyewe" (8T 313). "Kwa NEEMA yake Mungu PAMOJA na JUHUDI THABITI yao wenyewe, ni lazima wawe WASHINDI katika vita hii ya kupigana na MAOVU" (GC 425).

"Hatimaye, mzidi kuwa HODARI katika Bwana na katika UWEZA WA NGUVU ZAKE. Vaeni silaha zote za Mungu, mpate kuweza kuzipinga HILA ZA SHETANI. Kwa maana kushindana kwetu sisi si juu ya damu na nyama; bali ni juu ya FALME na MAMLAKA, juu ya WAKUU wa giza hili, juu ya MAJESHI ya pepo wabaya katika ULIMWENGU WA ROHO. Kwa sababu hiyo twaeni silaha zote za Mungu, mpate kuweza KUSHINDANA siku ya uovu, na mkiisha kuyatimiza yote, KUSIMAMA [KUJIKITA]. Basi simameni, hali mmejifunga KWELI [Yohana 17:17; Zaburi 119:142] viunoni, na kuvaa dirii ya HAKI [Wafilipi 3:9] kifuani, na kufungiwa utayari tuupatao kwa INJILI ya amani [Marko 16:15]; zaidi ya yote mkiitwaa ngao ya IMANI [Marko 9:23; Wafilipi 4:13], ambayo kwa hiyo mtaweza kuizima mishale yote yenye MOTO [I Petro 4:12-16] ya yule mwovu. Tena ipokeeni chapeo ya WOKOVU [2 Wakorintho 6:2], na upanga wa Roho ambao ni NENO LA MUNGU [Luka 6:46-49; Yakobo 1:22-25; Ufunuo 12:11]; kwa SALA zote na MAOMBI [Mathayo 26:41] mkisali KILA WAKATI katika Roho, mkikeshwa kwa jambo hilo na kudumu katika KUWAOMBEA watakatifu wote" (Waefeso 6:10-18). "Kila Mkristo inampasa kukeshwa daima, akilinda kila mlango wa moyo wake ambao kwa huo Shetani anaweza KUJIPENYEZA. Inampasa kuomba ili APEWE MSAADA wa Mungu na wakati uo huo APINGE KWA NGUVU ZAKE ZOTE kila mwelekeo wa dhambi. Kwa ushujaa, kwa imani, kwa kufanya kazi ya jasho, ANAWEZA kushinda. Walakini, hebu na akumbuke kwamba ili KUPATA USHINDI NI LAZIMA KRISTO AKAE NDANI yake na YEYE AKAE NDANI YA KRISTO.... Ni kwa njia ile tu ya MUUNGANO wetu binafsi [kila mmoja peke yake] na Kristo, kufanya mawasiliano [maombi] naye [Kristo] kila siku, kila saa, hapo ndipo tunaweza KUZAA MATUNDA ya Roho Mtakatifu" (5T 47,48). [Wagalatia 5:22,23]. "Basi na tuyavue matendo ya giza, na kuzivaa silaha za nuru. Kama ilivyohusika na mchana na tuenende kwa adabu; si kwa ulafi na ulevi, si kwa ufisadi na uasherati, si kwa ugomvi na wivu. Bali MVAENI BWANA YESU KRISTO, wala MSIUANGALIE MWILI, hata kuwasha tamaa zake" (Warumi 13:12-14).

"Ni kwa njia ya NIA YETU [KUTAKA KWETU] dhambi inatushika sisi" (MB 61). [Yakobo 1:12-15]. "Daima utakuwa katika hatari mpaka hapo utakapoelewa NGUVU halisi ya NIA yako. Unaweza kuamini na kuahidi mambo mengi, lakini ahadi zako au imani yako haina faida yo yote mpaka unapoiweka NIA yako upande wa IMANI yako na MATENDO. Ukivipiga vita vile vizuri vya imani KWA NGUVU ZAKO ZOTE ZA NIA YAKO, utashinda" (5T 513). Yule anayepata MAJARIBU anahitaji kuelewa nguvu halisi ya NIA yake. Hii ndiyo NGUVU inayotawala katika TABIA ya mtu, ----- nguvu ya KUKATA SHAURI [KUAMUA], nguvu ya KUCHAGUA. KILA KITU KINATEGEMEA UTENDAJI SAHIHI WA NIA YAKO. Kule kutamani mema na usafi ni sawa, kwa kadiri kulivyo; lakini kukikomea hapo, basi, HAKUAMBUI lo lote. Wengi WATAANGAMIA wakati wanatumaini na kutamani kuushinda mwelekeo wao mbaya. HAWAISALIMISHI NIA yao kwa Mungu. HAWACHAGUI kumtumikia. Mungu ametupa UWEZO WA KUCHAGUA; ni wetu kuutumia. Hatuwezi kuigeuza mioyo yetu, hatuwezi kuyatawala mawazo yetu, wala hisia zetu, wala MAPENZI yetu. Hatuwezi KUJITAKASA wenyewe, wala kujiweka katika hali ya kufaa kufanya kazi ya Mungu. Lakini TUNAWEZA KUCHAGUA kumtumikia Mungu [tuchague, tuanze kumtumikia bila kungoja kujisikia], tunaweza

kumpa NIA yetu [kuacha tupendayo]; hapo ndipo atakapoweza KUFANYA NDANI YETU KUTAKA KWETU NA KUTENDA KWETU, kwa kulitimiza kusudi lake jema". [Wafilipi 2;12,13]. Hivyo ndivyo TABIA yetu yote itakavyoletwa chini ya UTAWALA wa Kristo. Kwa kuitumia NIA ipasavyo, BADILIKO KAMILI linaweza kutokea katika MAISHA [ya mtu]. Kwa kuisalimisha [kuikabidhi] NIA yetu kwa Kristo, TUNAJIUNGANISHA wenyewe na NGUVU ya Mungu. Tunapokea NGUVU kutoka juu ya kutufanya tuwe IMARA. Maisha SAFI na ya HESHIMA, maisha ya USHINDI juu ya tamaa na ashiki [uzinifu], YANAWEZEKANA kwa kila mmoja wetu atakayeunganisha NIA yake ya kibinadamu iliyo dhaifu, inayotetereka na NIA YA MUNGU yenye UWEZA WOTE, ISİYOTETEREKA" (MH 176).

"NIA ya mwanadamu INAPOSHIRIKIANA na NIA ya Mungu, inakuwa na UWEZO wote. Lo lote linalopaswa kufanywa kwa amri Yake linaweza KUTIMIZWA KWA NGUVU Zake. MAAGIZO [AMRI] Yake yote ndani yake yana UWEZO wa kutuwezesha" [kuyatenda] (COL 333). "NAYAWEZA MAMBO YOTE KATIKA YEYE [KRISTO] ANITIAYE NGUVU" (Wafilipi 4:13). Maana mtafakarini sana Yeye [Kristo] aliyeyastahimili mapingamizi makuu namna hii ya watendao dhambi juu ya nafsi zao, MSIJE MKACHOKA, mkizimia mioyoni mwenu. HAMJAFANYA VITA HATA KUMWAGIKA DAMU [KUUAWA], mkishindana na DHAMBI" (Waebrania 12:3,4). "Inatupasa KUMTAZAMA Kristo; inatupasa KUIPINGA [dhambi] kama Yeye alivyoipinga; inatupasa KUOMBA kama alivyoomba Yeye; inatupasa KUTESEKA kama alivyoteseka Yeye, endapo tunataka KUSHINDA kama alivyoshinda Yeye" (KH 34).

Mwana wa Mungu katika ubinadamu wake alipigana na MAJARIBU YALE YALE MAKALI, yanayowashinda watu, ambayo yanawashambulia watu ----- majaribu ya TAMAA, ya kwenda kwa KIBURI mahali ambapo Mungu hajawaongoza [kujitia majaribuni kwa makusudi], na kumwabudu mungu wa ulimwengu huu, na kuachilia mbali furaha ya milele kwa ajili ya anasa zinazovutia za maisha haya. KILA MMOJA ATAJARIBIWA, lakini Neno la Mungu linasema kwamba HATUTAJARIBIWA KUPITA TUWEZAVYO KUVUMILIA [1 Wakorintho 10:13]. Tunaweza KUMPINGA na KUMSHINDA adui yetu mwenye hila" (1 SM 95). "Natamani ya kwamba ningeweza kuandika maneno ambayo yangeweza kulionyesha jambo hili kama lilivyo [hasa]. Mungu ANAWATAZAMIA askari Wake kuwa kazini [vitani] daima. Hawatakiwi kamwe kuanguka majaribuni, kamwe kutenda dhuluma. Wala hawatakiwi kusalimu amri, wala kukimbia. Wakitegemea NGUVU zake Mungu, wanatakiwa KUDUMISHA UAMINIFU wao. Kwa UTHABITI ambao HAUTAJISALIMISHA hata kama ni kwa inchi moja tu, wanatakiwa KULISHIKILIA SANA neno hili, IMEANDIKWA" (HP 260).

"Shetani alimshambulia Kristo kwa majaribu makali sana na ya hila mno, lakini alipingwa katika kila pambano. Vita vile vilipiganwa kwa niaba yetu, USHINDI ule unafanya iwezekane kwetu KUSHINDA. Kristo atawapa NGUVU wale wote wanaoitafuta [nguvu hiyo kwa maombi]. Hakuna mtu ye yote, BILA KUKUBALI YEYE MWENYEWE, anayeweza kushindwa na Shetani. Shetani HANA UWEZO wo wote KUITAWALA NIA ya mtu au KUMLAZIMISHA mtu kutenda dhambi. Anaweza kumwudhi, lakini HAWEZI kumtia unajisi [dhambi]. Anaweza kusababisha MATESO MAKALI, lakini pasipo kumtia waa lo lote mtu huyo. Ukweli ule wa kwamba KRISTO AMESHINDA ungewatia moyo wafuasi Wake KUPIGANA KIUME vita ile dhidi ya DHAMBI na SHETANI" (GC 510). "Basi NYENYEKEENI chini ya mkono wa Mungu ulio hodari, ili awakweze kwa wakati wake; huku MKIMTWIKA Yeye FADHAA zenu zote, kwa maana Yeye HUJISHUGHULISHA SANA kwa mambo yenu. Mwe na KIASI na KUKESHA; kwa kuwa

MSHTAKI wenu Ibilisi, kama simba angurumaye, huzunguka-zunguka, akitafuta mtu AMMEZE. Nanyi MPINGENI huyo, mkiwa thabiti katika IMANI, mkijua ya kuwa MATESO YALE YALE yanatimizwa kwa NDUGU ZENU walioko duniani" (1 Petro 5:6-9). "Kwa sababu ndio mlioitiwa; maana Kristo naye ALITESWA kwa ajili yenu akawaachia KIELELEZO, mfuata nyayo zake. Yeye HAKUTENDA DHAMBI, wala HILA haikuonekana kinywani mwake. Yeye ALIPOTUKANWA, hakurudisha matukano; ALIPOTESWA, hakuogofya; bali ALIJKABIDHI kwake Yeye ahukumuye kwa haki [Mungu]" (1 Petro 2:21-23). "Yesu hakupigania HAKI zake. Mara nyingi kazi yake ilifanywa kuwa ngumu isivyostahili kwa sababu aliifanya kwa HIARI na pasipo KULALAMIKA. Hata hivyo, HAKUSHINDWA wala KUKATA TAMAA. Aliishi JUU ya MATATIZO hayo, kana kwamba yuko katika nuru itokayo usoni kwake Mungu. Hakulipiza KISASI walipomtendea vibaya, bali ALISTAHIMILI matukano KWA UTULIVU" (DA 89).

"KAKA MKUBWA wa taifa letu yuko kwenye kiti cha enzi cha milele. Anamwangalia kila mtu anayegeuza uso wake KUMWELEKEA Yeye kama MWOKOZI. Anajua kwa UZOEFU wake UDHAIFU wa kibinadamu ulivyo, MAHITAJI yetu yalivyo, na MAHALI ILIPO NGUVU ya majaribu yetu; kwa kuwa Yeye 'ALIJARIBIWA SAWASAWA NA SISI KATIKA MAMBO YOTE, BILA KUFANYA DHAMBI' (Waebrania 4:15). Anakuangalia, Ewe mtoto wa Mungu utetemekaye. Je, unajaribiwa? ATAKUOKOA. Je, wewe u dhaifu? Atakutia NGUVU. Je, wewe u mjinga [hujui mambo]? ATAKUELIMISHA. Je, wewe umejeruhiwa? ATAKUPONYA" (MH 71).

----- Madondoo hayo juu yanatoka katika Biblia na vitabu mbalimbali vya Roho ya Unabii.

(Fight the good fight of faith-Kiswahili).

## KUKABILIANA NA KUMBUKUMBU YA MAISHA YETU

"Kazi ya kila mtu inachunguzwa mbele za Mungu na inaandikwa kama ni ya UAMINIFU ama ya KUKOSA UAMINIFU. Mbele yake kila jina katika vitabu vya mbinguni huandikwa kwa usahihi kabisa kila neno baya, kila tendo la uchoyo [ubinafsi], kila kazi isiyotimizwa, na kila dhambi ya siri, na kila unafiki uliofanywa kwa werevu. Maonyo yaliyotumwa kutoka mbinguni na makaripio YALIYOPUUZWA, wakati uliopotezwa bure [kucheza karata, bao, n.k.], nafasi ambazo hazikutumiwa vizuri, mvuto uliotolewa kwa WEMA au kwa UBAYA, pamoja na matokeo yake yafikayo mbali, vyote hivi vinawekwa katika kumbukumbu zenye tarehe na malaika yule anayetunza kumbukumbu hizo.

## KIPIMO KITAKACHOTUMIKA KATIKA HUKUMU

SHERIA YA MUNGU [AMRI KUMI] ndicho KIPIMO ambacho kwacho TABIA na MAISHA ya wanadamu vitapimwa katika hukumu hii [inayoendelea mbinguni sasa]. Asema yule mwenye hekima: "Mche Mungu, nawe UZISHIKE AMRI ZAKE [KUMI]. Maana kwa jumla ndiyo IMPASAYO [WAJIBU WAKE] mtu. Kwa maana Mungu ataleta hukumuni kila KAZI, pamoja na kila NENO LA SIRI, likiwa JEMA au likiwa BAYA." Mhubiri 12:13,14. Mtume Yakobo anawaonya ndugu zake: "SEMENI ninyi, na KUTENDA kama watu WATAKAOHUKUMIWA KWA SHERIA YA UHURU [AMRI KUMI]. Yakobo 2:12.

Wale ambao katika hukumu hii wana "hesabiwa kuwa wamestahili" watakuwa na sehemu yao katika UFUFUO WA WENYE HAKI. Yesu alisema: "Wale wahesabiwao kuwa wamestahili kuupata ulimwengu ule, na kufufuka katika wafu... huwa sawasawa na malaika; nao ni wana [watoto] wa Mungu, kwa vile walivyo wana [watoto] wa ufufuo." Luka 20:35,36. Tena anatangaza kwamba "wale waliofanya mema" watatoka "kwa UFUFUO WA UZIMA." Yohana 5:29. Wenye haki waliokufa [hawako mbinguni] hawatafufuliwa mpaka baada ya HUKUMU HII KUFUNGWA ambayo kwayo WATAHESABIWA kuwa wamestahili kuupata "ufufuo wa uzima." Tangu SASA wao hawatahudhuria KIMWILI katika MAHAKAMA [ile mbinguni] wakati KUMBUKUMBU zao zinapochunguzwa na KESI zao KUKATWA. [2 Wakorintho 5:10].

Yesu atatokea pale kama MTETEZI [MWOMBEZI] wao, kuwaombea mbele zake Mungu. "Na kama mtu akitenda dhambi tunaye MWOMBEZI [MTETEZI] kwa Baba, Yesu Kristo mwenye haki." 1 Yohana 2:1. "Kwa sababu Kristo hakuingia PATAKATIFU palipofanyika kwa mikono, ndio mfano wa PATAKATIFU HALISI; bali aliingia MBINGUNI HASA, aonekane sasa usoni pa Mungu kwa ajili yetu." "Naye, kwa sababu hii, aweza KUWAOKOA KABISA wao wamjiao Mungu kwa Yeye; maana YU HAI sikuzote ili AWAOMBEE." Waebrania 9:24; 7:25.

## KUMBUKUMBU [VITABU] KUFUNULIWA

Vitabu vya kumbukumbu vinapofunuliwa katika hukumu hii, MAISHA ya wale wote WALIOPATA KUMWAMINI YESU yanachunguzwa mbele zake Mungu [bila wao kuwapo kimwili]. Kuanzia na wale waliotangulia kuishi kwanza duniani humu [Adamu na Hawa], Mtetezi wetu anazishughulikia KESI za kila kizazi kilichofuata zinazotajwa mbele Yake, na kufunga na [kesi za] walio hai [sasa]. Kila jina linatajwa, kila kesi inachunguzwa kwa makini sana. Majina YANAKUBALIWA, majina YANAKATALIWA. Wakati atakapokuta watu wo wote wanazo dhambi zilizobaki katika vitabu vile vya kumbukumbu, ambazo HAZIJATUBIWA wala KUSAMEHEWA, majina yao YATAFUTWA katika kitabu cha uzima, na kumbukumbu ya MATENDO YAO MEMA itafutwa katika KITABU CHA UKUMBUSHO cha Mungu. Mungu alimtangazia Musa: "BWANA akamwambia Musa, Mtu ye yote ALIYENTENDA DHAMBI ndiye NITAKAYEMFUTA katika kitabu changu." Kutoka 32:33. Naye nabii Ezekieli asema: "Bali MWENYE HAKI atakapoghairi, na kuiacha haki yake, na KUTENDA UOVU ... Katika MATENDO yake yote ya HAKI aliyoyatenda HALITAKUMBUKWA hata mojawapo." Ezekieli 18:24.

Wale waliotubu dhambi zao kweli kweli, na kwa imani kudai damu yake Kristo kama kafara ya upatanisho wao, mbele ya majina yao katika vitabu vya mbinguni umeandikwa MSAMAHA; wamekuwa washirika wa HAKI yake Kristo, na TABIA zao zimeonekana kuwa zinapatana kabisa na Sheria ya Mungu [Amri Kumi], DHAMBI zao ZITAFUTWA, na wenyewe watahesabiwa kuwa wanastahili kuupata UZIMA WA MILELE. Kupitia kwa nabii Isaya, Bwana anatanga hivi: "Mimi, naam, Mimi, ndimi NIYAFUTAYE makosa yako kwa ajili yangu mwenyewe, wala SITAZIKUMBUKA dhambi zako." Isaya 43:25. Alisema Yesu: "Yeye ASHINDAYE [DHAMBI] atavikwa hivyo MAVAZI MEUPE [HAKI YA KRISTO], wala SITALIFUTA kamwe JINA LAKE katika KITABU CHA UZIMA, nami nitalikiri jina lake mbele za Baba yangu, na mbele ya malaika zake." "Basi, kila mtu atakayenikiri mbele ya watu, nami nitamkiri mbele za Baba yangu aliye mbinguni. Bali mtu ye yote atakayenikana mbele ya watu, nami nitamkana mbele za Baba yangu aliye mbinguni." Ufunuo 3:5; Mathayo 10:32,33.

Mwombezi wetu wa kimbangu anatoa ombi kwamba wale wote walioshinda kwa njia ya imani katika damu Yake WASAMEHEWE dhambi zao, kwamba wapate KUREJESHA KWENYE MAKAO YAO YA EDENI, na KUVIKWA TAJI kama WARITHI pamoja naye wa ile "MAMLAKA YA KWANZA" [aliyoipoteza Adamu]. Mika 4:8. Shetani katika juhudi yake yote ya KULIDANGANYA na KULIJARIBU taifa letu [la kibinadamu] alikuwa amefikiria KUUVURUGA mpango wa Mungu wa kumwamba mwanadamu; walakini Kristo SASA anamwomba [Baba Yake] kwamba MPANGO HUO SASA UTEKELEZWE kana kwamba MWANADAMU alikuwa HAJAPATA KUANGUKA [DHAMBINI] KAMWE. Anawaombea watu Wake sio tu MSAMAHA na KUHESABIWA HAKI kikamilifu kabisa, bali kwamba WAPATE KUSHIRIKI katika UTUKUFU Wake na KUKETI katika KITI CHAKE cha Enzi.

## KUZIFUTA DHAMBI

Kazi ya HUKUMU YA UPELELEZI (INVESTIGATIVE JUDGMENT) na KUZIFUTA DHAMBI (THE BLOTTING OF SINS) itakwisha KABLA ya marejeo ya pili ya Bwana [wetu]. Kwa vile wafu wanapaswa kuhukumiwa kutokana na mambo yaliyoandikwa katika vitabu vile, haiwezekani kabisa kwamba dhambi za wanadamu zifutwe isipokuwa mpaka BAADA ya [kufungwa] hukumu hiyo ambayo kwayo KESI zao zinapaswa kuchunguzwa. Walakini Mtume Petro anaeleza wazi ya kwamba dhambi za WAUMINI zitafutwa zitakapokuja "nyakati za kuburudishwa kwa kuwako kwake Bwana; apate kumtuma Kristo." Matendo Mitume 3:19,20. Hukumu ya Upelelezi itakapofungwa, KRISTO ATAKUJA, na UJIRA [MSHAHARA] Wake utakuwa pamoja naye KUMLIPA KILA MTU KAMA KAZI [MATENDO] YAKE ILIVYO. [Ufunuo 22:12; Warumi 6:23].

Katika huduma ile ya PATAKATIFU PA DUNIANI, Kuhani Mkuu, baada ya kufanya UPATANISHO kwa ajili ya Israeli, alitoka nje na KUWABARIKI mkutano. Hivyo ndivyo Kristo naye, mwisho wa kazi yake kama MPATANISHI, atatokea, 'pasipo dhambi, kwa HAO WAMTAZAMIAO KWA WOKOVU,' (Waebrania 9:28), na KUWABARIKI watu Wake wanaomngojea kwa kuwapa UZIMA WA MILELE. Kama vile yule Kuhani katika kuiondoa

dhambi kutoka katika PATAKATIFU, alivyoziungama dhambi juu ya kichwa cha Mbuji wa Azazeli, hivyo ndivyo naye Kristo atakavyoweka dhambi zote hizo juu ya SHETANI, Mwasisi na Mchochezi wa dhambi zote. Yule Mbuji wa Azazeli, akiwa amebeba dhambi za Israeli, alipelekwa mbali katika nchi "ISIYO NA WATU" (Mambo ya Walawi 16:22); hivyo ndivyo naye SHETANI, akiwa amechukua HATIA YA DHAMBI ZOTE alizowasababisha watu wa Mungu kuzitenda, atafungwa kwa MIAKA ELFU MOJA humu duniani, ambayo kwa wakati huo ITAKUWA UKIWA [TUPU], HAINA WATU, na hatimaye atapata adhabu kamili ya dhambi zake katika MOTO ule utakaowaangamiza waovu wote. [Ufunuo 20:9,10,15; Malaki 4:1-3; Ezekieli 28:14,15,17-19]. Hivyo ndivyo MPANGO ULE MKUU WA UKOMBOZI utakavyofikia UTIMILIFU wake katika tendo la mwisho la KUFUTILIA MBALI DHAMBI na KUWAKOMBOA wale wote waliopenda KUACHANA NA UOVU WOTE.

## NJIA YA UTAKATIFU

Wale watakaoshiriki manufaa ya kazi ya Mwokozi ya UOMBEZI [UPATANISHO] wasiruhusu kitu cho chote kuingilia kati hilo JUKUMU lao la KUKAMILISHA UTAKATIFU katika kicho chake Mungu. Saa zao za thamani, badala ya kuzitumia kwa mambo ya ANASA, KUJIONYESHA, au KUTAFUTA FAIDA, wangezitumia kwa KUJIFUNZA NENO LA KWELI kwa bidii na maombi. Somo la PATAKATIFU (THE SANCTUARY) na HUKUMU YA UPELELEZI (THE INVESTIGATIVE JUDGMENT) yanapaswa kueleweka kwa WAZI na watu Wake Mungu. Wote wanahitaji KUJUA wao wenyewe MAHALI ALIPO NA KAZI ANAYOFANYA Kuhani wao Mkuu [Yesu Kristo]. La sivyo, itakuwa HAIWEZEKANI kwao kuitumia imani yao ambayo ni ya muhimu kwa WAKATI HUU au KUKALIA NAFASI ambayo Mungu amekusudia wajaze. Kila mtu mmoja mmoja anayo roho yake ya KUIOKOA au KUIPOTEZA. Kila mmoja ana KESI [Kuna Wakristo wanaodhani hawatahukumiwa ati kwa sababu wanamwamini Kristo] INAYOMNGOJEA katika MAHAKAMA ya Mungu [mbinguni]. Kila mmoja atakutana na JAJI MKUU ana kwa ana [kwa njia ya kumbukumbu katika vitabu --- 2 Wakorintho 5:10]. Basi, ni jambo la muhimu jinsi gani kwamba kila moyo [mtu] utafakari sana mara kwa mara mandhari ile ya kutisha wakati hukumu itakapowekwa na vitabu vitakapofunuliwa, wakati ule, pamoja na Danieli, kila mtu mmoja mmoja atasimama katika KURA [NAFASI] yake, mwisho wa siku zile. [Danieli 7:9,10; 12:13].

Wale wote waliopata mwanga juu ya masomo haya [Patakatifu na Hukumu ya Upelelezi] wanatakiwa kutoa ushuhuda wao wa KWELI HIZI KUU ambazo Mungu amewakabidhi. PATAKATIFU PA MBINGUNI [HEKALU --- Ufunuo 11:19] ndicho KITOVU hasa cha KAZI YAKE KRISTO kwa niaba ya wanadamu. [Patakatifu hapo] PANAMHUSU kila mtu [roho] anayeishi duniani humu. Panatuonyesha sisi MPANGO WA UKOMBOZI, hadi mwisho kabisa wa wakati na kutufunulia suala lile la USHINDI MKUU WA PAMBANO kati ya HAKI na DHAMBI. Ni jambo la muhimu sana kwamba WOTE wangeyachunguza MASOMO haya [mawili yaliyotajwa juu] kwa ukamilifu na kuweza kutoa jibu kwa kila mmoja anayewauliza sababu ya TUMAINI lililo ndani yao.

## MAOMBEZI YAKE KRISTO

MAOMBEZI Yake Kristo kwa niaba ya mwanadamu katika PATAKATIFU PA MBINGUNI huko juu NI YA MUHIMU katika MPANGO WA WOKOVU kama kilivyokuwa KIFO CHAKE JUU YA MSALABA. Kwa njia ya KIFO Chake alianza kazi ile ambayo baada ya ufufuo Wake alipaa mbinguni kwenda KUIKAMILISHA. KWA IMANI tunapaswa kuingia ndani ya PAZIA, "alimoingia Yesu kwa ajili yetu, MTANGULIZI wetu." Waebrania 6:20. Pale ndipo NURU itokayo katika MSALABA ule wa Kalvari INAAKISIWA (reflected). Pale ndipo tunapoweza kuelewa wazi SIRI ZA UKOMBOZI. WOKOVU wa mwanadamu unatimizwa kwa gharama KUBWA MNO kwa Mbingu; KAFARA iliyotolewa ni sawa na madai ya SHERIA YA MUNGU ILIYOVUNJWA. Yesu amefungua njia ya kwenda kwenye KITI CHA ENZI cha Baba, na kwa njia ya MAOMBEZI Yake shauku ya dhiti ya wale wanaokuja Kwake kwa imani inaweza kufikishwa mbele zake Mungu.

"Afichaye dhambi zake HATAFANIKIWA; bali yeye AZIUNGAMAYE na KUZIACHA atapata REHEMA." Mithali 28:13. Kama wale wanaoficha na kutoa udhuru kwa makosa yao WANGEWEZA KUONA jinsi Shetani ANAVYOWASIMANGA, na jinsi ANAVYOMDHIHAKI Kristo pamoja na Malaika Watakatifu kwa mwenendo wao [mbaya], wangepanya haraka KUUNGAMA dhambi zao na KUZIACHA. Kwa njia ya KASORO zilizo katika TABIA zetu, Shetani anafanya kazi ili KUUTAWALA MOYO WOTE, naye anajua kwamba kasoro hizo zikitunzwa [nasi], basi, ATAFANIKIWA [KUTUSHINDA]. Kwa hiyo, DAIMA anatafuta kuwadanganya wafuasi wake Kristo, akitumia HILA zake za kufisha ambazo haiwezekani kwao kuzishinda. Lakini Yesu ANAWAOMBEA akidai mikono Yake iliyojeruhiwa, na mwili Wake uliochubuliwa; naye anawatangazia hivi wale wote ambao wangetaka kumfuata "NEEMA YANGU YAKUTOSHA." 2 Wakorintho 12:9. "Jitieni NIRA yangu, mjifunze kwangu; kwa kuwa mimi ni MPOLE na MNYENYEKEVU wa moyo; nanyi mtapata RAHA nafsi mwenu. Kwa maana NIRA Yangu [Amri Kumi] ni laini, na mzigo wangu ni mwepesi." Mathayo 11:29,30. Hebu asiwepo hata mmoja anayedhani kwamba KASORO zake haziwezi KUPONYEKA. Mungu atatoa IMANI na NEEMA ya kumwezesha KUSHINDA.

HIVI SASA tunaishi katika SIKU KUU ILE YA UPATANISHO [au HUKUMU]. Katika huduma ya PATAKATIFU PA DUNIANI, Kuhani Mkuu alipokuwa anafanya UPATANISHO kwa ajili ya Israeli, WOTE WALITAKIWA KUJITESA NAFSI ZAO kwa KUTUBU dhambi zao na KUJINYENYEKEZA mbele zake Bwana, ili WASIJE WAKAKATILIWA MBALI [WAKAUAWA GHAFULA] na [kutengwa] na watu Wake. Kwa njia iyo hiyo, wale wote WANAOTAKA MAJINA YAO KUBAKI katika KITABU CHA UZIMA, wakati wamebakiwa na siku chache tu za MUDA WAO WA MAJARIBIO (PROBATION) [MATAZAMIO], wangepitesa nafsi zao SASA mbele zake Mungu kwa KUHUZUNIKA [KUTUBU] kwa ajili ya dhambi zao na kuwa na TOBA YA KWELI. Lazima pawe na KUJICHUNGUZA SANA MOYO kwa uaminifu. Moyo ule wa kuyachukulia mambo haya kirahisi-rahisi tu na kimchezo hauna budi kuwekwa mbali.

Kuna vita vinavyohitaji juhudi ambavyo viko mbele ya wote watakaotaka kushinda MIELEKEO YAO MIOVU ambayo inajitahidi KUWATAWALA. Kazi ya KUJIWEKA TAYARI ni kazi ya kila mtu mmoja mmoja. HATUOKOLEWI KATIKA MAKUNDI. Usafi [wa maisha] na uchaji Mungu wa [mtu] mmoja HAUTAFIDIA upungufu wa SIFA hizo ndani ya [mtu] mwingine. Japokuwa mataifa yote yatapita katika hukumu hii mbele zake Mungu, bado Yeye ATAICHUNGUZA KESI ya kila mtu mmoja mmoja kwa MAKINI SANA kana kwamba hapakuwa na kiumbe [mwanadamu] mwingine ye yote duniani. Kila mmoja hana budi kupimwa na kuonekana kuwa hana WAA wala KUNYANZI wala kitu cho chote kama hicho.

Yanatisha mno matukio yale yahasikanayo na KUFUNGWA KWA KAZI YA UPATANISHO [mbinguni]. Ni ya maana kubwa sana mambo yaliyoko kule. HUKUMU INAENDELEA SASA KATIKA PATAKATIFU PA MBINGUNI. Kwa miaka mingi [tangu 1844] kazi hii imekuwa ikiendelea. UPESI ----- hakuna ajuaye ni upesi jinsi gani ----- HUKUMU HIYO ITAWAFIKIA WALIO HAI [wanaoishi duniani sasa]. Katika hali ya kutisha sana mbele zake Mungu MAISHA yetu yataletwa KUCHUNGUZZWA [sisi tutahukumiwa tukiwa hatuko kule kimwili -- Judgment in absentia]. Katika wakati huu kuliko wakati mwingine wo wote inampasa KILA MTU kusikia ONYO hili la Mwokozi, "Angalieni, KESHENI [Ombeni], kwa kuwa HAMJUI wakati ule utakapokuwapo." Marko 13:33. "Walakini USIPOKESHA, nitakuja kama mwivi, wala HUTAIJUA saa nitakayokuja kwako." Ufunuo 3:3.

## UMILELE WA WOTE KUAMULIWA

Kazi ya Hukumu ya Upelelezi itakapofungwa, UMILELE wa [watu] wote utakuwa UMEAMULIWA, ama kwa UZIMA, ama kwa MAUTI [Hapatakuwa na nafasi nyingine tena ya kuhubiriwa Injili]. MUDA WA MAJARIBIO [KUPIMWA] unakoma kipindi kifupi tu KABLA ya kuonekana kwa Bwana wetu katika mawingu ya mbinguni [kuja kulinyakua Kanisa Lake]. Kristo, akiangalia mbele, anatangaza katika kitabu cha Ufunuo maneno haya: "Mwenye KUDHULUMU na AZIDI kudhulumu; mwenye UCHAFU na AZIDI kuwa mchafu; NA MWENYE HAKI NA AZIDI KUTAKASWA. Tazama, naja upesi, na UJIRA [MSHAHARA] wangu u pamoja nami [Warumi 6:23], KUMLIPA kila mtu kama KAZI [MATENDO] yake ilivyo." Ufunuo 22:11,12. [2 Wathesalonike 1:5-10].

Wenye HAKI na WAOVU watakuwa bado wanaishi duniani katika hali yao inayokufa (mortal state) ----- watu watakuwa WAKIPANDA na KUJENGA, WAKILA na KUNYWA, wote wakiwa HAWANA HABARI kwamba HUKUMU YA MWISHO ISIYOBADILIKA [KUHUSU KESI ZAO] IMEKATWA na KUTANGAZWA katika PATAKATIFU PA MBINGUNI. Kabla ya Gharika, baada ya Nuhu kuingia katika safina, Mungu AKAMFUNGIA NDANI na KUWAFUNGIA NJE WAOVU; walakini KWA SIKU SABA watu, PASIPOKUJUA, kwamba MAANGAMIZI yao yalikuwa yameazimiwa, waliendelea na maisha yao ya KUTOJALI, maisha ya ANASA na KUDHIHAKI maonyo ya hukumu iliyokuwa inawajia ghafula. Mwokozi asema hivi: "Ndivyo kutakavyokuwa kuja Kwake Mwana wa Adamu." Mathayo 24:39. Kimya kimya, kama mwivi wa usiku wa manane, itakuja SAA ile ya kuamua MAMBO YOTE ambayo



itashuhudia KUFUNGWA KWA UMILELE wa kila mwanadamu, na kuondolewa kwa mara ya mwisho MSAADA wake wa REHEMA kwa wanadamu wenye dhambi [wakati huo haitawezekana kutubu].

"Kesheni basi... asije akawasili ghafula akawakuta mmelala [hamjajitayarisha]. Marko 13:35,36. Hali hii ni ya HATARI SANA kwa [Wakristo] wale ambao, wakiwa WAMECHOKA KUKESHA, wanageukia VISHAWISHI vya ulimwengu huu. [Mathayo 24:42-51]. Wakati mtu wa BIASHARA amezama [mawazo yake yote yako] katika KUTAFUTA FAIDA, wakati MPENDA ANASA anaendelea kutafuta kujiridhisha katika hiyo, wakati BINTI WA MITINDO anapanga MAPAMBO yake ----- huenda ni katika SAA hiyo HAKIMU WA DUNIA YOTE atakapotamka hukumu hii, "UMEPIMWA KATIKA MIZANI [AMRI KUMI] NAWA UMEONEKANA KUWA UMEPUNGUKA." Danieli 5:27.

----- E.G. White, in THE TRIUMPH OF GOD'S LOVE, Uk.284-290, or THE GREAT CONTROVERSY, Uk. 480-491.

----- ( Facing our Life Record - Kiswahili ) -----



## "WAWEZA KUNITAKASA"

Katika magonjwa yote yaliyojulikana huko Mashariki, UKOMA ulikuwa ugonjwa mbaya mno. Hali yake ya kutoponyeka na jinsi unavyoambukiza, na matokeo yake kwa wagonjwa, yote hayo huufanya [ugonjwa huo] uwe wa kutisha. Miongoni mwa Wayahudi ulidhaniwa kuwa ni ADHABU ya dhambi, kwa hiyo uliitwa "PIGO", "KIDOLE CHA MUNGU." Ulikuwa umeotesha mizizi, usioweza kuondolewa, mbaya, ulifikiriwa kama ni ISHARA YA DHAMBI. Kwa kawaida ya sheria za dini, mwenye ukoma alitangazwa kuwa ni NAJISI. Kama [mtu] aliyekufa tayari, alifungiwa nje ya makazi ya wanadamu. Kila alichokigusa kilikuwa NAJISI. Hewa ilichafuliwa na PUMZI yake. Mtu aliyehisiwa kuwa na ugonjwa huu alilazimika kujionyesha kwa makuhani, ambao wangemchunguza na kuamua shauri lake. Iwapo alitangazwa kuwa ni mwenye ukoma, alitengwa na familia yake, alitengwa kabisa na kusanyiko la Israeli, na kuhukumiwa kwenda kushirikiana na wale waliopatwa na ugonjwa huo tu. Sheria hiyo HAIKUWEZA KUPINDISHWA katika masharti yake. Hata wafalme na watawala HAWAKUSAMEHEWA. Mfalme aliyepatwa na ugonjwa huu mbaya ilimlazimu kuachia enzi yake, na kuhama kutoka kwenye familia yake.

Mbali na rafiki na jamaa zake, mwenye ukoma lazima abebe laana ya ugonjwa wake. Alilazimika kutangaza hadharani janga lake mwenyewe, kuchana nguo zake, na kupiga kelele, akiwaonya wote kukimbia mbali na uchafuzi wa kuwapo kwake. Kilio cha mimi "ni NAJISI! ni NAJISI!" kilisikika kwa sauti ya kuomboleza kutoka kwa yule aliyefukuzwa kwao na kuishi katika hali ya upweke, ilikuwa ni ishara iliyosikiwa na watu kwa hofu na chuki kuu.

Katika eneo lile ambalo Yesu alifanyia kazi Yake walikuwako wengi waliokuwa wanaugua ugonjwa huu na habari ya kazi yake iliwafikia, ikiwasha nuru ya MATUMAINI. Lakini tangu siku zile za Elisha yule nabii, jambo kama hilo la kumtakasa mwenye ukoma ambaye ugonjwa huu ulikuwa umejizatiti halikufahamika kamwe. Hawakuthubutu kumtazamia Yesu kuwafanyia kile ambacho alikuwa hajapata kamwe kumfanyia mtu ye yote yule. Hata hivyo, alikuwako mtu mmoja ambaye ndani ya moyo wake IMANI ilianza kujitokeza. Walakini mtu mwenyewe hakujua jinsi ya kumfikia Yesu. Akiwa amezuiwa hivyo kisheria kuweza kukutana na wenzake, angeweza kumfikia Mponyaji huyo? Naye akajiuliza iwapo Kristo angeweza kumponya kweli. Je, angeweza kuinama na kumwanguka yule aliyesadikiwa kuwa anateseka kwa sababu ya kuwa chini ya hukumu ya Mungu? Je, hatatangaza laana juu yake, kama Mafarisayo, na hata waganga, na kumwonya akimbie kutoka kwenye makazi hayo ya wanadamu? Akatafakari juu ya yote aliyoambiwa kumhusu Yesu. Hakuna hata mmoja aliyetaka MSAADA kwake aliyekuwa amefukuzwa. Mtu huyu mwenye huzuni akaamua KUMTAFUTA MWOKOZI. Japokuwa alitengwa mbali na miji, huenda angeweza kupishana naye [Kristo] katika barabara mojawapo ya vichochoroni kule milimani, ama huenda atamkuta akifundisha nje ya miji midogo. Ugumu [wa kumwona] ulikuwa mkubwa, lakini hilo ndilo lilikuwa TUMAINI lake la pekee.

Mwenye ukoma yule anaongozwa kwa Mwokozi. Yesu anafundisha kando ya bahari, na watu wamekusanyika na kumzunguka. Akiwa amesimama mbali, mwenye ukoma huyo anasikia maneno machache toka katika kinywa cha Mwokozi. Anamwona akiweka mikono Yake juu ya wagonjwa. Anawaona viwete, vipofu, na waliopooza, na wale wanaoelekea kufa kwa magonjwa mbalimbali, wakimsimama wakiwa na afya, wakimsifu Mungu kwa ukombozi wao. Imani inaimarishwa ndani ya moyo wake. Anasogea karibu na karibu zaidi kwenye halaiki ya watu waliokusanyika pale. Masharti yaliyowekwa juu yake, usalama wa watu, na hofu ambayo watu wanayo juu yake, vinasahuliwa. Anafikiria tu juu ya tumaini lenye baraka la kuponywa kwake. Yeye [mwenye ukoma] ni kioja cha kuchukiza mno. Ugonjwa huo umemwingilia na kumharibu kwa namna ya kutisha, na mwili wake unaoendelea kuoza unatisha kuutazama. Kumwona watu wanaanguka nyuma kwa hofu. Wanakanyagana katika haraka yao ya kutaka kumkwepa wasigusane naye. Wengine wanajaribu kumzuia ili asimkaribie Yesu, lakini ni kazi bure. Yeye hawaoni wala hawasikii. Nyuso zao zenye chuki haziangalii wala hazijali. Anamwona Mwana wa Mungu peke yake. Anaisikia peke yake sauti ile inayotamka uzima kwa wanaotaka kufa. Akiwa anasonga mbele kwenda kwa Yesu, anajitupa miguuni pake na kulia, "Bwana, ukitaka, waweza kunitakasa."

Yesu akajibu, "Nataka; takasika," akanyosha mkono wake akamgusa. Mathayo 8:3.

Mara hiyo badiliko likatokea juu ya mwenye ukoma. Mwili wake ukawa wenye afya, mishipa yake ya fahamu ikaanza kufanya kazi, misuli yake ikawa imara. Ngozi yake ya juu inayoparuzua yenye magamba ambayo hutokana na ukoma ikatoweka, na mahali pake ukaonekana mng'aro uliofifia kama ule unaoonekana juu ya ngozi ya mtoto mwenye afya.

Yesu akamwagiza mtu yule ya kuwa asitangaze kazi ile iliyofanyika, bali aende moja kwa moja na sadaka yake kujionyesha hekaluni. Sadaka kama hiyo isingeweza kupokelewa mpaka makuhani wamchunguze na kumtangaza mtu huyo kuwa ni mzima kabisa na hana ugonjwa huo. Japokuwa wasingependa kufanya huduma hiyo, wasingeweza kukwepa kufanya uchunguzi huo na kutoa uamuzi wao juu ya jambo hili.

Maneno ya Maandiko yanaonyesha ni kwa msisitizo gani Kristo alimwamuru mtu huyo kuona umuhimu wa kunyamaza na kuchukua hatua ya haraka. "Akamkataza kwa nguvu, akamwondoa mara, akamwambia, Angalia, usimwambie mtu neno lo lote, ila enenda zako ukajionyeshe kwa kuhani, ukatoe alivyoamuru Musa kwa kutakasika kwako, iwe ushuhuda kwao." [Marko 1:43,44]. Makuhani wangukuwa wamejua ukweli kuhusu uponyaji wa mwenye ukoma huyu, chuki yao kwa Kristo ingeweza kuwaongoza kutoa hukumu isiyo ya uaminifu. Yesu alitaka mtu yule ajionyeshe hekaluni kabla uvumi wo wote juu ya mwujiza huo haujawafikia [makuhani wale]. Hivyo uamuzi wa haki ungepatikana, na mwenye ukoma aliyeponywa angeweza kuruhusiwa kuungana tena na familia yake na marafiki.

Kulikuwa na makusudi mengine ambayo Kristo alikuwa nayo mawazoni mwake kwa kumwamuru mtu yule kuwa kimya. Mwokozi alijua kwamba adui zake daima walikuwa wanataka kuzuia kazi Yake, na kuwazuia watu wasimwende. Alijua kwamba kama kuponywa kwa mwenye ukoma huyo kungetangazwa, basi, wagonjwa wengine wa ugonjwa huu mbaya wangukusanyika na kumzunguka, na kelele ingepazwa kwamba wangetiwa unajisi kwa kugusana na wenye ukoma hao. Wengi wa hao wenye ukoma wasingekitumia vizuri kipawa hiki cha afya kwa njia ambayo

ingekifanya kuwa mbaraka kwao wenyewe na kwa wengine. Na kwa kuwavuta wenye ukoma kumzunguka, angetoa nafasi kwa mashtaka kwamba alikuwa anavivunja viziwi vilivyowekwa na sheria ile ya ibada. Hivyo kazi Yake ya kuhubiri injili ingezuiwa.

Tukio lile lilionyesha haki ya Kristo kutoa onyo lile. Kundi kubwa la watu lilikuwa limeshuhudia uponyaji wa mwenye ukoma yule, nao walikuwa na hamu ya kujua uamuzi wa makuhani. Mtu yule [aliyekuwa na ukoma] aliporudi kwa rafiki zake, palikuwa na furaha kuu. Licha ya onyo la Yesu, mtu yule hakuweza kujizuia tena kuficha ukweli wa kuponywa kwake. Kwa kweli ingekuwa haiwezekani kabisa kuuficha [ukweli huo], mwenye ukoma huyo akalitangaza tu lile neno. Akidhani kwamba ni aibu ya Yesu iliyomfanya aweke sharti lile juu yake, alizunguka kote akitangaza uwezo wa Mponyaji huyu mkuu. Hakuelewa kwamba kujionyesha wazi kama huko kuliwafanya makuhani na wazee kudhamiria zaidi kumwamamiza Yesu. Mtu yule aliyeponywa alijisikia ya kwamba mbaraka ule wa afya ulikuwa wa thamani mno [kwake]. Alifurahia nguvu ya uanaume wake na kule kurejeshwa kwake kwenye familia yake na jamii yake, naye akajisikia ya kuwa haiwezekani kwake kujizuia kumpa utukufu Tabibu wake aliyemfanya kuwa mzima. Lakini kitendo chake cha kueneza habari zake [Yesu] mbali kilikuwa na matokeo ya kuizuia kazi Yake kwa muda.

Kila tendo la huduma Yake Kristo lilikuwa na upeo mpana katika makusudi yake. Ndani yake lilikuwa na mambo mengi zaidi kuliko yale yaliyoonekana katika tendo lenyewe. Hivyo ndivyo ilivyokuwa katika suala hili la mwenye ukoma huyu. Kristo alipokuwa anawahudumia wale wote waliomjia, alitamani mno kuwabariki wale ambao hawakuweza kumjia. Wakati alipowavuta kwake watoza ushuru, wapagani, na Wasamaria, alitamani sana kuwafikia makuhani na waalimu ambao walijifungia ndani kutokana na chuki na mapokeo yao. Hakuacha njia hata moja ambayo kwayo wangeweza kufikiwa. Kwa kumtuma kwa makuhani mwenye ukoma yule aliyeponywa, aliwapa ushuhuda uliokusudiwa kuwaondolea chuki zao [kwake].

Mafarisayo walidai kwamba mafundisho ya Kristo yalipingana na sheria ambayo Mungu alikuwa amewapa kupitia kwa Musa, bali kwa agizo lake lile kwa mwenye ukoma yule aliyetakaswa la kutoa sadaka kulingana na sheria ile, alibainisha uongo wa shtaka hili. Ulikuwa ushuhuda tosha kwa ajili ya wote waliotaka kusadikishwa.

Viongozi wa Yerusalemu waliwatuma wapelelezi ili kutafuta sababu fulani za kumwua Yesu. Aliwajibu kwa kuwapa ushahidi wa upendo wake kwa wanadamu, heshima Yake kwa sheria na uweza wake wa kuokoa kutoka dhambini na kifoni. Kwa hiyo aliwashuhudia hivi: "Wamenichukuza mabaya badala ya mema, na chuki badala ya upendo wangu." Zaburi 109:5. Yeye [Kristo] ambaye katika mlima ule alitoa kanuni hii, "Wapendeni adui zenu," Yeye Mwenyewe alionyesha kwa mfano kanuni hii, kwa kutolipa "baya kwa baya, au laumu kwa laumu; bali... kubariki." Mathayo 5:44; 1 Petro 3:9.

Makuhani wale wale waliomhukumu mwenye ukoma kwenda uhamishoni, walithibitisha kupona kwake. Hukumu hii, iliyotangazwa hadharani na kuandikwa, ikawa ushahidi wa kudumu kwa Kristo. Na kama vile mtu huyo alivyorudishwa katika kusanyiko la Israeli, kwa uthibitisho wa makuhani wenyewe kwamba hakuwa na waa lo lote la ugonjwa huo juu yake, hivyo ndivyo yeye mwenyewe alivyogeuka na kuwa shahidi hai wa Mfadhili wake [Kristo]. Kwa furaha akatoa sadaka yake, na kulitukuza jina la Yesu. Makuhani walisadiki juu ya uweza wa Mungu aliokuwa nao

Mwokozi. Nafasi ilitolewa kwao [makuhani] kuweza kujua kweli na kunufaika kwa nuru ile. Ingekataliwa, basi, ingeweza kutoweka, isirudi kamwe. Wengi waliikataa nuru ile; walakini haikutolewa bure. Mioyo mingi iliguswa ambayo kwa muda fulani haikutoa ishara yo yote [ya kuikubali]. Wakati wa maisha Yake Mwokozi, kazi Yake ilionekana kupendwa kidogo na makuhani na waalimu; lakini baada ya kupaa kwake "jamii kubwa ya makuhani wakaitii ile Imani." Matendo ya Mitume 6:7.

Kazi ya Kristo ya kumtakasa mwenye ukoma katika ugonjwa wake mbaya ni kielelezo cha kazi Yake ya kuitakasa roho kutokana na dhambi. Mtu yule aliyekuja kwa Yesu alikuwa "amejawa na ukoma." Sumu yake ya kufisha ilienea katika mwili wake wote. Wanafunzi walitaka kumzuia Bwana wao ili asinguse [yule mwenye ukoma]; kwa sababu kila aliyemgusa mwenye ukoma aligeuka na kuwa najisi. Lakini kwa kuweka mkono Wake juu ya mwenye ukoma yule, Yesu hakunajisika. Mguso Wake ulitoa nguvu iletayo uzima. Ukoma ukatakaswa. Hivyo ndivyo ilivyo kuhusu ukoma wa dhambi, ----- iliyootesha mizizi mirefu, ya kufisha, na isiyowezezana kutakaswa kwa uwezo wa kibinadamu. "Kichwa chote ni kigonjwa, moyo wote umezimia. Tangu wayo wa mguu hata kichwani hamna uzima ndani yake; bali jeraha na machubuko na vidonda vitokavyo usaha; havikufungwa, havikuzongwa-zongwa, wala havikulainishwa kwa mafuta." Isaya 1:5,6. Lakini Yesu, akija kuishi kibinadamu, hachafuki. Kuwapo Kwake kuna nguvu ya uponyaji kwa mwenye dhambi. Ye yote atakayeanguka miguuni pake, akisema kwa imani, "'Bwana, ukitaka, waweza kunitakasa," atasikia jibu, "Nataka, takasika." Mathayo 8:2,3.

Kwa aina nyingine za uponyaji, Yesu hakutoa pale pale mibaraka iliyoombwa. Lakini kwa ugonjwa huu wa ukoma, mara tu alipoomba alikubaliwa. Tunapoomba kwa ajili ya mibaraka ya kidunia, majibu kwa maombi yetu yanaweza kucheleweshwa, au Mungu anaweza kutupa kitu kingine kuliko kile tulichoomba, bali sio hivyo tunapoomba kuokolewa kutoka dhambini. Ni mapenzi Yake kututakasa dhambi zetu, kutufanya sisi kuwa watoto Wake, na kutuwezesha sisi kuishi maisha matakatifu. Kristo "alijitoa nafsi Yake kwa ajili ya dhambi zetu, ili atuokoe na dunia hii mbovu iliyopo sasa, kama alivyopenda Mungu, Baba yetu." Wagalatia 1:4. Na "huu ndio ujasiri tulio nao Kwake, ya kuwa tukiomba kitu sawasawa na mapenzi Yake, atusikia. Na kama tukijua kwamba atusikia, tuombacho chote, twajua kwamba tunazo zile haja tulizomwomba." 1 Yohana 5:14,15. "Tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote." 1 Yohana 1:9.

Katika kumponya mtu yule aliyekuwa amepooza kule Kapernaumu, Kristo alifundisha ukweli ule ule tena. Ilikuwa ni kwa kusudi la kuonyesha uwezo Wake wa kusamehe dhambi, ndio maana mwujiza huu ulifanyika. Na uponyaji huu wa yule aliyepooza pia unaonyesha kweli zingine za thamani. Umejaa matumaini na unatia moyo, na kutokana na shutuma za Mafarisayo, una fundisho la onyo pia.

Kama yule mwenye ukoma, mtu huyu aliyepooza alikuwa amepoteza matumaini yake yote ya kupona. Ugonjwa wake ulikuwa ni matokeo ya maisha yake ya dhambi, na kuumwa kwake kulikuwa kuchungu kutokana na majuto yake. Muda mrefu kabla ya hapo alikuwa amewaomba Mafarisayo na waganga, akitumainia kupata nafuu kutokana na mateso yake ya mawazo na maumivu ya mwili wake. Lakini bila huruma wakamtangaza kuwa hawezi kupona kabisa, nao wakamwacha apatwe na hasira ya Mungu. Mafarisayo walidhani kwamba ugonjwa wake ulikuwa ni ushahidi wa ghadhabu ya Mungu, nao walijitenga wenyewe mbali na wale waliokuwa wagonjwa

na wahitaji. Lakini mara nyingi wale waliojisifu wenyewe kuwa ni watakatifu, walikuwa na hatia nyingi zaidi kuliko wagonjwa wale waliowashutumu

Mtu yule aliyepooza hakuwa na msaada wo wote kabisa, naye pasipo kuwa na matumaini yo yote ya kupata msaada kutoka ko kote kule, alikuwa amekata tamaa kabisa. Kisha akasikia habari za matendo ya ajabu ya Yesu. Akaambiwa kwamba wengine wenye dhambi na wasiokuwa na msaada wo wote kama yeye walikuwa wameponywa; hata wale wenye ukoma walikuwa wametakasika. Na rafiki zake waliompasha habari hizo wakamtia moyo ili asadiki kwamba naye pia angeweza kuponywa kama angeweza kubebwa na kupelekwa kwa Yesu. Lakini tumaini lake likamtoka alipokumbuka jinsi ugonjwa wake ulivyompata. Aliogopa kwamba Tabibu yule Mtakatifu asingeweza kuvumilia kumwona mbele zake.

Walakini haukuwa uponyaji wake wa kimwili alioutaka sana kama kule kupata nafuu kwa kuondolewa mzigo wake wa dhambi. Laiti angeweza kumwona Yesu, na kupokea uthibitisho wa msamaha wa dhambi zake, na kupatanishwa na Mbingu, angekuwa radhi kuishi au kufa, kulingana na mapenzi Yake Mungu. Kilio cha mtu yule aliyekuwa anaelekea kufa kilikuwa, Laiti kama ningaliweza kufika mbele Zake! Hapakuwa na wakati wa kupoteza; tayari nyama za mwili wake zilizokuwa zimedhoofika zilikuwa zinaonyesha dalili ya kuoza. Akawasihi sana rafiki zake kumbeba kwenye kitanda chake na kumpeleka kwa Yesu, nao kwa furaha wakakubali kufanya hivyo. Lakini umati ulikuwa mkubwa mno uliokuwa umekusanyika ndani na kuzunguka nyumba ile ambamo Mwokozi alikuwamo; hata ikawa haiwezekani kwa mgonjwa yule na rafiki zake kumfikia [Yesu], au hata kusogea mahali ambapo wangeweza kuisikia sauti Yake.

Yesu alikuwa akifundisha nyumbani mwa Petro. Kulingana na desturi yao, wanafunzi Wake walikuwa wamekaa karibu Naye kuzunguka, na "Mafarisayo na waalimu wa torati walikuwa wameketi hapo, waliotoka katika kila kijiji cha Galilaya, na Uyahudi, na Yerusalemu." Hao walikuwa wamekuja kama wapelelezi, wakitafuta shtaka dhidi ya Yesu. Nje ya maofisa hao palikuwa na halaiki ya mchangamano wa watu mbalimbali, wenye hamu ya kusikia, wanyenyekevu, wadadisi, na wasioamini. Mataifa mbalimbali pamoja na tabaka zote za jamii zilikuwa zimewakilishwa pale. "Na uweza wa Bwana ulikuwapo apate kuponya." Roho wa uzima aliukalia mkusanyiko ule, bali Mafarisayo na waalimu hawakutambua kuwapo Kwake [Roho]. Hawakusikia haja yo yote ya kuhitaji, na uponyaji ule haukuwa kwa ajili yao. "Wenye njaa amewashibisha mema, na wenye mali amewaondoa mikono mitupu." [Luka 1:53].

Tena na tena wale waliombeba yule mwenye kupooza walijaribu kujipenyeza katika umati ule, lakini ikawa kazi bure. Mtu yule mgonjwa alitazama huku na huko akiwa na uchungu usioneneka. Wakati msaada ule alioutamani sana ulikuwa karibu, angeweza kuliacha tumaini lake? Kwa ushauri wake rafiki zake wakamchukua juu ya paa la nyumba, wakatoboa dari, na kumtelemsha chini miguuni pake Yesu. Mahubiri yakakatishwa. Mwokozi akauangalia uso ule wenye kuomboleza, naye akayaona macho yanayomsihi yakimtazama. Alimjua mgonjwa yule; Alikuwa ni Yeye aliyemvuta Kwake mtu yule aliyekuwa na wasiwasi na mashaka. Wakati yule mwenye kupooza alipokuwa angali nyumbani, Mwokozi ndiye aliyeifanya dhamiri yake ipate kusadiki. Alipotubu dhambi zake, na kuuamini uweza wa Kristo wa kumfanya kuwa mzima, rehema zile za Mwokozi zitoazo uzima zilikuwa zimeubariki kwanza moyo wake uliokuwa unatamani sana [kusamehewa]. Yesu alikuwa ameiangalia nuru ndogo ya imani yake ya awali ikikua na kuwa

imani iliyomtambua Yeye kuwa ndiye aliyekuwa msaada wa pekee kwa mwenye dhambi, naye alikuwa ameiona [imani] ikipata nguvu zaidi kwa kila juhudi aliyofanya kutaka kuja mbele Zake.

Sasa, kwa maneno yaliyoanguka kama muziki katika sikio la mgonjwa yule, Mwokozi akasema, "Jipe moyo mkuu, mwanangu, UMESAMEHEWA dhambi zako."

Mzigo wa kukata tamaa unatoweka moyoni mwa mtu yule mgonjwa; amani ya kusamehewa inakaa moyoni mwake, nayo inang'aa usoni pake. Maumivu yake ya mwili yametoweka, na mwili wake wote umebadilika. Mwenye kupooza asiyejiweza ameponywa! mwenye dhambi aliye na hatia amesamehewa!

Kwa imani rahisi akayakubali maneno ya Yesu kama ndiyo mbaraka wa maisha yake mapya. Hakusisitiza ombi lingine zaidi, bali alilala kimya akiwa mwenye furaha, akiwa na furaha nyingi sana kiasi cha kukosa maneno ya kusema. Nuru ya Mbinguni iliungaza uso wake, na watu wakaangalia tukio lile kwa hofu.

Waalimu walikuwa wamengoja kwa wasiwasi kuona mwelekeo gani atakuwa nao Yesu kwa mgonjwa huyu. Walikumbuka jinsi mtu huyo alivyowaomba wao msaada, na jinsi walivyokuwa wamekataa kumpa tumaini lo lote wala kumwonyesha huruma yao. Pasipo kutosheka na hilo, walikuwa wametangaza kwamba alikuwa anateseka kutokana na laana ya Mungu kwa dhambi zake. Mambo haya yalikuja upya mioyoni mwao walipomwona mtu yule mgonjwa mbele yao. Waliangalia shauku waliyokuwa nayo [watu] wote kuliangalia tukio hilo, nao wakashikwa na hofu kuu ya kupoteza mvuto wao juu ya watu wale.

Wakuu hao hawakubadilishana maneno pamoja, bali kwa kutazamana usoni walisoma wazo lile lile ndani ya kila mmoja wao, ya kwamba jambo fulani halina budi kufanywa kuzuia wimbi la hisia za watu. Yesu alikuwa ametangaza kwamba dhambi za mwenye kupooza zilikuwa zimesamehewa. Mafarisayo wakadaka maneno hayo na kusema kwamba huko ni kukufuru, nao wakatunga njama kwamba wangeweza kulileta jambo hilo kama dhambi inayostahili kifo. Mioyoni mwao wakasema, "Anakufuru. Ni nani awezaye kusamehe dhambi isipokuwa mmoja, ndiye Mungu?" Marko 2:7.

Akiwa amewakazia macho, wakanywea na kujikunja, Yesu akasema, "Mbona mnafikiri hivi mioyoni mwenu? Vyepesi ni vipi, kumwambia mwenye kupooza, Umesamehewa dhambi zako, au kusema, Ondoka, ujitwike godoro lako, uende? Lakini mpate kujua ya kwamba Mwana wa Adamu anayo amri duniani ya kusamehe dhambi," akamgeukia yule mwenye kupooza, na kusema, "Ondoka ujitwike godoro lako uende nyumbani kwako."

Hapo ndipo yule aliyekuwa amechukuliwa kwenye kitanda mpaka kwa Yesu, anasimama kwa miguu yake kwa wepesi na nguvu za ujana. Damu itoayo uzima inaenda kwa nguvu katika mishipa yake. Kila kiungo cha mwili wake kwa ghafula kinaanza kufanya kazi yake. Nuru nyekundu ya uso wenye afya inakuwa badala ya kukwajuka [kuwa na uso mweupe kwa ugonjwa] kunakoonyesha hali ya kufa. "Mara akaondoka, akajitwika godoro lake, akatoka mbele yao wote; hata wakastaajabu wote, wakamtukuza Mungu, wakisema, Namna hii hatujapata kuiona kamwe" [Marko 2:12].



Loo! ni upendo wa Kristo wa ajabu ulioje, kujidhili ili apate kuwaponya wenye hatia na wagonjwa! Uungu ukihuzunika na kupunguza makali ya maumivu yanayoletwa na magonjwa ya wanadamu wanaoteseka! Loo! ni nguvu ya ajabu jinsi gani inayodhihirishwa hivyo kwa watoto wa wanadamu! Je, ni nani anayeweza kuwa na mashaka na ujumbe huu wa wokovu? Ni nani anayeweza kuzidharau rehema za Mkombozi huyu mwenye huruma?

Hakikuhitajika kitu cho chote pungufu kuliko uweza ule wa uumbaji ili kuurejeshea afya mwili ule uliokuwa unaoza. Sauti ile ile iliyotamka uzima kwa mwanadamu yule aliyumbwa kutoka katika mavumbi ya ardhi, ilikuwa imetamka uzima kwa mtu yule aliyepooza aliyekuwa anaelekea kufa. Na ni uweza ule ule ulioupa mwili wake uzima, ndio ulioupa moyo wake nguvu mpya. Yule [Kristo] ambaye wakati ule wa uumbaji "alisema na ikawa," ambaye "aliamuru, ikasimama" (Zaburi 33:9) alikuwa ametamka uzima kwa roho ile iliyokuwa imekufa katika makosa na dhambi. Uponyaji wa mwili wake ulikuwa ni ushahidi wa uwezo ule ulioupa moyo wake nguvu mpya. Kristo akamwamuru yule aliyekuwa amepooza kusimama kwa miguu yake na kuondoka, "ili mpate kujua," akasema, "ya kwamba Mwana wa Adamu anayo amri duniani ya kusamehe dhambi."

Mwenye kupooza alipata kwa Kristo uponyaji kwa vyote viwili, roho yake na mwili wake. Uponyaji wa kiroho uliofuatiwa na kurejeshwa kwa afya yake ya mwili. Fundisho hili lisisahauliwe. Leo kuna watu maelfu ambao huugua magonjwa ya kimwili, ambao, kama mwenye kupooza yule, wanatamani kupata ujumbe kama ule, usemao, "dhambi zako zimesamehewa." Mzigo wa dhambi pamoja na wasiwasi wake na tamaa zake zisizoweza kutoshelezwa, ndicho chanzo cha maradhi yao. Hawawezi kupata nafuu yo yote mpaka waje kwa Mponyaji wa roho zao. Amani ambayo ni yeye peke yake awezaye kuwapa, ingetia akili yao nguvu, na kuupa mwili wao afya.

Yesu alikuja "ili azivunje kazi za Ibilisi." "Ndani Yake ndimo ulimokuwa uzima," naye asema, "Mimi nalikuja ili wawe na uzima, kisha wawe nao tele." Yeye ndiye ile "roho yenye kuhuisha." 1 Yohana 3:8; Yohana 1:4; 10:10; 1 Wakorintho 15:45. Na Yeye bado anao uweza ule ule wa kutoa uzima kama alivyokuwa nao alipowaponya wagonjwa hapa duniani, na kunena msamaha kwa mwenye dhambi. "Akusamehe maovu yako yote, Akuponya magonjwa yako yote." Zaburi 103:3.

Matokeo juu ya watu wale yaliyoletwa na uponyaji wa yule mwenye kupooza yalikuwa kana kwamba Mbingu ilikuwa imefunguliwa, na kuufunua utukufu wa ulimwengu ule ulio bora. Mtu yule aliyeponywa alipopita katikati ya umati ule wa watu, akimsifu Mungu kwa kila hatua [aliyotembea], huku akiwa ameubeba mzigo wake kana kwamba ulikuwa na uzito wa unyoya, watu wale wakaanguka kinyumenyume na kumwachia nafasi, huku wakiwa na nyuso zenye kujawa na hofu, wakamkazia macho, wakinong'ona kimya kimya miongoni mwao wenyewe, na kusema, "Leo tumeona mambo ya ajabu."

Mafarisayo wakawa kimya kwa mshangao na kwa kulemewa kabisa na kushindwa kwao. Wakaona kwamba hapa hapakuwa na nafasi ya wivu wao wa kutaka kuwachochea watu waliokusanyika pale. Kazi ya ajabu iliyotendwa juu ya mtu yule waliyekuwa wamemtoa apate ghadhabu ya Mungu, ilikuwa imewagusa mno watu hata waalimu wale wakawa wamesahauliwa kwa muda fulani. Waliona ya kuwa Kristo alikuwa na uwezo ambao waliuhesabu kuwa ni wa Mungu peke yake; walakini tabia Yake iliyojaa upole na heshima ilikuwa na mwonekano dhahiri uliokuwa kinyume na kiburi chao. Wakawa wameudhika na kuaibika, wakatambua, ila hawakukiri,

kuwapo kwa kiumbe aliyekuwa mkuu kuliko wao. Kutoka nyumbani mwa Petro, walimomwona yule mwenye kupooza akiponywa kwa neno Lake [Kristo], wakaondoka kwenda zao kutunga hila mpya za kumnyamazisha Mwana wa Mungu.

Ugonjwa wa kimwili, japokuwa ulikuwa wa kufisha na ulikuwa umejizatiti, uliponywa kwa uweza wake Kristo; bali ugonjwa ule wa kiroho ulishikamana sana na wale waliofumba macho yao dhidi ya nuru ile. Ukoma na kupooza hayakuwa magonjwa ya kutisha sana kama ushupavu wao wa dini na kutokuamini.

Nyumbani kwa yule aliyeponywa ugonjwa ule wa kupooza kulikuwa na shangwe kuu aliporudi kwa familia yake, akibeba kwa urahisi kitanda chake alichokuwa amebewa juu yake kutoka mbele yao muda mfupi tu uliopita. Walimkusanyikia na kumzunguka wakiwa na machozi ya furaha, kwa shida wakijaribu kuyaamini macho yao. Akasimama mbele yao katika nguvu kamili ya uanaume. Mikono ile waliyokuwa wameiona kuwa haina uhai ilikuwa tayari kutii upesi mapenzi yake. Nyama za mwili wake zilizokuwa zimesinyaa na kuwa na rangi ya kijivu sasa zikawa mwili wenye afya na wenye rangi nyekundu [yenye afya]. Alitembea kwa hatua za ukakamavu, na uhuru. Furaha na tumaini viliandikwa katika kila umbo la uso wake; na mwonekano wa usafi [wa maisha] na amani vikawa vimechukua mahali pa alama zile za dhambi na mateso. Shukrani zilizojaa furaha zikapanda juu kutoka katika nyumba ile na Mungu akatukuzwa kupitia kwa Mwana Wake, aliyekuwa amemrejeshea tumaini mtu yule aliyekuwa hana tumaini, na kumpa nguvu yule aliyekuwa amepatikana na udhaifu. Mtu huyu na familia yake wakawa tayari kuyatoa mhanga maisha yao kwa ajili ya Yesu. Hakuna shaka lo lote lililoweza kuizima imani yao, hakuna kutokuamini ko kote kulikoathiri ahadi yao ya kumtumikia Yeye [Kristo] kwa moyo wote, yule aliyewaletea nuru katika nyumba yao yenye giza.

---- Ellen G. White, THE DESIRE OF AGES, Pages 262-271.

"Thou Canst Make Me Clean"

KIPINDI KIKUU CHA UNABII

=====

MIAKA 2300 YA DANIELI 8:14

Agizo kwa malaika Gabrieli lilikuwa hivi: "Mfahamishe mtu huyu maono haya." Danieli 8:16. Kwa hiyo, katika maelezo ya malaika huyu juu ya maono ya Danieli 8, bila shaka tunapaswa kupata ufafanuzi wa kipindi hiki cha unabii cha miaka 2300. Yatupasa kukumbuka pia ya kwamba mwisho wa kipindi hiki unaonyesha mwanzo wa kazi ya hukumu mbinguni, au kutakaswa kwa Patakatifu.

Walakini, sura hii ya nane inafunga bila kutaja mwanzo wa kipindi hicho cha wakati [wa miaka 2300], ambao ni kipimo cha maana sana cha unabii. Malaika yule alikuwa ameeleza mifano inayowakilisha Umedi-Uajemi, Uyunani, na Rumi. Alikuwa ameongelea sana juu ya kazi ile ya Mpinga Kristo ambayo ingejitokeza. Lakini alikuwa ameacha sehemu ile iliyohusu WAKATI wa kipindi hiki cha unabii bila kutoa maelezo yo yote, isipokuwa kusema tu kwamba ulikuwa ni "wakati ujao," na ya kwamba ungekuwa "baada ya siku nyingi" ----- mbele sana baadaye.

Hapa malaika aliacha [kusema], kwa kuwa Danieli alikuwa amezimia. Kiroho nabii huyu alikuwa ameangaza macho yake juu ya pambano lile la UASI MKUU dhidi ya kweli ya Mungu katika vizazi vyote, na ni dhahiri lilikuwa limemwondolea nguvu yote iliyokuwa ndani yake. Danieli alikifunga kisa cha maono haya kwa maneno haya: "Nami naliyastaajabia yale maono, ila hakuna aliyefahamu." Fungu la 27.

Walakini yule malaika alikuwa ameagizwa ku"mfahamish[a] mtu huyu maono haya"; na, kama ilivyoandikwa katika sura inayofuata, Gabrieli akamtokea nabii huyu na kumwambia maneno haya:

"Ee Danieli, nimetokea sasa, ili nikupe akili upate kufahamu....basi ITAFAKARI HABARI HII, NA KUYAFAHAMU MAONO HAYA." Danieli 9:22,23.

Mara moja yule malaika akaanza kushughulika na suala lile la wakati katika unabii huu. Hilo lilikuwa ni jambo lile lile la sura ile ya nane ambalo [Gabrieli] alikuwa bado hajamfanya Danieli kufahamu. Kwa hiyo, maono yale ya miaka 2300 ndilo jambo linalozungumzwa hapa.

## MWANZO WAKE

Kwanza kabisa, malaika alisema kwamba kipindi kifupi kingekatwa kutoka katika kipindi kile kirefu, na kuamriwa [kugawanywa] juu ya Wayahudi. Kipindi hiki kifupi kilikusudiwa kufika hadi wakati ule atakapokuja Masihi na kujazwa kwa kikombe cha maovu ya Yerusalemu. Maneno ya nabii [Danieli] ni haya:

"Muda wa majuma sabini [siku 490 za unabii, au miaka halisi 490] umeamriwa [umekatwa, kama neno "umeamriwa" linavyoamaanisha] juu ya watu wako, na juu ya mji wako mtakatifu, ili kukomesha makosa, na kuishiliza dhambi, na kufanya upatanisho kwa ajili ya uovu, na kuleta haki ya milele, na kutia muhuri maono ya unabii, na kumtia mafuta Yeye aliye Mtakatifu." Fungu la 24.

Kipindi hiki "kilichokatwa" cha miaka 490 kilifunika historia ya watu wa Yerusalemu [Wayahudi] mpaka hapo watakapokijaza kikombe chao cha maovu. Kipindi pekee cha unabii ambacho kutokana nacho miaka hii 490 inaweza kusemwa kwa usahihi kwamba "imekatwa," bila shaka, ni kipindi kile kirefu zaidi cha miaka 2300, ambacho kinakwenda mbali mbele hadi kuufikia ule "wakati wa mwisho." Kwa hiyo, miaka 490 na miaka 2300 haina budi kuanza kwa wakati ule ule mmoja.

Kilikuwa ni kipindi hiki cha wakati ambacho malaika Gabrieli alikuwa bado hajakieleza, naye akaanza kutoa maelezo yake kwa kuonyesha kwamba miaka ile 490 ya mwanzo ya kipindi kile [kirefu] ingezifikia siku zile za Masihi. Kisha akataja tukio ambalo lilionyesha mwanzo wa miaka hiyo 490, tukio ambalo pia halina budi kuonyesha mwanzo wa ile miaka 2300.

Hilo ndilo [Gabrieli] aliloagizwa kumfanya Danieli "kufahamu" maono hayo ya miaka 2300 yalipotolewa kwake kwanza. Sasa anamwambia "ayafahamu":

"Basi ujue na kufahamu, ya kuwa tangu kuwekwa AMRI ya kutengeneza na kuujenga upya Yerusalemu hata zamani zake Masihi aliye Mkuu; kutakuwa na majuma saba; na katika majuma sitini na mawili utajengwa tena pamoja na njia kuu zake na handaki, naam, katika nyakati za taabu. Na baada ya yale majuma sitini na mawili, Masihi atakatiliwa mbali, naye atakuwa hana kitu; na watu wa mkuu atakayekuja watauangamiza mji, na Patakatifu; na mwisho wake utakuwa pamoja na gharika, na hata mwisho ule vita vitakuwapo; ukiwa umekwisha kukusudiwa." Danieli 9:25,26.

Kwa hiyo, tarehe ya kutolewa amri ile ya kutengeneza na kuujenga upya Yerusalemu ndiyo tarehe ya kuanza ule mstari wa kupimia wakati wa unabii. Miaka 490 ya mwanzo wa kipindi hicho ingeufikia wakati ule na kazi Yake Masihi alipokuja mara ya kwanza. Mwisho wa miaka ile 2300 ulionyesha mwanzo wa saa ya hukumu kule mbinguni. Maadam mahali pa kuanzia pamewekwa, basi, matukio yote ya kipindi kile kirefu hayana budi kufuatana sawasawa kama yalivyotolewa katika ratiba hiyo ya unabii wa Mungu.

## TAREHE YA MWANZO WA KUUTENGENEZA YERUSALEMU

Palikuwa na amri kadhaa zilizotolewa kuhusu kuutengeneza Yerusalemu baada ya utumwa ule wa Babeli kukoma. Koreshi, na Dario, na Artashasta Longimano (Longimanus) kila mmoja alitoa amri kama hiyo. Ipi inayojibu lugha ya unabii huu isemayo "amri ya kutengeneza na kuujenga upya Yerusalemu"?

Amri ya Artashasta ilikuwa na mambo mengi sana ndani yake (Ezra 7), ikiruhusu kurejesha kikamilifu MAMLAKA YA SERIKALI NA DINI katika Yerusalemu na Yudea. Na Maandiko haya yaliyovuviwa yanasema kwa maneno machache tu kwamba amri zote hizo zimetimizwa kwa amri ile ya Artashasta, ambayo ndiyo "AMRI" hasa iliyotoa madaraka:

"Wakajenga, wakaimaliza kazi yao, kwa maagizo ya Mungu wa Israeli, na kwa amri ya Koreshi, na Dario, na Artashasta mfalme wa Uajemi." Ezra 6:14.

Kulingana na Maandiko haya, utimilifu wa "kuwekwa amri ya kutengeneza na kuujenga," unanzia kwa amri hii ya Artashasta. Na amri hii ilitolewa "katika mwaka wa saba wa mfalme Artashasta." Ezra 7:7.

Ni mwaka gani uliokuwa mwaka wa saba wa [mfalme] Artashasta ----- tarehe ambayo ni ya muhimu sana kwetu ili kuweza kukadiria mwaka huo bila kuwa na mashaka yo yote?

Kanuni kuu ya taratibu ya miaka ya wafalme wa enzi zile za kale ni Kanuni (Canon), au Sheria ya Historia ya Ptolemy. Ptolemy alikuwa mwanahistoria Mgiriki, mwanajiografia, na mtaalam wa mambo ya nyota (astronomer), ambaye aliishi katika Hekalu la Serapis, karibu na Alexandria, Misri. Kutokana na kumbukumbu za kale alitayarisha orodha ya Wafalme wa Babeli, Uajemi, Uyunani, na Rumi (akiiendeleza orodha ya Kirumi mpaka kufikia wakati wake, ambao ulikuwa ni karne ile ya pili baada ya Kristo).

Pamoja na orodha yake ya wafalme na miaka ya kupokezana kwao, Ptolemy alitayarisha kumbukumbu ya uchunguzi wa kale wa kupatwa kwa mwezi au jua. Kwa mfano, angeandika kwamba katika mwaka fulani wa mfalme fulani, siku fulani ya mwezi, palitokea kupatwa kwa mwezi au jua. Wataalam wa nyota wamefanya mahesabu ya kumbukumbu hizo [za Ptolemy], na kuzithibitisha. Msomi Dkt. William Hales alisema:

"Kwa usahihi wa nakala hizi za Kanuni (Canon) ya Ptolemy, ushuhuda wenye nguvu kabisa umetolewa kwa kupatana kabisa, tarehe zaidi ya ishirini, na hesabu za kupatwa kwa mwezi au jua katika makala za Ptolemy zilizojengwa juu ya elimu ya zamani sana (Almagest)."

----- CHRONOLOGY, Vol.I, uk.166.

Hivi ndivyo asemavyo James B. Lindsay, Mtaalam wa Elimu Wendo (chronologist) Mwingereza, "msingi umewekwa kwa Elimu Wendo (chronology) ambao ni wa hakika kama zilivyo nyota." Kwa hiyo, jua na nyota, watunza wakati hao walioteuliwa na Mungu, wanatoa ushuhuda wao kuhusu usahihi wa kumbukumbu hii ya kihistoria.

Tunamshukuru Mungu kwa jambo hilo, kwa vile tunatamani kujua kama tunaweza kuitegemea Kanuni hiyo ya Ptolemy ili kutusaidia kukadiria kwa hakika mwaka ule wa saba wa Artashasta.

Kwa mujibu wa Ptolemy, Artashasta alirithi kiti cha enzi katika mwaka wa mia mbili na themanini na nne kwa kanuni hiyo. Kwa hesabu za kisasa, mwaka huu wa mia mbili na themanini na nne unanzia Desemba 17, 465 K.K. mpaka Desemba 17, 464 K.K.. Kanuni hiyo haituelezi ni wakati gani wa mwaka huo mfalme huyo aliporithi kiti hicho cha enzi; inashughulika tu na miaka kamili. Ili kuwa na hakika, swali hasa ni hili: Je, Artashasta alikalia kiti cha enzi mwezi ule wa Desemba, 465 K.K. au wakati fulani katika mwaka ule wa 464 K.K.? Ni majira gani ya mwaka mfalme huyo aliporithi kiti cha enzi?

Wanahistoria wengine, wakiwa wanalishughulikia jambo hili kwa kukisia tu, wanaweka tarehe ya [mfalme huyo] kurithi kiti cha enzi kuwa ni mwaka ule wa 465 K.K. Lakini tunaposhughulika na unabii wa Mungu, tunahitaji kuwa na hakika na mahali tunapoweza kuanza kuhesabu mwaka huo wa saba wa Artashasta, ambao kwa huo kipindi cha unabii huu kinaanzia.

Na kwa maongozi ya Mungu tunayo hakika. Katika wafalme wote wa Ashuru, Babeli, na Umedi-Uajemi, katika orodha ile ndefu ya Ptolemy, yuko mmoja ambaye kukalia kiti chake cha enzi kunatupa wakati ule ule wa mwaka katika Maandiko ----- na huyo ni Artashasta. Huyo ndiye mtu mmoja ambaye tunahitaji kujua kwa hakika majira ya mwaka [aliporithi kiti chake cha enzi], ili tuweze kuiweka tarehe iliyo ya muhimu kwa unabii huu, naye ni mtu ambaye Maandiko haya yaliyovuviwa yanatupa habari zake halisi. Ni nani anayeweza kushindwa kuuona mkono wa Mungu katika jambo hili?

Kumbukumbu ya pamoja ya Nehemia 1:1; 2:1 na Ezra 7:7-9\*, huonyesha kwamba Artashasta alikalia kiti cha enzi kati ya mwezi wa tano wa mwaka wa Kiyahudi na mwezi wa tisa ----- kwa kukisia tu, ni kati ya Agosti na Desemba ----- au katika majira ya kupukutika kwa majani (Autumn). Biblia inatupatia sehemu moja ya kumbukumbu, na Kanuni ile ya Ptolemy inatupatia sehemu nyingine; basi, kwa kumbukumbu ya pamoja tunajua ya kwamba Artashasta alikalia kiti cha enzi mwishoni mwa mwaka 464 K.K., na kwa hiyo, mwaka wa saba wa utawala wake ungekuwa ni ule mwaka wa 457 K.K..

Huu ndio mwaka uliowekwa na vianzo vingine vya Elimu ya Wendo inayoaminika. Bwana Isaac Newton alifanya mahesabu kwa kutumia njia kadhaa za ushahidi kutokana na mamlaka za kale na katika kila njia aliufikia mwaka 464 K.K. kama ndio mwaka wa kwanza wa utawala wa Artashasta, ambao unaufanya mwaka wa saba kuwa mwaka 457 K.K.

Amri hii ilitolewa kwa madhumuni ya kutengeneza na kuujenga upya Yerusalemu katika mwaka ule wa saba wa utawala wa Artashasta. Tukio hilo linauweka mwanzo wa ile miaka 2300, na pia mwanzo wa kipindi kile cha miaka 490 ambacho kilikatwa kutoka katika kipindi hicho [kirefu] kwa ajili ya Wayahudi.

Kwa hiyo, mwaka ule wa 457 K.K. ni tarehe [mwaka] muhimu sana. Unasimama kama jiwe la maili la dhahabu katika Baraza lile la Kale (Forum) kule Rumi, kutoka kwalo umbali wote ulipimwa kwenda kwenye miisho ya dola ile. Kuanzia tarehe [mwaka] hiyo, 457 K.K. zinatoka kamba za dhahabu za [kupimia] wakati wa unabii huu. Kamba hizo zinagusa matukio katika maisha ya Yesu hapa duniani na huduma yake kule mbinguni, mambo ambayo yana faida yenye kina cha milele kwa wanadamu wote leo hii.

----- W. A. Spicer, OUR DAY IN THE LIGHT OF PROPHECY, Sura 21, uk.172-178, Signs of the Times Publishing Assn, (1952), Canada.

\* Mafungu haya huonyesha kwamba mfalme huyo alikuja kwenye kiti chake cha enzi katika majira yale ya kupukutisha majani (Autumn), hivyo miaka ya utawala wake ingeweza kuhesabiwa kuanzia majira yale ya kupukutisha majani hadi majira ya kupukutisha majani. Nehemia 1:1 [fungu hili] linaanza kuielezea kumbukumbu hiyo hivi: "Ikawa katika mwezi wa Kisleu, MWAKA WA ISHIRINI." Nehemia 2:1 linaendelea kueleza hivi: "Ikawa katika mwezi wa Nisani, MWAKA WA ISHIRINI wa Artashasta." Hivyo ni wazi kwamba katika kalenda ya miezi ya utawala halisi wa Mfalme huyo mwezi ule wa Kisleu ulikuja kwanza katika mpangilio wake, kisha ukaja mwezi wa Nisani. Kisleu ulikuwa ni mwezi wa tisa wa mwaka mtakatifu wa Kiyahudi, kwa kukadiria ni Desemba. Nisani ni mwezi wa kwanza, Aprili. Na miezi hiyo, Desemba, Aprili, ----- katika mpangilio huo, ----- ilikuja katika mwaka wa kwanza [wa utawala] wa mfalme [Artashasta], na kusema kweli, ni sawa na mwaka wake [umri wake] wa ishirini. Na katika mwaka ule ule ulikuja mwezi wa tano, Agosti; kwa maana Ezra 7:7-9 huonyesha kwamba mwezi ule wa kwanza na wa tano ----- kwa mpangilio ule ----- iliangukia pia katika mwaka ule ule wa utawala wake. Basi, tunajua kwa hakika kwamba utawala wake ulianza mahali fulani kati ya Agosti na Desemba, yaani, katika majira yale ya kupukutisha majani. Mwaka wa kwanza wa Artashasta ulianza sehemu ya mwisho ya 463 K.K., basi, mwaka wa saba, ukihesabiwa kwa urahisi, ungeanzia karibu na mwisho wa 458 hadi karibu na mwisho wa 457. Kwa amri ya Ezra, watu walianza kupanda kwenda Yerusalemu katika majira yale ya kuchipua (Spring) ya mwaka ule wa 457 K.K. (katika mwezi wa kwanza, au Aprili), nao wa "kafika Yerusalemu mwezi wa tano" (Agosti). Ezra 7:8,9. Ezra na wenzake mara tu baada ya hapo "wakawapa manabu wa mfalme, na maliwali wa ng'ambo ya Mto, maagizo ya mfalme; nao wakawapa watu, na nyumba ya Mungu, msaada." Ezra 8:36. Amri hiyo ya kutengeneza na kuujenga upya Yerusalemu, kwa hakika, ilikuwa imetolewa kikamilifu, wakati walipowapa maagizo ya mfalme. Na kuanzia tarehe [mwaka] hii, 457 K.K. kinaanza kile kipindi kikuu cha unabii huu.

## KUJA KWA KRISTO MARA YA PILI

"ATATOKEA MARA YA PILI, pasipo dhambi, kwa hao wamtazamiao kwa wokovu." Waebrania 9:28.

Mara nyingi sana kuja kwa Kristo mara ya pili huangaliwa tu kama fundisho la dini. Ni zaidi ya fundisho la dini. Ni tukio lililo karibu sana kutokea ----- jambo ambalo litatokea duniani. Bila swali, hili ni tukio kubwa mno na linayapita yote tangu Kristo alipokuja mara ya kwanza na kufa Kalvari kwa ajili ya dhambi za wanadamu.

Kuja kwa Kristo mara ya pili, kama kuja kwake mara ya kwanza, limekuwa somo kuu la unabii wa Mungu tangu mwanzo. Jambo hilo lilitiliwa mkazo na Mtume Petro katika hubiri lake la pili lililoandikwa. Aliwasisitizia watu wale wa Yerusalemu ukweli kwamba mambo yale "aliyohubiri Mungu tangu zamani kwa kinywa cha manabii wake wote, ya kwamba Kristo Wake aliteswa" (Matendo ya Mitume 3:18), yalikuwa yametimizwa kabisa mbele ya macho yao. Hakuna neno hata moja ambalo halikutimia. Alisema kwamba vivyo hivyo mambo yote waliyoyanena manabii juu ya kuja Kwake mara ya pili yangetimizwa.

"Apate kumtuma Kristo Yesu mliyewekewa tangu zamani; ambaye ilimpasa kupokewa mbinguni hata zije zamani za kufanywa upya vitu vyote, zilizonenwa na Mungu kwa kinywa cha manabii Wake watakatifu tokea mwanzo wa ulimwengu." Matendo ya Mitume 3:20,21.

## AHADI YA KUJA KWAKE

Maovu yalipozidi kuongezeka sana Mungu alituma ujumbe Wake kwa watu wale walioishi kabla ya Gharika, akitangaza kwamba kuja kwa Kristo katika utukufu kungekomesha utawala wa dhambi: "Na Henoko, mtu wa saba baada ya Adamu, alitoa maneno ya unabii juu ya hao, akisema, Angalia, Bwana alikuja na watakatifu wake, maelfu, ili afanye hukumu juu ya watu wote." Yuda 14,15.

Ahadi ya kuja kwake Kristo ilikuwa ndilo "tumaini lenye baraka" katika kizazi kile cha mababa zetu. Katika saa ile ya giza ya majaribu ya Ayubu moyo wake uliishikilia ahadi hii, naye alilindwa asikate tamaa: "Mimi najua ya kuwa Mteteaji wangu yu hai, na ya kuwa hatimaye atasimama juu ya nchi... Nami nitamwona, mimi nafsi yangu, na macho yangu yatamtazama, wala si mwingine." Ayubu 19:25-27.

Mtunga Zaburi aliimba habari Zake:

"Mungu wetu atakuja wala hatanyamaza, moto utakula mbele zake, na tufani yavuma sana ikimzunguka pande zote." Zaburi 50:3.

Manabii wa nyakati za baadaye za Agano la Kale, nao walivuviwa kunena na kuandika juu ya tukio lile la mwisho wa dunia. Walisema juu ya utukufu wake, na maandalizi ambayo yangetakiwa kufanywa kukutana nalo.

"Nimeweka walinzi juu ya kuta zako, Ee Yerusalemu; hawatanyamaza mchana wala usiku; ninyi wenye kumkumbusha BWANA, msiwe na kimya." "Tazama, BWANA ametangaza habari mpaka mwisho wa dunia, Mwambieni binti Sayuni, Tazama, wokovu wako unakuja; Tazama, thawabu Yake i pamoja naye, Na malipo Yake yako mbele Zake." Isaya 62:6,11.

Ujumbe huu wa kuja Kwake unatakiwa kutangazwa mpaka MWISHO WA DUNIA; kwa maana hiyo ndiyo "HABARI NJEMA YA FURAHA KUU" kwa kila mmoja atakayeipokea.



Usiku ule kabla ya kusulibiwa Kwake, Yesu "alihuzunika, kiasi cha kufa." Mzigo wa dhambi zetu zote ulikuwa karibu kuwekwa juu Yake. Wakati kama huo, upendo wa Kristo kwa waliokombolewa walio Wake ulifanya wazo lile la kuja Kwake mara ya pili kuwa kuu kuliko yote moyoni mwake. Angekuja kuwakusanya waaminifu Wake na kuwaingiza katika ufalme Wake, wakiwa salama mbali na dhambi zote na taabu. Alisema:

"Msifadhaike mioyoni mwenu; mnamwamini Mungu, niaminini na Mimi. Nyumbani mwa Baba yangu mna makao mengi; kama sivyo, ningaliwaambia; maana naenda kuwaandalia mahali. Basi mimi nikienda na kuwaandalia mahali, nitakuja tena niwakaribishe kwangu; ili nilipo mimi, nanyi mwepo." Yohana 14:1-3.

Moyo unatulia katika uthibitisho huo. Loo! ni ahadi ya thamani ilioje, "Nitakuja tena"! "Ninakuja kwa ajili yenu," huo ndio UJUMBE UNAOCHANGAMSHA MOYO. "Naam, Bwana," nasi tunajibu, "tutangoja, na kukesha, na kujiweka tayari, kwa neema Yako."

## JINSI ATAKAVYOKUJA

Kuja kwa Kristo mara ya pili kutaonekana kwa ulimwengu wote. Hakuna siri yo yote wala fumbo lo lote juu ya jambo hilo. Mwandishi wa kitabu cha Ufunuo asema hivi: "Tazama, yu aja na mawingu; na KILA JICHO LITAMWONA." Ufunuo 1:7.

Kristo Mwenyewe alilielezea tukio hilo kwa wanafunzi Wake kama litakavyoonekana machoni pa wote: "Kwa maana KAMA VILE UMEME UTOKAVYO MASHARIKI UKAONEKANA HATA MAGHARIBI, HIVYO NDIVYO KUTAKAVYOKUWA KUJA KWAKE MWANA WA ADAMU." Mathayo 24:27. Hapo ndipo WATAKAPOMWONA Mwana wa Adamu akija mawinguni kwa nguvu nyingi na utukufu." Marko 13:26.

SIKU ILE YA BWANA ----- kufungwa kwa mlango wa rehema [toba], kumwagwa kwa hukumu za mwanzo za Mungu ----- mambo hayo yatakuja "kama mwivi usiku." Lakini kuja Kwake mara ya pili hakutakuwa kwa siri. Mbingu zitafunguka, nchi itatetemeka, na parapanda ya Mungu italia na kutoa mwanzi wake ulimwenguni kote [wote wataisikia]. Hakuna jicho la mwanadamu ye yote lililopata kuona utukufu kama huo utakaonekana ghafula juu ya ulimwengu huu hapo Yesu atakapokuja kama Mfalme wa wafalme na Bwana wa mabwana.

Mungu anapenda sisi tuelewe kwamba huyo Mmoja anayekuja katika "nguvu na utukufu" [si mwingine bali] ni Mwokozi yule yule wa wanadamu ambaye zamani alitembea kando ya bahari ile ya kibuluu ya Galilaya. Wanafunzi wake walipomtazama Mwokozi wao, na wetu, akipaa kimwili kwenda mbinguni kutoka katika Mlima ule wa Mizeituni mpaka "wingu [kundi la malaika] likampokea kutoka machoni pao," na mara hiyo malaika wawili wakasimama karibu nao, na kusema: Enyi watu wa Galilaya, mbona mmesimama mkitazama mbinguni? HUYU YESU [YESU

YUYU HUYU] aliyechukuliwa kutoka kwenu kwenda juu mbinguni, atakuja JINSI IYO HIYO mlivyomwona akienda zake mbinguni." Matendo ya Mitume 1:9,11.

"Huyu Yesu [Yesu YUYU huyu]!" Yule aliyekuwa anapaa kwenda mbinguni alikuwa rafiki ya wale Mitume na Kaka [Yetu] Mkubwa ----- akiwa ndiye Mwana wa Adamu na Mwana wa Mungu pia. Lakini kulingana na ahadi hiyo tukufu atakuja tena kwa utukufu usioelezeka, akiwa na "malaika watakatifu WOTE pamoja naye."

Waliokombolewa watakapomwona yule aliyesulibiwa kwa ajili yao akija katika utukufu Wake, watapiga kelele, wakisema, "TAZAMA, HUYU NDIYE MUNGU WETU, NDIYE TULIYEMNGOJA ATUSAIDIE; HUYU NDIYE BWANA TULIYEMNGOJA, NA TUSHANGILIE NA KUUFURAHIA WOKOVU WAKE." Isaya 25:9.

Matukio ya siku ile kuu yanapita ufahamu wa kibinadamu hata ni vigumu kutambua kwamba wakati kama huo uko mbele yetu kweli.

## KUSUDI LA KUJA KWAKE

Maandiko hayatuachi katika mashaka yo yote kuhusu kusudi la kuja Kwake Kristo mara ya pili na matukio ya siku ile kuu. Limekuwa ndilo tumaini la wana [watoto] wa Mungu katika vizazi vyote. Mtume Paulo analiita "TUMAINI LENYE BARAKA."

"Maana neema ya Mungu iwaokoayo wanadamu wote imefunuliwa; nayo yatufundisha kukataa ubaya na tamaa za kidunia; tupate kuishi kwa kiasi, na haki na utauwa, katika ulimwengu huu wa sasa; tukilitazamia TUMAINI LENYE BARAKA na mafunuo ya utukufu wa Kristo Yesu, Mungu Mkuu na Mwokozi wetu." Tito 2:11-13.

Makundi na makundi ya watakatifu wamelala usingizi wa mauti [wamekufa] ----- imani yao ikitazama mbele hadi siku ile ya kufunuliwa [kuonekana kwa macho] Kristo katika utukufu Wake. Hivyo ndivyo ilivyokuwa kwa mzee yule mwenye hekima, Mtume Paulo, kwamba naye akafa, macho yake yakiwa yamekazwa juu ya "siku ile."

"Kwa maana, mimi sasa namiminwa [nachinjwa kama kafara], na wakati wa kufariki kwangu umefika. Nimevipiga vita vilivyo vizuri, mwendo nimeumaliza, Imani nimeilinda; baada ya hayo NIMEWEKEWA TAJI YA HAKI, ambayo Bwana, mhukumu mwenye haki, atanipa SIKU ILE; wala si mimi tu, bali na watu wote pia waliopenda KUFUNULIWA [KUJA] Kwake." 2 Timotheo 4:6-8.

Kuja kwa Kristo mara ya pili ni MWISHO MTUKUFU WA MPANGO ULE WA WOKOVU. Hapo ndipo wana [watoto] wa Mungu watakapokaribishwa katika UFALME ULE WA MILELE. Hapo ndipo wale waliookolewa watakapoingia kupitia katika milango ya mji ule mtakatifu. Hapo ndipo TAJI ZA UZIMA zitakapotolewa. Hapo ndipo baba yule wa zamani na nabii, mtume na

mwanamatengenezo, pamoja na watakatifu wa "siku za mwisho" watakapopokea thawabu zao. Kuhusu wastahiki wale wa kale imeandikwa hivi: "Na watu hao wote wakiisha kushuhudiwa kwa sababu ya imani yao, hawakuipokea ahadi; kwa kuwa Mungu alikuwa ametangulia kutuwekea sisi kitu kilicho bora, ili wao wasikamilishwe pasipo sisi." Waebrania 11:39,40.

Ni kwa kusudi la kuwachukua watoto Wake kwenda nao kwenye makao yale ya milele ndio maana Kristo anakuja mara ya pili. Hii ndiyo ilikuwa ahadi Yake kwa wanafunzi Wake: "Maana naenda KUWAANDALIA MAHALI... NITAKUJA TENA NIWAKARIBISHE KWANGU; ili nilipo Mimi, nanyi mwepo." Yohana 14:2,3.

Si kwa kutaja kila kitu, bali ni kwa kufuata mpangilio wake, hebu na tuyafuatie matukio ya siku ile kuu.

## KUJA KWAKE KUTUKUFU

Yohana, mwandishi wa kitabu cha Ufunuo, aliona katika maono, kama ilivyo, mwanzo wa siku ile ya mwisho:

"Sauti kuu ikatoka katika Hekalu, katika kile kiti cha enzi, ikisema, IMEKWISHA KUWA. Pakawa na umeme na sauti ya radi; na palikuwa na tetemeko la nchi kubwa, ambalo tangu wanadamu kuwako juu ya nchi hapakuwa na namna ile... na MIJI ya mataifa IKAANGUKA; na BABELI ULE MKUU ukakumbukwa mbele za Mungu." Ufunuo 16:17-19.

"Mbingu zikaondolewa kama ukurasa ulivyokunjwa, na kila mlima na kisiwa kikahamishwa kutoka mahali pake." Ufunuo 6:14.

Mwandishi wa kitabu cha Ufunuo aliona jambo fulani kuhusu utukufu wa Mwokozi ambao utaiangaza dunia [yote] kwa ghafula wakati ule wa kuja Kwake mara ya pili:

"Ndipo itakapoonekana ishara Yake Mwana wa Adamu mbinguni; ndipo MATAIFA YOTE ya ulimwengu WATAKAPOOMBOLEZA, nao watamwona Mwana wa Adamu akija juu ya mawingu ya mbinguni pamoja na NGUVU NA UTUKUFU MWINGI." Mathayo 24:30.

"Kisha nikaona, na tazama, wingu jeupe, na juu ya wingu hilo ameketi Mmoja, mfano wa MWANADAMU, mwenye taji ya dhahabu juu ya kichwa chake [Yesu Kristo], na katika mkono wake mundu mkali. Na malaika mwingine akatoka katika HEKALU, akimlilia kwa sauti kuu yeye aliyekuwa ameketi juu ya lile wingu, Tia mundu wako, ukavune; kwa kuwa SAA YA KUVUNA IMEKUJA; kwa kuwa MAVUNO YA NCHI [WATAKATIFU] YAMEKOMAA." Ufunuo 14:14,15.

## UFUFUO NA KUBADILISHWA GHAFULA

Wakati wa mavuno umekuja na ngano [watakatifu] hatimaye inakusanywa na kuwekwa katika ghala yake [nyumbani mwake] Bwana:

"Hatutalala [hatutakufa] sote, lakini tutabadilika, kwa dakika moja, kufumba na kufumbua, wakati wa parapanda ya mwisho; maana PARAPANDA italia, na WAFU WATAFUFULIWA, WASIWE NA UHARIBIFU, NASI TUTABADILIKA." I Wakorintho 15:51,52.

"Kwa kuwa twawaambieni haya kwa neno la Bwana, kwamba sisi TULIO HAI, TUTAKAOSALIA HATA WAKATI WA KUJA KWAKE BWANA, hakika HATUTAWATANGULIA WALIOKWISHA KULALA MAUTI [wala wao hawatatutangulia]. Kwa sababu Bwana Mwenyewe [Kristo] atashuka kutoka mbinguni pamoja na MWALIKO [SAUTI KUU YA KUPASUKA], na sauti ya MALAIKA MKUU [KRISTO], na parapanda ya Mungu; nao WALIOKUFA KATIKA KRISTO WATAFUFULIWA KWANZA. KISHA SISI TULIO HAI, TULIOSALIA, TUTANYAKULIWA PAMOJA NAO katika mawingu, ili TUMLAKI BWANA HEWANI; na hivyo tutakuwa pamoja na Bwana milele. Basi, farijianeni kwa maneno hayo." I Wathesalonike 4:15-17(18).

"Naye atawatuma MALAIKA ZAKE pamoja na sauti kuu ya parapanda, nao WATAWAKUSANYA WATEULE WAKE toka pepo nne [pande nne za dunia] toka mwisho huu wa mbingu mpaka mwisho huu." Mathayo 24:31.

Wenye haki waliokufa watafufuliwa na kupewa uzima wakati wa sauti ile ya KRISTO, MALAIKA MKUU, itakapoenea duniani kote. "Makaburi ya zamani yaliyoota majani" yanawatoa mateka [wafu] wake kwa amri ya Mtoaji-Uzima [Kristo]. Na zaidi ya hayo: wakati hautakuwa mrefu wa kutosha kushuhudia tukio jingine la makaburi.

Pamoja na wale "watakatifu wanaolala [mauti]" hapo Kristo atakapokuja, wapo "wenye haki walio hai." Hao watabadilishwa kwa ghafula kutoka katika mwili wao unaokufa na kupewa mwili usiokufa ----- kutoka katika hali ya kufa waliyo nayo wanadamu wote kwenda katika hali ya wanadamu wasioweza kufa. Hapo ndipo wote kwa pamoja [makundi hayo mawili ----- waliofufuliwa na walio hai] wakisindikizwa na malaika, wataandamana na Mwokozi kwenda naye kwenye makao yale ya mbinguni ambayo amewaandalia katika mji ule wa Mungu [Yerusalemu Mpya].

KUANGAMIZWA KWA WAOVU

Hakuna dhambi inayoweza kustahimili mbele ya utukufu adhimu wa Mfalme yule ajaye, kwa maana imeandikwa: "Mungu wetu ni moto ulao." LEO ndiyo siku ya mwenye dhambi ya rehema. LEO kama kwa imani ataungama dhambi zake, Mungu ataziteketeza moyoni mwake. Lakini kama hatafanya hivyo, mwenye dhambi huyo asiyekuwa na toba atateketezwa kwa moto pamoja na dhambi zake.

Hii ndiyo ile siku kuu iliyotabiriwa zamani na waonaji na manabii.

Hebu na tusome maelezo kuhusu itakavyomaanisha [itakavyokuwa] kwa wale wasiookolewa watakapomwona Kristo akija katika utukufu wake. Hakika, hofu ya siku ile haina budi kutuonya sisi sasa kukaa katika kivuli cha neema ya pendo lake Mwokozi.

"Na wafalme wa dunia, na wakuu, na majemadari, na matajiri, na wenye nguvu, na kila mtumwa, na mwungwana, **WAKAJIFICHA KATIKA PANGO NA CHINI YA MIAMBA YA MILIMA, WAKIAMBIA MILIMA NA MIAMBA TUANGUKIENI, TUSITIRINI, MBELE ZA USO WAKE YEYE AKETIYE JUU YA KITI CHA ENZI, NA HASIRA YA MWANA KONDOO.** Kwa maana **SIKU ILIYO KUU**, ya hasira yao, **IMEKUJA**; naye ni nani awezaye kusimama?" Ufunuo 6:15-17.

Utukufu ule ule unaowabadilisha wenye haki ni moto ulao kwa wale waliokataa wokovu wake Kristo:

"Hapo ndipo atakapofunuliwa yule Asi [Mpinga Kristo], ambaye Bwana Yesu atamwua kwa pumzi ya kinywa chake, na kumwangamiza kwa Ufunuo wa kuwapo Kwake." 2 Wathesalonike 2:8.

"Wakati wa kufunuliwa kwake Bwana Yesu kutoka mbinguni pamoja na malaika wa uweza wake; **KATIKA MWALI WA MOTO; HUKU AKIWALIPIZA KISASI WAO WASIOMJUA MUNGU, NAO WASIOITII INJILI YA BWANA YESU** [hawatapewa nafasi nyingine ya kuhubiriwa Injili]; watakaoadhibiwa kwa **MAANGAMIZI YA MILELE**, kutengwa na uso wa Bwana na utukufu wa nguvu zake." 2 Wathesalonike 1:7-9.

Siku ile itakuwa ni siku ya giza na siku ya nuru pia. Waovu, wakiwa wamechelewa mno, ndipo watakapotambua kile walichopoteza kwa kuukataa mvuto ule wa upendo wa Kristo, amani na msamaha wake. Wataona ya kwamba wameidharau njia pekee ambayo kwayo wangukuwa wamejitayarisha kuwa na nafasi katika umilele wake Mungu. Hapo ndipo watakapoomboleza: "Mavuno yamepita, wakati wa hari umekwisha, wala sisi **HATUKUOKOKA.**" Yeremia 8:20. Watatamka maneno ya kuhuzunisha sana yawezayo kunenwa ama kuandikwa kwa kalamu, "ingalikuwa hivyo kwetu sisi."

**MWISHO WA HISTORIA YA BINADAMU**

Kuja kwa Kristo mara ya pili kutaleta UFUFUO WA WENYE HAKI waliokufa na KUBADILISHWA GHAFULA KWA WENYE HAKI WALIO HAI. Tukio kuu lilo hilo litasababisha KIFO KWA WENYE DHAMBI WALIO HAI na KUIKOMESHA DUNIA. Ufufuo wa jumla wa WAOVU hautokei wakati huu. Walakini, kuna UFUFUO WA PEKEE wa "HAO WALIOMCHOMA." Ufunuo 1:7. Hao watafufuliwa ili kuona kuja kwake katika utukufu yule Mmoja [Kristo] waliyemsulibisha. Lakini hao WATAANGUKA [WATAKUFUFA] tena mbele ya utukufu ulao kama moto wa Kuwako Kwake [Kristo].

Watakatifu watachukuliwa kwenda kutawala pamoja na Kristo katika mji ule wa mbinguni kwa miaka ELFU MOJA. Katika kipindi chote kile dunia hii itakaa katika hali ya kuharibika na kuvurugika, bila kuwa na watu wa kukaa ndani yake, shimo lenye giza, gereza la kusikitisha la Shetani. Kuhusu fufuo hizo mbili, wa kwanza wa WENYE HAKI na kisha ule [wa pili] wa WAOVU, tunaambiwa hivi:

"Nao [wenye haki] WAKAWA HAI [WAKAFUFUKA], wakatawala pamoja na Kristo MIAKA ELFU. Hao wafu [waovu] waliosalia HAWAKUWA HAI [HAWAKUFUFUKA], hata ITIMIE ILE MIAKA ELFU. Huo ndio UFUFUO WA KWANZA [WA WENYE HAKI]. Heri na MTAKATIFU, ni yeye aliye na sehemu katika UFUFUO WA KWANZA; juu ya hao MAUTI YA PILI [ZIWA LA MOTO ---- UFUNUO 20:14] haina nguvu." Ufunuo 20:4-6.

Ni MWISHO wa miaka ile elfu moja utakapotokea UFUFUO WA WAOVU. Halafu MJI WA MUNGU UTASHUKA CHINI, "YERUSALEMU MPYA, UKISHUKA KUTOKA MBINGUNI KWA MUNGU" [Ufunuo 21:2]. Huo ndio wakati wa KUFUFUKA WAOVU ili wapate ADHABU yao ambayo ni MAUTI YA PILI, ambayo haina ufufuo.

"WAKATI ULIOKUBALIKA NDIO SASA"

Siku ya WOKOVU ndiyo SASA. SASA, kwa neema yake Kristo, tunaweza kujiweka tayari kwa siku ile kuu. Kuonekana miongoni mwa wale waliokombolewa walio Wake [Kristo] kutakuwa na thamani kubwa sana kuliko kitu cho chote ambacho ulimwengu huu unaweza kutoa, iwe ni anasa, au mali, au heshima. Hakuna kitakachokuwa na maana wakati ule isipokuwa tu lile TUMAINI LENYE BARAKA.

Selina, mke wa mkuu wa mkoa wa Huntingdon, alimpokea Mwokozi katika siku zile za uamsho wa Wamethodisti kule Uingereza. Mali yake yote pamoja na mvuto wake wote wa kijamii akavitoe wakf kwa Kristo. Walakini, baadhi ya rafiki zake wenye vyeo walichukizwa kwa uhusiano wake wa karibu na maskini na wanyonge walioupokea ujumbe wa saa ile na kujitahidi kuingia katika ufalme [wa Mungu]. Aliandika hivi juu ya furaha yake kwa kuhesabiwa pamoja na watoto wa Mungu:

"Napenda kukusanyika miongoni mwao sasa

Mbele ya kiti chako cha neema kusujudu,  
Japo mimi ni dhaifu kuliko wote;  
Wala siwezi kustahimili wazo linalonichoma,  
Kuona jina langu lisilofaa kabisa likiachwa,  
Wakati Wewe utakapowaita."

Usiku mmoja, wakati wa dansi rasmi ya kifalme, Mwana wa Mfalme aliyeishi Walesi (Prince of Wales) alimwuliza mke wa lodi mmoja mwenye cheo kuhusu mahali alipokuwa yule mke wa mkuu wa mkoa wa Huntingdon. "Ee, nadhani anaomba pamoja na baadhi ya ombaomba mahali fulani!" likawa ndilo jibu lake la kushtukia. "Oo!" akasema Mwana wa Mfalme, "siku ile ya mwisho nafikiri ya kwamba mimi ningekuwa mtu mwenye furaha kushika upindo wa vazi la mke mstahiki wa mkuu wa mkoa wa Huntingdon."

----- W.A. Spicer, OUR DAY IN THE LIGHT OF PROPHECY, Sura ya 4, Uk.34-43, Signs of the Times Publishing Assn, (1952), Canada.

The Second Coming of Christ.

PATAKATIFU PA MFANO (TYPE) NA PA ASILIA (ANTITYPE)

=====

JENGO LENYEWE

Mungu akasema: "NAO NA WANIFANYIE PATAKATIFU; ILI NIPATE KUKAA KATI YAO." Kutoka 25:8. Hivyo ndivyo alivyoagiza Mungu kujenga jengo ambalo lingekuwa maskani Yake miongoni mwa wana wa Israeli, na hatimaye kuwa mahali pao pakuu pa ibada kwa mamia ya miaka. Sio tu Mungu aliamuru lijengwe, bali alitoa mfano (pattern) wa kufuata katika kulijenga.

Jengo hili, pamoja na hekalu lililochukua mahali pake [baadaye], lilikuwa ni jengo lililofurahia sifa ya pekee ya kuwa jengo la pekee duniani ambalo lilipata kufananishwa na jengo lililoko mbinguni.

Kwa mwonekano wake lilifanana na hema. Lilikuwa na urefu wa karibu futi hamsini na nne, na upana wa futi kumi na nane, na kimo cha futi kumi na nane. Patakatifu (the sanctuary) palikuwa ni jengo la kupendeza. Vifuniko vya paa lake vilikuwa vinne. Kuanzia [kifuniko cha] nje, kuelekea kwenye hewa, palikuwa na ngozi za pomboo. Chini yake ngozi za kondoo waume, zilizotiwa rangi nyekundu. Kisha chini yake palikuwa na pazia jeupe la singa za mbuzi. Kifuniko cha ndani, ambacho kiliweza kuonekana kwa makuhani waliohudumu humo, kilikuwa kimetengenezwa kwa "nguo ya kitani nzuri ya kusokota, pamoja na nyuzi za rangi ya samawi, na ya zambarau, na nyekundu, pamoja na makerubi, kazi ya fundi stadi." Kutoka 26:1.

Mbao zenye kusimama, za pande zote mbili na upande mmoja wa jengo lile, zilifunikwa kwa dhahabu. Mlango wa kuingilia, ambao daima ulikuwa upande wa mashariki, ulitegemezwa kwa nguzo tano zilizofunikwa kwa dhahabu, ambazo kwazo pazia lilitundikwa likiwa linaning'inia na hilo ndilo lililofanya "mlango wa Hema, wa nyuzi za rangi ya samawi, na za rangi ya zambarau, na za rangi nyekundu, na kitani nzuri yenye kusokotwa, kazi ya mshona taraza." Kutoka 26:36.

Kulizunguka hema hilo ulikuwa ni ua, futi tisini kwa futi mia moja themanini, ambao ulizuia wadadisi wasiweze kuangaza macho yao ndani ili kuliona jengo hilo, wala kuruhusu wale wasiojali kulikaribia jengo hilo kwa karibu sana. Ua huo ulitengenezwa kwa mapazia meupe ya kitani yaliyoangikwa kwenye vigingi vya shaba vyenye urefu wa futi tisa. Mlango wake, pia, ulielekea upande wa mashariki, nao ulifungwa kwa pazia lililofanana na lile la Patakatifu.

Jengo hili takatifu lenyewe liligawanywa katika vyumba viwili kwa pazia lilitundikwa kwenye vigingi vinne. Chumba cha kwanza kilitwa PATAKATIFU, na cha pili, PATAKATIFU PA PATAKATIFU. Katika chumba kile [cha kwanza] cha Patakatifu palikuwa na kinara cha taa saba, na meza pamoja na mikate yake ya "wonyesho" iliyokuwa inabadilishwa mara kwa mara. Zaidi ya [vifaa] hivyo, madhabahu ya kufukizia uvumba ilisimama mbele tu karibu na pazia la pili [la ndani]. Juu ya madhabahu hii uvumba wenye harufu nzuri, ukiwa ni mfano wa kazi ya maombezi yake Kristo inayoendelea [mbinguni] pasipo kukoma, ulifukizwa asubuhi na jioni.

Ndani ya pazia lile la ndani palikuwa ni pale Patakatifu pa Patakatifu, lilimokuwamo sanduku lenye mbao mbili za Sheria [Amri Kumi], zilizoandikwa kwa kidole cha Mungu. Kifuniko cha sanduku hilo kilikuwa ndicho kiti cha rehema cha dhahabu. Mwisho wa kila upande wake alisimama Kerubi mmoja wa dhahabu, mabawa yao yalikutana upande wa juu, na nyuso zao daima zilikitazama kiti kile cha rehema. Kilikuwa mfano wa kiti cha enzi cha Mungu ----- malaika wanaokizunguka kiti hicho, sheria ambayo ndiyo MSINGI WA SERIKALI ya Mungu, na kiti cha rehema chenye kilikuwa mfano wa kuingilia kati kwa rehema na msamaha [wa Mungu] kwa ajili ya mwenye dhambi; na juu yake utukufu unaonekana wa Bwana ulikuwapo, yaani Shekina.

## HUDUMA YA UKUHANI

Fundisho la Biblia kuhusu Patakatifu pa huduma ile ya Walawi huonyesha wazi kwamba kutakaswa kwa Patakatifu ndilo JIBU LA MUNGU KWA MAKOSA NA UASI.



Huduma ya ukuhani katika Patakatifu pa Duniani, au Hekalu, katika siku zile za Israeli, ilikuwa ni mfano wa kazi ya Kristo, Kuhani wetu Mkuu, katika Hekalu la Mbinguni. Makuhani wa duniani walihudumu kwa "MFANO WA KIVULI CHA MAMBO YA MBINGUNI." Waebrania 8:5. Na kuhusu huduma yake Kristo katika Hekalu lile la Mbinguni tunaambiwa hivi:

"Basi, katika hayo tunayosema, neno lililo kuu ndilo hili TUNAYE KUHANI MKUU NAMNA HII, ALIYEKETI MKONO WA KUUME WA KITI CHA ENZI CHA UKUU MBINGUNI, MHUDUMU WA PATAKATIFU, NA WA ILE HEMA YA KWELI, AMBAYO BWANA ALIWEKA WALA SI MWANADAMU." Waebrania 8:1,2.

Katika huduma ya hapa duniani, kutakaswa kwa Patakatifu ilikuwa ni kazi ya Kuhani Mkuu ya kufungia [mwaka]. Kwa hiyo, kutakaswa kwa Patakatifu wakati ule wa mwisho, kwa mujibu wa fundisho la hakika la mfano (type), hakuna budi kuwa ni huduma ya kufungia [kazi] ya Kuhani wetu Mkuu katika Hekalu la Mbinguni, kabla hajaiweka kando [hajaiacha] kazi Yake ya ukuhani na kuja kwetu katika utukufu wake.

Palikuwa na sehemu mbili tofauti za huduma ya ukuhani katika Hema kule Israeli. Kwanza, palikuwa na huduma ya "kila siku," ambayo ilikomea katika chumba kile cha kwanza. Na sehemu ile ya pili, ni huduma ile ya "kila mwaka," yaani, huduma ya siku ile ya UPATANISHO, ambayo Kuhani Mkuu peke yake aliruhusiwa kuingia ndani ya Patakatifu pa Patakatifu.

## HUDUMA YA KILA SIKU

Kuhusu huduma katika chumba kile cha kwanza inaelezwa hivi: "Basi vitu hivi vikiisha kutengenezwa hivyo, makuhani huingia katika Hema hiyo ya kwanza daima [kila siku], wakiyatimiza mambo ya ibada." Waebrania 9:6.

Kila siku makuhani walihudumu katika chumba cha kwanza. Kila siku walihudumia "sadaka ya dhambi ya mtu mmoja mmoja," na "sadaka ya kuteketezwa ya daima." Agizo la Mungu kwa mwenye dhambi mmoja mmoja lilikuwa kama ifuatavyo:

"Na mtu awaye yote katika watu wa nchi akifanya dhambi, pasipo kukusudia, kwa kufanya neno lo lote katika hayo ambayo BWANA alizuilia yasifanywe, naye akapata hatia; akijulishwa hiyo dhambi yake aliyoifanya, ndipo atakapoleta mbuzi mke mkamilifu, awe matoleo yake kwa ajili ya dhambi yake aliyoifanya. Naye ATAWEKA MKONO WAKE KICHWANI MWAKE HIYO SADAKA YA DHAMBI, NA KUMCHINJA SADAKA YA DHAMBI MAHALI HAPO PA SADAKA YA KUTEKETEZWA. KISHA KUHANI ATATWAA KATIKA HIYO DAMU YAKE KWA KIDOLE CHAKE, NA KUITIA KATIKA PEMBE ZA MADHABAHU YA KUTEKETEZA NA DAMU YAKE YOTE ATAIMWAGA CHINI YA MADHABAHU.... NA

KUHANI ATAFANYA UPATANISHO KWA AJILI YAKE, NAYE ATASAMEHEWA."  
Mambo ya Walawi 4:27-31.

Hapa inaonekana picha ya mpango wa Mungu wa kumwondolea dhambi zake yule mwenye dhambi. Katika nyakati za Agano la Kale kazi hiyo ilitimizwa, kwa mfano, kwa njia ya damu ile ya sadaka ya dhambi. Katika siku zile mwenye dhambi alileta sadaka yake, iliyokuwa mfano wa Kristo, penye mlango wa Patakatifu. Pale aliweka mikono yake juu ya kichwa cha mhanga [kafara] wake asiyekuwa na hatia, naye ilimpasa KUUNGAMA DHAMBI ZILE ZILE alizokuwa na hatia nazo. Hakutakiwa kusema kwa jumla tu, bali kutaja dhambi halisi [moja moja kwa jina lake]. Kwa njia ya ibada hii alizihamishia dhambi zake kwenye kichwa cha mwana kondoo yule.

Lakini hayo si yote: ilimpasa kwa mkono wake yeye mwenyewe kumchinja mwana kondoo huyo. Ndipo Kuhani alipoichukua sehemu ya damu hiyo na kuinyunyiza kwenye pembe za madhabahu ya sadaka za kuteketezwa, na damu iliyobaki aliimwaga yote chini ya madhabahu hiyo. Kwa njia ya huduma hii yenye madoido mengi dhambi za mwenye dhambi yule zilihamishwa kwa njia ya damu kutoka kwake kwenda kwenye madhabahu na hatimaye kufika Patakatifu.

Kwa njia hiyo "siku kwa siku wanyama wa kafara walichinjwa karibu na madhabahu mbele ya pazia la nje, na damu 'ililetwa ndani ya Patakatifu' na kuhani." Jambo hili lilitendeka kukiri UVUNJAJI WA SHERIA ya Mungu [Amri Kumi] na kuwa ushuhuda kwamba yule mwenye dhambi alistahili kifo. Lilikuwa ni ungamu la imani katika Mwana-Kondoo wa Mungu ambaye angekufa badala ya mwenye dhambi yule, na ambaye damu Yake ya upatanisho ingemtetea [mwenye dhambi] mbele ya Sheria ya Haki [iliyovunjwa].

Siku kwa siku, daima, makuhani walihamisha dhambi kwa mfano (type) kutoka kwa mwenye dhambi kwenda Patakatifu, na matokeo yake ni kwamba yule mwenye dhambi alipata msamaha. Tendo hilo lilifanyika aidha kwa kunyunyiza damu "mbele zake Bwana" au kwa kula sehemu ya nyama ya sadaka ile iliyoteketezwa katika [chumba cha] Patakatifu.

## SADAKA YA ASUBUHI NA JIONI

Zaidi ya ile sadaka ya dhambi ilikuwako "sadaka ya asubuhi na jioni," au "sadaka ya kuteketezwa ya daima." Mungu aliwaagiza watu kwa maneno haya yafuatayo:

"Basi sadaka utakazozitoa juu ya madhabahu ni hizi; wana-kondoo wa mwaka mmoja wawili siku baada ya siku daima. Mwana-kondoo mmoja utamchinja asubuhi; na mwana-kondoo wa pili utamchinja jioni;... Itakuwa ni sadaka ya kuteketezwa milele katika vizazi vyenu vyote mlangoni pa ile hema ya kukutania mbele ya BWANA; hapo nitakapokutana nanyi, ili ninene na wewe hapo." Kutoka 29:38,39,42.

Sadaka ya kuteketezwa ya daima zaidi sana ilikuwa ni sadaka ya taifa zima kuliko kuwa sadaka ya mtu mmoja mmoja. Ilikuwa ni mfano wa kafara ya Yesu Kristo msalabani, na mbele za Bwana ilikuwa na harufu nzuri kwa ajili ya Israeli yote. Madhabahu ya sadaka za kuteketezwa ilikuwa mfano wa msalaba, kama vile kafara juu ya madhabahu hiyo ilivyokuwa mfano wa kafara ile msalabani. Katika moshi uliopanda juu kutoka kwenye madhabahu hiyo ulionekana msaada wa kivuli [mfano] wa damu ile iliyomwagika pale msalabani.

Sadaka ya asubuhi iliendelea kuteketezwa juu ya madhabahu hiyo mpaka wakati wa sadaka ya jioni, na sadaka ya jioni iliendelea kuteketezwa mpaka asubuhi. "Hivyo daima palikuwa na sadaka madhabahuni, mchana na usiku, ishara ya UPATANISHO WA MILELE uliotolewa

katika Kristo.... 'Sadaka ya asubuhi ilikuwa kwa ajili ya upatanisho wa dhambi zilizotendwa usiku uliotangulia, sadaka ya mchana [jioni] ilikuwa kwa ajili ya dhambi zilizotendwa mchana.'" ----- M. L. Andreasen, THE BOOK OF HEBREWS, uk. 372.

Katika huduma hii kuhani mkuu alinyunyiza damu juu ya kiti cha rehema na Patakatifu; "kwa sababu ya unajisi wa wana wa Israeli." Patakatifu palisuluhishwa au kutakaswa kutokana na dhambi zote zilizokuwa zimewekwa pale kwa mfano (type) kwa njia ya damu ya sadaka iliyoletwa pale siku kwa siku katika kipindi cha mwaka ule.

Kuhani Mkuu alipotoka nje, akizichukua dhambi, alizihamisha zote kwenda juu ya kichwa cha mbuzi yule wa Azazeli, ambaye alipelekwa mbali jangwani. Kwa njia hiyo "dhambi zao zote" zilichukuliwa mbali na kambi lao kwenda jangwani, na Patakatifu pakawa pametakaswa. (Angalia Mambo ya Walawi 16.)

Huo ulikuwa ni wakati wa kutisha sana wa hukumu katika Israeli. Maisha ya kila mtu yalichunguzwa siku ile. Je, kila dhambi ilikuwa imeungamwa? Ye yote ambaye alionekana hana uhusiano mwema na Mungu, huduma ile ilipoendelea kufanywa, alikatiliwa mbali [alikufa ghafula] asiwe na sehemu yo yote na watu wake Mungu.

"Kwa kuwa ni siku ya upatanisho, ili kufanya upatanisho kwa ajili yenu mbele za BWANA, Mungu wenu. KWA KUWA MTU AWAYE YOTE ASIYEJITESA MWENYEWWE [KWA KUUNGAMA DHAMBI ZAKE KWA DHATI] SIKU IYO HIYO, ATAKATILIWA MBALI NA WATU WAKE." Mambo ya Walawi 23:28,29.

## SIKU YA UPATANISHO

Kwa mwaka mzima, isipokuwa siku moja tu, huduma ya ukuhani iliendelea katika chumba kile cha kwanza, au Patakatifu. Lakini katika siku ile ya mwisho ya huduma ya mwaka mzima -----

"siku ya kumi ya mwezi wa saba" ----- Kuhani Mkuu aliingia katika chumba kile cha pili, au Patakatifu pa Patakatifu.

Katika siku hiyo Kuhani Mkuu alitakiwa kutwaa kutoka mikononi mwa mkutano wa Waisraeli mbuzi waume wawili. "Kisha [Haruni] atawatwaa wale mbuzi wawili na kuwaweka mbele za BWANA mlangoni pa hema ya kukutania. Na Haruni atapiga kura juu ya wale mbuzi wawili; kura moja kwa ajili ya BWANA; na kura ya pili kwa ajili ya Azazeli. Na Haruni atamleta yule mbuzi aliyeangukiwa na kura kwa ajili ya BWANA, na kumtoa awe SADAKA YA DHAMBI. Bali yule mbuzi aliyeangukiwa na kura kwa ajili ya Azazeli ATAWEKWA HAI mbele za BWANA ili kumfanyia upatanisho, ili kumpeleka jangwani kwa ajili ya Azazeli [Shetani]." Mambo ya Walawi 16:7-10.

Wakati ule mwenye dhambi alipokuwa ametakaswa kwa damu ile ya sadaka ya dhambi, wakati alipowekwa huru mbali na dhambi zake na kupatanishwa na Mungu, ilikuwa bado haijafanyika hatua ya mwisho ya kuziondolea mbali dhambi zake. Zilikuwa zimehamishwa tu kutoka kwake, kwa njia ya damu ile ya mfano, kwenda Patakatifu. Siku kwa siku kwa mwaka mzima mamia na maelfu ya wenye toba walileta sadaka zao za dhambi penye mlango wa Patakatifu, na kwa njia ya damu ya mwana kondoo dhambi zao zilihamishiwa Patakatifu kutoka kwao.

Siku ile ya Upatanisho [au Hukumu] ilikuwa ni siku ya kilele ya taratibu za kafara [dhabihu] za mwaka mzima. Katika siku hiyo ondoleo la dhambi la mwisho lilifanyika, na, japokuwa,

lilifanyika kwa namna ya mfano, hata hivyo, mioyoni mwao lilileta picha, kama vile linavyoleta picha mioyoni mwetu, ya ondoleo la dhambi la mwisho siku ile ya mwisho.

"Kisha atamchinja yule mbuzi wa sadaka ya dhambi, aliye kwa ajili ya watu, na kuileta damu yake ndani ya pazia, na kwa damu hiyo atafanya vile vile kama alivyofanya kwa damu ya ng'ombe, na kuinunyiza juu ya kiti cha rehema, na mbele ya kiti cha rehema, naye ATAFANYA UPATANISHO KWA AJILI YA MAHALI PATAKATIFU, KWA SABABU YA MAMBO MACHAFU YA WANA WA ISRAELI, NA KWA SABABU YA MAKOSA YAO, NAAM, KWA AJILI YA DHAMBI ZAO ZOTE.... Wala hapatakuwa na mtu katika hema ya kukutania, wakati aingiapo ili kufanya upatanisho katika Patakatifu, hata atakapotoka nje.... Kisha atatoka na kuiendea madhabahu iliyo mbele za BWANA na kufanya upatanisho kwa ajili yake." Mafungu ya 15-18.

## KAZI YA KRISTO YA MWISHO MBINGUNI

Kwa sababu hiyo awamu ya mwisho ya huduma yake Kristo kama Kuhani wetu Mkuu katika Patakatifu pa Mungu juu, haina budi kuwa kazi ya HUKUMU. Haina budi kuhusika na

kuzichunguza kumbukumbu zile zilizoko mbinguni, sawasawa na huduma ile ya mwisho katika chumba cha pili katika hema ile ya duniani, yaani, Patakatifu palipotakaswa.

Nabii Danieli alionyeshwa badiliko hilo katika huduma ya Kuhani wetu Mkuu, yaani, kutoka chumba cha kwanza kwenda chumba cha pili katika Hekalu lile la mbinguni. Anaelezea mandhari hiyo ya ajabu kuwa ni kiti cha Mungu kilicho hai, chenye magurudumu yake yawakayo moto kwa utukufu Wake, kikiingia katika Patakatifu pa Patakatifu pale pa mbinguni, kwa madhumuni ya kumaliza kazi ya mwisho ya huduma yake Kristo:

"Nikatazama hata viti vya enzi vikawekwa, na Mmoja aliye mzee wa siku ameketi; mavazi yake yalikuwa meupe kama theluji, na nywele za kichwa chake kama safu safi; kiti chake cha enzi kilikuwa miali ya moto, na gurudumu zake moto uwakao. Mto kama moto ukatoka ukapita mbele zake; maelfu elfu wakamtumikia, na elfu kumi mara elfu kumi wakasimama mbele zake; HUKUMU IKAWEKWA NA VITABU VIKAFUNGULIWA." Danieli 7:9,10.

Fungu linalofuata linaonyesha kwamba mandhari hii inafunuliwa [hukumu hii inawekwa] wakati UASI bado unajitukuza wenyewe duniani. Walakini, katika wakati uo huo HUKUMU INAENDELEA MBINGUNI. Kumalizika kwa kazi hiyo [ya Hukumu] kutatoa jibu kamili la Mungu kwa uasi huo, na kumfanya Kristo aje mara ya pili katika utukufu Wake kuja kuukomesha kabisa utawala huo wa dhambi. Ni katika wakati huo wa kutakaswa kwa Patakatifu ----- wakati ambapo ni kwa hali halisi, sio kwa mfano, kesi iliyoandikwa Patakatifu inachunguzwa kwa mara ya mwisho mbele zake Mungu. Kazi hiyo [ya Hukumu] inapofungwa, kulingana na ule mfano [wa Patakatifu pa Duniani], ye yote ambaye hataonekana kuwa na uhusiano mzuri na Mungu [ambaye atakuwa hajaungama dhambi zake na kuziacha] atakatiliwa mbali asiwe na sehemu yo yote na watu Wake waliokombolewa.

Hapo ndipo huduma ya ukuhani ya Kristo itakapofungwa, na umilele [uzima au mauti] wa kila mtu utakuwa umefungwa [haubadiliki] kwa milele zote. Hadi wakati ule utakapofika maneno haya yaliyonenwa na Yesu yatahusika: "MWENYE KUDHULUMU NA AZIDI KUDHULUMU;... NA MWENYE HAKI NA AZIDI KUFANYA HAKI; NA MTAKATIFU NA AZIDI KUTAKASWA. TAZAMA, NAJA UPESI, NA UJIRA WANGU U PAMOJA NAMI, KUMLIPA KILA MTU KAMA KAZI [MATENDO] YAKE ILIVYO." Ufunuo 22:11,12.

Lakini kwa wakati huu Mwokozi wetu, toka mahali pake pa huduma huko juu anasema kwa wote maneno haya ya mausia na matumaini: "Yeye ASHINDAYE [DHAMBI] atavikwa hivyo MAVAZI MEUPE [HAKI YA KRISTO], wala sitalifuta kamwe jina lake katika KITABU CHA UZIMA, nami nitalikiri jina lake mbele za Baba yangu, na mbele ya malaika zake." Ufunuo 3:5.

Kipindi kile cha unabii cha miaka 2300 kilitolewa ili kuwajulisha watu lini kazi hii ya hukumu, yaani, kutakaswa kwa Patakatifu, ilianza kule mbinguni. Ni jambo la maana sana kwetu kujua lini kipindi hicho kinaanza na kumalizika.

-----W. A. Spicer, OUR DAY IN THE LIGHT OF PROPHECY, Sura ya 20, uk.165-171.

Type and Antitype (The Sanctuary).

## KWA NINI DHAMBI NA MATEO VILIRUHUSIWA?

Kwa watu wengi chanzo cha dhambi na sababu ya kuwako kwake ni chimbuko la utata mkubwa. Wanayaona matendo mabaya, pamoja na matokeo yake ya kutisha ya misiba na uharibifu, kisha wanajiuliza kwa jinsi gani [mambo] hayo yote yanaweza kuwako chini ya mamlaka ya yule Mmoja ambaye ana hekima yote, uwezo wote, na upendo wote. Hapa kuna siri ambayo maelezo yake hawayapati. Na katika hali yao ya kutokuwa na hakika na mashaka yao wanapofushwa macho wasiweze kuziona kweli zilizofunuliwa wazi katika Neno la Mungu, ambazo ni za muhimu kwa wokovu wetu. Kuna wale ambao, katika kutafuta habari zinazohusu kuwako kwa dhambi, wanajaribu kufanya utafiti wao katika kile ambacho Mungu hajakifunua; kwa hiyo hawapati suluhisho lo lote kwa matatizo yao; na [watu] kama hao wanaoongozwa na mwelekeo wao wa kuona mashaka na kubisha hulishikilia jambo hilo [la kutopata suluhisho] kama ndio udhuru wao wa kuyakataa maneno ya Maandiko Matakatifu. Walakini, wengine wanashindwa kuwa na ufahamu wa kutosha kuhusu tatizo hili kubwa la uovu, kwa sababu mapokeo na tafsiri potofu zimetia giza mafundisho ya Biblia kuhusu tabia ya Mungu ilivyo, asili [msingi] ya Serikali Yake, na kanuni zake za kuishughulikia dhambi.

Ni jambo lisiloweze kana kueleza chanzo cha dhambi kiasi cha kuweza kutoa sababu ya kuwako kwake. Lakini kiasi cha kutosheleza kwa mambo yote mawili kinaweza kufahamika kuhusu chanzo na mwisho wa dhambi pamoja na kudhihirisha kikamilifu HAKI na FADHILI za Mungu katika kushughulika kwake kote na uovu huo. Hakuna jambo linalofundishwa kwa wazi zaidi katika Maandiko kama lile la kwamba Mungu kwa vyo vyote vile HAHUSIKI NA KUIINGIA KWA DHAMBI; kwamba Mungu hakuiondoa neema yake kiholela, kwamba hapakuwa na kasoro yo yote katika Serikali ya Mungu, ambayo ingesababisha kuwapo mwanya wa kuinuka maasi hayo. Dhambi ni kitu kilichojiingiza chenyewe, ambacho kuwako kwake hakuna sababu inayoweza kutolewa. Ni kitu cha ajabu, kisichokuwa na maelezo yo yote; KUITOLEA UDHURU NI KUITETEKA. Kama udhuru ungaliweza kupatikana kwa ajili yake, ama sababu ingaliweza kutolewa kwa kuwako kwake, basi, ingekoma kuwa dhambi. Maana yetu ya dhambi ni ile tu iliyotolewa katika Neno la Mungu; [dhambi] ni "UVUNJAJI WA SHERIA," [I Yohana 3:4, AJKK], ni utendaji wa kanuni ile inayoipiga vita Sheria kuu ya upendo [Amri Kumi] ambayo ndiyo msingi wa Serikali ya Mungu.

Kabla ya dhambi kuingia kulikuwa na amani na furaha katika malimwengu yote. Vyote vilikuwa katika mwafaka mkamilifu na mapenzi ya Muumbaji. Upendo wao kwa Mungu ulikuwa umefikia kipeo chake, na upendo kwa kila mmoja ulikuwa hauna ubaguzi. Kristo, ambaye ni Neno, Mwana wa pekee wa Mungu, alikuwa UMOJA na Baba yake wa milele, ----- katika asili, tabia, na makusudi, ----- kiumbe wa pekee katika malimwengu yote aliyeweza kuingia katika mashauri na makusudi yote ya Mungu. Kwa njia ya Kristo, Baba aliumba viumbe vyote vya mbinguni. "Kwa kuwa katika Yeye vitu vyote viliumbwa, vilivyo mbinguni... ikiwa ni viti vya enzi, au usultani, au enzi, au mamlaka" (Wakolosai 1:16); na kwa Kristo, kama vile kwa Baba Yake, mbingu yote ilionyesha utii wake.

Sheria ya upendo [Amri Kumi] ikiwa ndiyo msingi wa Serikali ya Mungu, kuafikiana kabisa na kanuni zake za haki lilikuwa ndilo tegemeo la furaha ya viumbe vyote vilivyombwa. Mungu anataka huduma ya upendo kutoka kwa viumbe vyake vyote ----- ibada ile inayotokana na kuithamini kwa akili tabia yake. Hana furaha na utii wa kujilazimisha, tena huwapa wote uhuru wa kufanya wapendavyo, ili waweze kumpa huduma ya hiari.

## LUSIFA, WA KWANZA MIONGONI MWA MAKERUBI

Lakini alikuwako mmoja aliyechagua kuutumia uhuru wake vibaya. Dhambi ilianzishwa na yule ambaye, akiwa wa pili toka kwa Kristo, alikuwa amepewa heshima kubwa sana, naye alikuwa amesimama mahali pa juu sana pa uwezo na utukufu miongoni mwa wakazi wote wa mbinguni. Kabla ya anguko lake, Lusifa alikuwa ni Kerubi afunikaye wa kwanza, mtakatifu, na asiye na waa. "BWANA Mungu asema hivi; Wewe wakitia muhuri kipimo, umejaa hekima, na

ukamilifu wa uzuri. Ulikuwa ndani ya Edeni, bustani ya Mungu; kila jiwe la thamani lilikuwa kifuniko chako." "Wewe ulikuwa kerubi mwenye kutiwa mafuta afunikaye; nami nalikuweka hata ukawa juu ya mlima mtakatifu wa Mungu, umetembea huko na huko kati ya mawe ya moto.



Ulikuwa MKAMILIFU katika njia zako tangu siku ile ulipoumbwa, hata UOVU ulipoonekana NDANI yako." Ezekeieli 28:12-15.

Lusifa angaliweza kubakia katika upendeleo wa Mungu, akiwa anapendwa na kuheshimiwa na jeshi lote la malaika, akitumia uwezo wake mkuu kuwaletea furaha wengine na kumtukua Muumbaji wake. Lakini, asema nabii huyu, "Moyo wako uliinuka kwa sababu ya uzuri wako; umeiharibu hekima yako kwa sababu ya mwangaza wako." Fungu la 17. Kidogo kidogo, Lusifa akaanza kuingiwa na tamaa ya kujiinua mwenyewe. "Umeweka moyo wako kama moyo wa Mungu." "Nawe ulisema... Nitakiinua kiti changu juu kuliko nyota za Mungu; Nami nitaketi juu ya mlima wa mkutano... Nitapaa kupita vimo vya mawingu, Nitafanana na Yeye Aliye juu." Fungu la 6; Isaya 14:13,14. Badala ya yeye kumfanya Mungu aonekane kuwa ndiye Mkuu kuliko wote katika mapenzi na utiifu wa viumbe vyake, ilikuwa ni jitihada yake Lusifa kuwashawishi watote huduma yao pamoja na utii wao kwake yeye mwenyewe. Naye akiwa anatamani sana heshima ile ambayo Baba wa milele alikuwa amempa Mwanawe, mkuu huyo wa malaika akataka sana kujipatia mamlaka hayo ambayo ilikuwa ni haki ya Kristo peke yake kuyatumia.

Mbingu yote ilikuwa imefurahia kuakisi utukufu wa Muumbaji wao na kuzitangaza sifa zake. Naye Mungu alipoheshimiwa hivyo, kukawa na amani na furaha kote. Lakini sauti ya kutopatana sasa ikaharibu mwafaka wote uliokuwako mbinguni. Kuitumikia na kuiinua juu nafsi, kinyume na mpango wa Muumbaji, kukaamsha hisia za uovu mioyoni mwa wale ambao walikuwa wameupa utukufu wa Mungu kipaumbele. Mabaraza ya mbinguni yakamsihi Lusifa. Mwana wa Mungu akaonyesha mbele yake [Lusifa] ukuu, fadhili, na haki ya Muumbaji, pamoja na utakatifu na tabia ya Sheria yake isiyobadilika. Mungu Mwenyewe ndiye aliyeweka utaratibu wa mbinguni; na kule kujitenga nao, Lusifa angekuwa anamvunjia heshima Muumbaji wake, na kujiletea maangamizi mwenyewe. Lakini onyo hilo, lililotolewa kwa upendo na rehema isiyokuwa na kifani, likaamsha tu roho ya upinzani [ndani yake]. Lusifa akauachilia wivu wake juu ya Kristo kuzidi sana, naye akazidi kuwa shupavu zaidi.

Kiburi kutokana na uzuri wake kikachochea tamaa ya kutaka ukuu kuliko wote. Heshima kuu alizopewa Lusifa hazikuthaminiwa kama ni karama ya Mungu wala hazikumfanya awe na shukrani yo yote kwa Muumbaji wake. Akajitukuza kwa mwangaza wake na kujiinua, na kutaka sana kuwa sawa na Mungu. Alipendwa sana na kuheshimiwa na jeshi lote la mbinguni. Malaika walifurahia kutekeleza maagizo yake, naye alipewa hekima na utukufu zaidi ya wote. Hata hivyo, Mwana wa Mungu alikuwa ndiye Mfalme wa mbinguni aliyetambulikana, akiwa na uweza na mamlaka kama Baba yake. Katika mashauri ya Mungu, Kristo alishiriki, ambapo Lusifa hakuruhusiwa kwa sababu hiyo kuingia katika makusudi ya Mungu. "Kwa nini," akauliza malaika huyu mwenye uwezo mwingi, "Kristo awe mkuu kuliko wote? Kwa nini anaheshimiwa zaidi kuliko Lusifa?"

## KUTORIDHIKA MIONGONI MWA MALAIKA

Akiondoka mahali pake mbele za Mungu, Lusifa akatoka kwenda kueneza roho ya kutoridhika miongoni mwa malaika. Akifanya kazi yake kwa siri kubwa, na kwa kitambo kuficha kusudi lake

hasa chini ya mwonekano wa heshima kuu kwa Mungu, akajitahidi kuchochea hali ya kutoridhika juu ya sheria zilizovitawala viumbe vya mbinguni, akatangaza kwamba ziliweka vizuio visivyokuwa vya lazima. Kwa vile tabia zao zilikuwa takatifu, akasisitiza kwamba malaika wangepaswa kuyatii mapenzi ya nia zao. Akajaribu kuwavuta wapate kushirikiana naye kwa kuwaeleza kwamba Mungu alikuwa hajamtendea yeye kwa haki kwa kumpa Kristo heshima kubwa sana. Alidai kwamba kule kutaka kwake uwezo mkubwa zaidi na heshima alikuwa hana lengo la kujiinua nafsi yake, bali alikuwa anatafuta njia ya kuwapatia uhuru wakazi wote wa mbinguni, na kwamba kwa njia hii wangeweza kuifikia hali ya juu zaidi ya maisha.

## REHEMA KUU ZA MUNGU

Mungu kwa rehema zake nyingi alimvumilia Lusifa kwa muda mrefu. Hakumtelemsha cheo chake mara moja, wala hakufanya hivyo hata wakati ule [Lusifa] alipoanza kutoa madai yake ya uongo mbele ya malaika wale watiifu. Aliachwa na kubaki mbinguni kwa muda mrefu. Tena na tena alipewa msamaha kwa sharti la kutubu na kunyenyekea. Juhudi kama hizo kutoka kwake aliye na upendo wa milele na hekima isiyokuwa na kikomo zilikusudiwa kwa ajili ya kumthibitishia [Lusifa] kosa lake. Roho hii ya kutoridhika ilikuwa haijapata kujulikana kamwe mbinguni. Mwanzoni Lusifa mwenyewe hakujua alikuwa anaelekea wapi; hakuelewa kiini halisi cha hisia zake. Lakini kule kutoridhika kwake kulipothibitika kuwa hakukuwa na msingi wa wote, Lusifa akasadiki ya kwamba alikuwa amekosa, ya kwamba madai ya Mungu yalikuwa ya haki, na ya kwamba ilimpasa yeye kuyakubali kuwa ndivyo yalivyo mbele ya mbingu yote. Laiti angalifanya hivyo, angekuwa amejiokea mwenyewe pamoja na malaika wengi. Wakati huu alikuwa bado hajautupilia mbali utii wake kwa Mungu. Japo alikuwa amekiacha cheo chake kama Kerubi Afunikaye, hata hivyo kama angetaka kumrudia Mungu, akiitambua hekima ya Muumbaji wake, na kutosheka kukalia nafasi aliyopewa katika mpango mkuu wa Mungu, angekuwa amerejeshwa katika cheo chake. Lakini kiburi chake kilimzuia kunyenyekea. Akaendelea tu kuitetea njia yake, akisema kwamba hana haja yo yote ya kutubu, naye akajitoa kikamilifu kulianzisha pambano lile kuu dhidi ya Muumbaji wake.

Nguvu zake zote za akili sasa zikaelekezwa katika kufanya udanganyifu, kuwashawishi malaika wale waliokuwa chini ya uongozi wake ili wapate kushirikiana naye. Hata ukweli ule wa kwamba Kristo alikuwa amemwonya na kumshauri ulipotoshwa ili kutimiza hila zake za uhaini. Kwa [malaika] wale waliofungwa kwa upendo wao kumtegemea yeye, Shetani aliwaeleza kwamba alikuwa amehukumiwa pasipo kufuata haki, kwamba cheo chake hakikupewa heshima inayostahili, na ya kwamba uhuru wake utapunguzwa. Kutoka katika [mbinu yake ya] kuyaeleza vibaya maneno ya Kristo akaingia katika uongo na uongo wa moja kwa moja, akimshutumu Mwana wa Mungu kwamba ana hila ya kumwadhihi mbele ya wakazi wote wa mbinguni. Pia alitafuta njia ya kuleta hoja ya uongo kati yake na malaika wale watiifu. Wale wote ambao alishindwa kuwageuza na kuwaleta upande wake kabisa akawashutumu kwamba hawajali hali njema ya viumbe wote wa mbinguni. Mambo yale yale aliyokuwa anayafanya mwenyewe, lawama yake akawatupia malaika wale waliodumu kuwa waaminifu kwa Mungu. Kisha akayaendeleza mashtaka yake juu ya Mungu kwamba hana haki, akaanza kueleza kwa ubaya maneno na matendo ya Muumbaji wake. Ulikuwa

ni mpango wake kuwachanganya mawazo malaika wale kwa hoja zake za chini chini kuhusu makusudi ya Mungu. Kila jambo lililokuwa la kawaida akalifunika kwa usiri, na kwa hila yake potofu akatia mashaka juu ya semi zilizo wazi kabisa za Yehova. Cheo chake kikubwa, kilichomweka karibu sana na utawala wa Mungu, kilimpa nguvu nyingi sana kwa maneno aliyosema, na wengi wakashawishika kujiunga naye katika maasi dhidi ya mamlaka ya Mungu.

## UDANGANYIFU WA SHETANI

Katika hekima yake Mungu alimruhusu [alimwacha] Shetani kuendeleza kazi yake, mpaka hapo roho ya chuki itakapokomaa na kuzaa maasi hai. Lilikuwa ni jambo la lazima kwa mipango yake [Shetani] kukamilika, ili tabia yake halisi na mwelekeo wake upate kuonwa na wote. Lusifa, kama malaika aliyetiwa mafuta, alikuwa ametukuzwa sana; alipendwa sana na viumbe [vyote] vya mbinguni, na mvuto wake juu yao ulikuwa na nguvu. Serikali ya Mungu haikuwajumuisha tu wakazi wote wa mbinguni, bali wa malimwengu yote aliyokuwa ameyaumba; na Shetani akadhani kwamba kama angewachukua malaika wote wa mbinguni katika maasi hayo, basi, angeweza pia kuyachukua malimwengu yale mengine. Kwa hila akatoa maelezo ya msimamo wake katika suala lile, akitumia werevu na udanganyifu kutekeleza malengo yake. Uwezo wake wa kudanganya ulikuwa mkubwa sana, na kujificha katika vazi la udanganyifu alijipatia faida. Hata malaika wale waliokuwa waaminifu hawakuweza kabisa kuitambua tabia yake au kuona kazi yake ilikuwa inaelekea kuleta matokeo gani.

Shetani alikuwa amepata heshima kubwa sana, na matendo yake yote yalikuwa na usiri, hata ikawa vigumu [kwa Mungu] kuwafunulia malaika wale hali halisi ya kazi yake. Mpaka itakapofikia ukamilifu wake, dhambi isingalionekana kuwa ni kitu kibaya kama ilivyo. Mpaka wakati huo ilikuwa haina nafasi yo yote katika malimwengu ya Mungu, na viumbe wale watakatifu hawakuwa na dhana yo yote ya hali yake halisi na ubaya wake. Hawakuweza kutambua matokeo yatakayotokea kwa kitendo cha kuiweka kando Sheria ya Mungu [Amri Kumi]. Mwanzoni Shetani alikuwa ameificha kazi yake kwa maungamo ya juu juu tu kwamba alikuwa mtiifu kwa Mungu. Alidai kwamba alikuwa anatafuta njia ya kuikuza heshima ya Mungu, uthabiti wa Serikali yake, na manufaa ya wakazi wote wa mbinguni. Wakati anaendelea kuchochea hali ya kutoridhika mioyoni mwa malaika waliokuwa chini yake, kwa hila alikuwa amefanya ionekane kwamba alikuwa anatafuta kuiondoa hali hiyo ya kutoridhika. Aliposisitiza kwamba mabadiliko yafanyike katika taratibu na Sheria za Serikali ya Mungu [Amri Kumi], alikuwa na kisingizio kwamba hayo yalikuwa ya lazima ili kuhifadhi amani mbinguni.

Katika kushughulika kwake na dhambi, Mungu angeweza kutumia tu haki na kweli. Shetani angeweza kutumia kile ambacho Mungu asingeweza kutumia ----- kujipendekeza na udanganyifu. Alikuwa ametafuta njia ya kulifanya Neno la Mungu lionekane kuwa la uongo na kuelezea vibaya mpango wa Serikali Yake [Mungu] mbele ya malaika wale, akidai kwamba Mungu alikuwa hana haki kuwawekea sheria na kanuni wakazi wale wa mbinguni; kwamba katika kuwataka viumbe wake wanyenyekee na kumtii, [Mungu] alikuwa anataka kujiinua Mwenyewe. Kwa hiyo, ikawa ni lazima kudhahirisha mbele ya wakazi wote wa mbinguni, pamoja na wale wa malimwengu

mengine, kwamba Serikali ya Mungu ilikuwa ya haki, Sheria yake [Amri Kumi] ilikuwa kamilifu. Shetani alikuwa amefanya ionekane kwamba yeye alikuwa anatafuta kuendeleza manufaa ya ulimwengu mzima. Tabia halisi ya tapeli huyo [wa ufalme], makusudi yake hasa, wote walipaswa kuyajua. Hana budi kupewa muda wa kujidhihirisha mwenyewe kwa matendo yake maovu.

## TAPELI AFICHULIWA

Fitina iliyosababishwa na mwenendo wake mwenyewe kule mbinguni, Shetani akailaumu Sheria na Serikali ya Mungu [kuwa ndicho chanzo chake]. Akatangaza kwamba maovu yote yalikuwa ni matokeo ya utawala wa Mungu. Akadai kwamba lilikuwa ni lengo lake yeye kuziboresha sheria za Yehova. Kwa ajili hiyo, ilikuwa ni lazima kwamba apewe nafasi ya kuonyesha sura ya madai yake, na kuonyesha utendaji wa mabadiliko yake aliyokuwa amependekeza kufanyika katika sheria ile ya Mungu. Kazi yake mwenyewe haina budi kumhukumu. Tangu mwanzo Shetani alikuwa amedai kwamba alikuwa hajafanya maasi yo yote. Ulimwengu wote unapaswa kumwona tapeli huyo akifichuliwa.

Hata ilipoamuliwa kwamba asingeweza kuendelea tena kuishi mbinguni, Mungu mwenye hekima hakumharibu Shetani. Kwa vile ni huduma ya upendo tu inayokubaliwa na Mungu, utiifu wa viumbe vyake vyote unapaswa kutegemea juu ya kutambua haki yake na fadhili zake. Wakazi wa mbinguni na malimwengu mengine, wakiwa hawajawa tayari kuelewa tabia au matokeo ya dhambi, wakati ule wasingeweza kuona haki na rehema ya Mungu katika kumwanganamiza Shetani. Kama angefutuliwa mbali papo hapo, basi, wangukuwa wanamtumikia Mungu kwa hofu kuliko kwa upendo. Mvuto wa tapeli huyo usingeweza kufutika kabisa. Uovu hauna budi kuachwa mpaka ukomae. Kwa manufaa ya malimwengu yote kwa vizazi visivyokuwa na mwisho, Shetani hana budi kuzidhihirisha kikamilifu kanuni zake, ili shutuma zake dhidi ya Serikali ya Mungu zionekane katika nuru yake halisi kwa viumbe vyake vyote, ili haki na rehema ya Mungu na Sheria yake isiyobadilika kamwe [Amri Kumi] viwekwe mbali na hoja yo yote milele.

Maasi haya ya Shetani yalipaswa kuwa fundisho kwa malimwengu yote kwa vizazi vyote vijavyo, ni ushuhuda wa kudumu wa tabia na matokeo ya kutisha ya dhambi. Utendaji wa utawala wa Shetani, matokeo yake juu ya wanadamu na malaika, ungeonyesha matokeo yatakavyokuwa kwa kuyaweka kando mamlaka ya Mungu. Ungeshuhudia kwamba kule kuwako kwa Serikali ya Mungu na Sheria yake [Amri Kumi] kumefungamana na usitawi wa viumbe vyote alivyoviumba. Kwa njia hiyo, historia ya jaribio hilo la kutisha la maasi lingekuwa kinga ya milele kwa viumbe vyote vitakatifu vyenye akili, ili kuvizuia visipate kudanganywa [tena] kuhusu hali halisi ya uvunjaji huo [wa sheria], kuwaokoa wasitende dhambi na kupatwa na mateso ya adhabu zake.

## DHARAU KWA SHERIA YA MUUMBAJI

Mpaka mwisho kabisa wa pambano hili kule mbinguni, tapeli yule mkuu aliendelea kujihesabia haki mwenyewe. Ilipotangazwa kwamba yeye pamoja na washirika wake wote ni lazima wafukuzwe kutoka kwenye makao yale yenye raha, ndipo kiongozi huyo wa maasi alipotoa tamko lake la wazi kwa ujasiri na kuidharau Sheria ya Muumbaji [Amri Kumi]. Akarudia tena madai yake kwamba malaika hawakuwa na haja yo yote ya kutawaliwa, bali wangeachwa kufuata mapenzi yao wenyewe, ambayo daima yangewaongoza vizuri. Akazishutumu Amri za Mungu [Kumi] kuwa zilikuwa kizuizi cha uhuru wao na kutangaza kwamba lilikuwa ni kusudi lake kupata kibali cha kuifutulia mbali sheria hiyo; kwamba, wakiisha kuwekwa huru mbali na kizuio hicho, basi, majeshi yote ya mbinguni yangeingia katika hali ya juu zaidi, na ya utukufu zaidi ya maisha yao.

Kwa kauli moja, Shetani na majeshi yake wakamtupia Kristo lawama yote kwa maasi yale, wakitangaza kwamba kama wasingekaripiwa, basi, wasingeweza kamwe kufanya maasi yale. Wakawa sugu na tayari kupigana vita kwa utovu wa utii wao, bure wakatafuta kuipindua Serikali ya Mungu, lakini kwa wakati uo huo wakadai kwa makufuru ya kwamba wao wenyewe ni wahanga wasiokuwa na hatia yo yote wa mamlaka hiyo ya ukandamizaji. Mwasi Mkuu pamoja na wale wote walioshirikiana naye hatimaye wakafukuziliwa mbali kutoka mbinguni.

Roho [Pepo] yule yule aliyechochea maasi mbinguni bado anachochea maasi duniani. Shetani ameendelea kushughulika na wanadamu kwa kutumia hila yake ile ile aliyoitumia kwa malaika wale. Roho yake sasa inatawala ndani ya wana wa kuasi. Kama yeye wanatafuta kuvivunjilia mbali vizuio vya Sheria ya Mungu [Amri Kumi], tena wanawaahidia watu uhuru kwa njia ya kuzivunja amri zake [kumi]. Karipio la dhambi kwao bado linaamsha roho ile ya chuki na upinzani. Ujumbe wa Mungu wa maonyo unapoletwa kwao na kugusa dhamiri zao, Shetani anawaongoza watu hao kujihesabia haki wenyewe na kutafuta wengine wa kuwaunga mkono katika njia yao ya dhambi. Badala ya kuyarekebisha makosa yao, wanachochea chuki kali dhidi ya mkemeaji, kana kwamba yeye ndiye aliyekuwa chimbuko la pekee la tatizo lao. Tangu siku zile za Habili mwenye haki mpaka siku hizi zetu hiyo ndiyo roho iliyokwisha kuonyeshwa kwa wale wanaothubutu kuihukumu dhambi.

Kwa kuieleza vibaya tabia ya Mungu kama vile alivyofanya mbinguni, akimfanya afikiriwe kuwa ni mkali na dhalimu, Shetani alimshawishi mwanadamu kutenda dhambi. Na baada ya kufanikiwa mpaka hapo, akatangaza kwamba vizuio vya Mungu visivyokuwa vya haki ndivyo vilivyomfanya mwanadamu kuanguka dhambini, kama vile vilivyomfanya yeye mwenyewe kuangukia katika maasi.

Lakini yule Aliye wa Milele yeye mwenyewe anaitangaza tabia yake hivi: "BWANA, BWANA, Mungu mwingi wa huruma, mwenye fadhili, si mwepesi wa hasira, mwingi wa rehema na kweli; mwenye kuwaonea huruma watu elfu elfu, mwenye kusamehe uovu na makosa na dhambi; wala si mwenye kumhesabia mtu mwovu kuwa hana hatia kamwe." Kutoka 34:6,7.

Katika kitendo cha kumfukuza Shetani kutoka mbinguni, Mungu alitangaza haki yake na kutunza heshima ya kiti chake cha enzi. Lakini mwanadamu alipokosa kwa kuyakubali madanganyo ya roho [pepo] huyo aliyeasi, Mungu alitoa ushahidi wa UPENDO WAKE KWA KUMTOA MWANAWA PEKEE kufa kwa ajili ya wanadamu walioanguka [dhambini]. Katika upatanisho huu tabia ya Mungu imedhihirika. Hoja yenye nguvu ya msalaba hudhihirisha kwa ulimwengu wote

kwamba njia ya dhambi ambayo Lusifa aliichagua kwa vyo vyote vile Serikali ya Mungu isingeweza kutupiwa lawama yo yote.

Katika pambano lile kati ya Kristo na Shetani, wakati wa kazi ya Mwokozi duniani, tabia ya tapeli huyo mkuu ilifichuliwa. Hakuna kitu cho chote ambacho kingeweza kumng'oa Shetani kutoka katika upendo [waliokuwa nao kwake] malaika wale wa mbinguni pamoja na wale wa malimwengu yote matiifu kama lilivyofanya pambano lile la kikatili dhidi ya Mkombozi wa ulimwengu. Ujasiri wa madai yake yenye makufuru kwamba Kristo angemsujudu yeye, ujasiri wake uliojaa kiburi wa kumchukua mpaka juu ya kilele cha mlima mrefu mno na juu ya kinara cha hekalu, kusudi lake ovu likajidhihirisha kwa kumshurutisha ajitupe chini kutoka umbali ule unaotia kizunguzungu, uovu wake usiolala usingizi uliomwinda toka mahali hadi mahali, ukiichochea mioyo ya makuhani na watu kulikataa pendo lake, na mwishowe kupiga kelele, "Msulibishse! Msulibishse!" ----- mambo hayo yote yaliamsha mshangao mkuu na hasira ya malimwengu [yote].

Alikuwa ni Shetani aliyeuchochea ulimwengu kumkataa Kristo. Mkuu huyo wa uovu alitumia uwezo wake wote na hila kumwangamiza Yesu; kwa maana aliona kwamba rehema na upendo wa Mwokozi, huruma yake na upole, vilikuwa vinaidhihirisha tabia ya Mungu mbele ya ulimwengu huu. Shetani alipinga kila dai alilotoa Mwana wa Mungu na kuwatumia watu kama mawakala wake ili kuyajaza maisha ya Mwokozi huyu na mateso na huzuni. Udanganyifu na uongo ambao alikuwa ametafuta ili kuizuia kazi ya Yesu, chuki ile iliyoonyeshwa kwake kupitia kwa wana wale wa kuasi, mashtaka yale ya kikatili dhidi Yake [Kristo] ambaye maisha yake yalikuwa mema yasiyo na kifani, yote hayo yalitokana na roho yake [Shetani] ya kulipiza kisasi. Moto wa wivu wake na uovu pamoja na chuki yake na kisasi, ukalipuka pale Kalvari dhidi ya Mwana wa Mungu, wakati mbingu yote imeangaza macho yake kuliangalia tukio lile kwa hofu kuu na kimya.

. Kafara ile kuu ilipokwisha kutolewa, Kristo alipaa juu, akikataa kupokea ibada ya malaika mpaka hapo atakapolitua ombi hili: "Baba, hao ulionipa nataka wawe pamoja nami po pote nilipo." Yohana 17:24. Ndipo kwa upendo usioelezeka na kwa nguvu jibu likaja kutoka kwenye kiti cha enzi cha Baba: "Na wamsujudu malaika wote wa Mungu." Waebrania 1:6. Hapakuwa na waa lo lote juu ya Yesu. Kujinyenyekeza kwake kukakoma, kafara yake ikakamilika, akapewa jina lile lipitalo kila jina.

Basi hatia ya Shetani ikajitokeza bila kuwapo na udhuru wo wote. Alikuwa ameidhihirisha tabia yake halisi kama mwongo na mwuaji. Ikaonekana ya kwamba kwa roho ile ile aliyowatawala wana wa wanadamu, ambao walikuwa chini ya mamlaka yake, angekuwa ameidhihirisha endapo angekuwa ameruhusiwa kuwatawala wakazi wa mbinguni. Alikuwa amedai kwamba uvunjaji wa Sheria ya Mungu [Amri Kumi] ungeleta uhuru na utukufu; lakini ukaonekana kuleta matokeo ya utumwa na hali mbaya.

Mashtaka ya uongo ya Shetani dhidi ya tabia ya Mungu na Serikali yake yakaonekana katika nuru yake halisi. Alikuwa amemshtaki Mungu kuwa anatafuta tu kujiinua mwenyewe kwa kutaka unyenyekevu na utii kutoka kwa viumbe vyake, naye alikuwa ametangaza kwamba, wakati Muumbaji anawaamuru wengine wote kujikana nafsi, Yeye hajizoezi kujikana nafsi yake wala kujitoa mhanga. Basi ikaonekana kwamba Mtawala huyo wa ulimwengu alikuwa ametoa kafara kubwa sana ambayo ni upendo peke yake ungeweza kutoa kwa ajili ya wokovu wa wanadamu walioanguka, yaani, wenye dhambi; kwa maana "Mungu alikuwa ndani ya Kristo, akiupatanisha

ulimwengu na nafsi yake." 2 Wakorintho 5:19. Pia ilionekana kwamba, wakati Lusifa alipokuwa amefungua mlango na kuiingiza dhambi kwa tamaa yake ya kupata heshima na uwezo mkuu wa kutawala, Kristo, ili kuiharibu dhambi, alikuwa amejinyenyekeza mwenyewe na kuwa mtii hata mauti [ya msalaba].

## HOJA KWA AJILI YA MWANADAMU

Mungu alikuwa amedhihirisha chuki yake juu ya kanuni zile za uasi. Mbingu yote ikaiona haki yake ikifunuliwa kwa kumhukumu Shetani na kumkomboa mwanadamu. Lusifa alikuwa ametangaza kwamba kama Sheria ya Mungu [Amri Kumi] ilikuwa haibadiliki, basi, na adhabu yake isingeweza kuondolewa, kila mvunja sheria angepaswa kuzuiwa milele asipate upendeleo wote wa Muumbaji. Alikuwa ametoa madai yake kwamba taifa lile la wanadamu lililokuwa limetenda dhambi lilikuwa limekwenda mbali na lisingeweza kukombolewa, na kwa sababu hiyo walikuwa mateka wake halali. Walakini kifo chake Kristo kilikuwa ni hoja iliyotolewa kwa ajili ya mwanadamu ambayo isingeweza kupinduliwa. Adhabu ya Sheria ile ilimwangukia yeye aliyekuwa sawa na Mungu, na mwanadamu akawa huru kuipokea haki yake na kwa maisha yake ya toba na unyenyekevu kupata ushindi, kama vile Mwana wa Mungu alivyopata ushindi juu ya nguvu ya Shetani. Hivyo Mungu ni mwenye haki na mwenye kuwahesabia haki wote wanaomwamini Yesu.

Lakini haikuwa tu kwa ajili ya kujipatia ukombozi wa mwanadamu kwamba Kristo alikuja duniani humu kuteseka na kufa. Alikuwa ili "kuitukuza Sheria [Amri Kumi]" na "kuiadhimisha." Sio tu kwamba wakazi wa ulimwengu huu wapate kuiangalia sheria yake ipasavyo, bali ilikuwa kwa ajili ya kuonyesha kwa dunia zote za malimwengu kwamba Sheria ya Mungu HAIBADILIKI. Endapo madai yake yangeweza kuwekwa kando, basi, Mwana wa Mungu naye asingepaswa kuutoa uhai wake ili kufanya upatanisho kwa ajili ya uvunjaji wake [Sheria hiyo]. Kifo cha Yesu kinathibitisha kwamba [Sheria] haibadiliki kamwe. Na kafara ile ambayo upendo wa milele ulimsukuma Baba na Mwana kuitoa, ili wenye dhambi wapate kukombolewa, inadhihirisha kwa malimwengu yote ----- kwamba kitu cho chote pungufu kuliko mpango huo wa upatanisho kisingeweza kutosheleza ----- kwamba haki na rehema ndio msingi wa Sheria na Serikali ya Mungu.

Katika utekelezaji wa mwisho wa hukumu itaonekana kwamba hapakuwa na sababu yo yote kwa dhambi kuwako. Wakati yule Jaji wa dunia yote atakapomwuliza Shetani, "Kwa nini wewe umeniasi Mimi, na kuninyang'anya raia hao wa ufalme Wangu?" mwasisi huyu wa dhambi hataweza kutoa udhuru wote. Kila kinywa kitafumbwa, na majeshi yote ya uasi yatatekewa.

Msalaba wa Kalvari, wakati unatangaza kwamba SHERIA HAIBADILIKI, unatangaza kwa ulimwengu kwamba MSHAHARA WA DHAMBI NI MAUTI. Katika kilio cha mwisho cha Mwokozi, alicholia, akisema, "IMEKWISHA," kengele ya kifo cha Shetani iligongwa. Pambano kuu lililokuwa limeendelea sana wakati huo likaamuliwa, na hatua ya mwisho ya kuzifutilia mbali dhambi likathibitishwa. Mwana wa Mungu alipitia malango yale ya kaburi, ili "kwa njia ya mauti AMHARIBU yeye aliyekuwa na nguvu za mauti, yaani, IBILISI." Waebrania 2:14. Tamaa ya Lusifa ya kujiinua mwenyewe ilikuwa imemwongoza kusema: "Nitakiinua kiti changu juu kuliko

nyota za Mungu;... Nitafanana na Yeye Aliye juu." Mungu anatangaza hivi: "Nami ni[ta]kufanya kuwa majivu juu ya nchi,... wala HUTAKUWAPO TENA HATA MILELE." Isaya 14:13,14; Ezekieli 28:18,19. Hivyo "siku ile inakuja, inawaka kama tanuru; na watu wote wenye kiburi, nao wote watendao uovu, watakuwa makapi; na siku ile inayokuja ITAWATEKETEZA, asema BWANA wa majeshi; hata haitawaachia SHINA wala TAWI." Malaki 4:1.

Malimwengu yote yatakuwa yameshuhudia tabia na matokeo ya dhambi. Na kule kufutiliwa mbali kabisa kwa [dhambi], ambako mwanzoni kungekuwa kumewaletea hofu malaika wale na kumvunjia heshima yake Mungu, sasa kutathibitisha haki ya upendo wake na kuimarisha heshima yake mbele ya malimwengu yote ya viumbe vyake wanaofurahia kuyafanya mapenzi yake, na ambao mioyoni mwao imo Sheria yake [Amri Kumi]. Kamwe dhambi haitaonekana tena. Lasema Neno la Mungu, "Mateso hayatainuka mara ya pili." Nahumu 1:9. Sheria ya Mungu [Amri Kumi], ambayo Shetani ameishutumu kuwa ni kongwa la utumwa, itaheshimiwa kama SHERIA YA UHURU. Viumbe waliojaribiwa na kuthibitishwa hawataweza kamwe kugeuka tena na kuacha utii wao kwake yeye ambaye tabia yake imedhihirishwa kikamilifu mbele yao kuwa ni ya UPENDO wenye kina kisichopimika na hekima isiyochunguzika.

----- E.G. White, THE TRIUMPH OF GOD'S LOVE, uk.291-297.

"Why were sin and suffering permitted?"

OR, THE GREAT CONTROVERSY, Sura ya 29, uk. 492-504.

"The Origin of Evil."





## WHY WERE SIN AND SUFFERING PERMITTED? (THE TRIUMPH OF GOD'S LOVE)

Please insert the following scripts under the pictures on the pages indicated:-

### PICTURE ON PAGE 294

Tapeli mkuu alianzisha maasi yake miongoni mwa viumbe wale wa mbinguni kwa hila na kujipendekeza kwao. Njia hizo Mungu hakuweza kuzitumia wakati anashughulika na Shetani.

### PICTURE ON PAGE 296

Tabia ya uovu uliokithiri ya Shetani ilifunuliwa kikamilifu kwa malimwengu yote Yesu alipoangikwa juu ya msalaba ule wa kikatili wa Kalvari



## JE, WAFU WANAWEZA KUONGEA NASI?

Huduma ya malaika watakatifu, kama ilivyoelezwa katika Maandiko, ni ukweli wenye faraja kuu na wa thamani kwa kila mfuasi wa Kristo. Walakini fundisho la Biblia juu ya jambo hili limetiwa giza na kupotoshwa kwa njia ya makosa yanayotokana na theolojia inayopendwa sana na watu wengi. Fundisho lile lisemalo kwamba mwanadamu ana roho isiyokufa, ambalo liliazimwa kwanza kutoka kwa falsafa ya kipagani, na hatimaye wakati wa giza lile la UASI MKUU likaingizwa katika imani ya Kikristo, limechukua mahali pa ile kweli, inayofundishwa kwa wazi kabisa katika Maandiko, kwamba "WAFU HAWAJUI NENO LO LOTE." Watu wengi sana wamekuja kuamini kwamba ni roho za wale waliokufa "watumikao, wakitumwa kuwahudumu wale watakaourithi wokovu." Walakini [imani] hiyo ni kinyume na ushuhuda wa Maandiko yanayohusu kuwako kwa malaika mbinguni, na uhusiano wao na historia ya mwanadamu, kabla ya [kutokea] kifo cha mwanadamu ye yote.

Fundisho lisemalo kwamba mtu anapokufa anaendelea kuishi, hasa imani ile isemayo kwamba roho za wafu zinarudi kuja kuwatumikia walio hai, limetayarisha njia kwa dini ya siku hizi ya kuongea na mizimu (modern spiritualism). Kama wafu wanaruhusiwa kufika mbele za Mungu na mbele ya malaika watakatifu, na kupewa uwezo wa kuwa na maarifa yanayozidi yale waliyokuwa nayo kwanza, kwa nini, basi, wasirudi duniani na kugawa maarifa yao na kuwafundisha walio hai? Iwapo roho za wafu zinarukaruka juu ya [vichwa vya] rafiki zao waliomo duniani humu, kama wafundishavyo wanatheolojia hao wanaopendwa sana na watu wengi, kwa nini, basi, wasiruhusiwe kuongea nao, na kuwaonya dhidi ya maovu, ama kuwafariji katika huzuni zao? Ni kwa jinsi gani wale wanaoamini kwamba mtu akifa roho yake inaendelea kuishi wanaweza KUIKATAA nuru ile inayowajia kama nuru itokayo mbinguni ambayo inaletwa na pepo [roho] hao wenye utukufu? Hapo ndipo ipo njia inayodhaniwa kuwa ni takatifu, ambayo Shetani anaitumia kutekeleza MAKUSUDI yake. Malaika wale walioanguka ambao wanatekeleza amri zake [Shetani] wanakuja kama wajumbe wanaotoka katika ulimwengu wa roho. Wakati [wenye dini ya mizimu] wanadai kwamba wanawaleta walio hai katika mawasiliano na wafu, hapo ndipo yule mkuu wa uovu anapotumia nguvu yake ya uchawi juu ya mioyo [akili] yao [hao walio hai].

Anao uwezo wa kuleta mbele ya wanadamu mfano [kivuli] wa ndugu zao waliokufa. Mfano huo [umbile la marehemu] unakuwa kamili; mtazamo wake huwa ni ule ule waliouzoa kuuona, maneno yake, sauti yake, huigwa kabisa kwa namna ya kushangaza sana. Wengi hufarijika kwa matumaini ya kwamba ndugu zao wapendwa wanafurahia raha isiyo na kifani kule mbinguni, na

bila kushuku hatari inayowakabili, wanatega sikio lao "wakisikiliza roho [mapepo] zidanganyazo, na mafundisho ya mashetani." [I Timotheo 4:1.]

Baada ya kusadiki kwamba wafu wanarudi kweli na kuongea nao, Shetani anafanya watokee wale walioingia makaburini mwao wakiwa hawajajiweka tayari [yaani, waovu]. Hao hudai kwamba wanayo furaha mbinguni na ya kwamba wanakalia hata vyeo vya juu kule, na kwa njia hiyo uongo unaenezwa kote kwamba hakuna tofauti yo yote kati ya wenye haki na waovu. Wageni hao wasemao uongo [mapepo] wanaowatembelea [wanadamu] kutoka katika ulimwengu wa roho wakati mwingine wanatoa tahadhari na maonyo ambayo hutokea kuwa ni ya kweli. Basi, imani [ya walio hai] inapoimarishwa hivyo, wanaanza kutoa mafundisho ambayo moja kwa moja yanaihafifisha imani [ya watu hao] katika Maandiko. Huku wakijionyesha kuwa wanapenda sana kuwaona marafiki zao waliomo duniani wakiwa na hali njema ya maisha, wanapenyeza mafundisho ya uongo kwa hila ambayo ni ya hatari sana [kiroho]. Ukweli wa kwamba wanatoa baadhi ya mafundisho yaliyo ya kweli, na wakati fulani wanaweza kubashiri matukio yatakayotokea baadaye, hufanya maneno yao wanayosema yawe na mwonekano wa kutegemewa; mafundisho yao ya uongo yanapokelewa kwa upesi na watu wengi sana, na kusadikiwa kabisa [pasipo shaka lo lote], kana kwamba [maneno hayo] yalikuwa ni zile kweli takatifu sana za Biblia. Sheria ya Mungu [Amri Kumi] huwekwa kando, Roho wa neema anadharauliwa, na damu ile ya agano inahesabiwa kuwa ni kitu kilicho najisi. Roho hizo [mapepo] zinakana Uungu wa Kristo na hata zinamweka Muumbaji kuwa yuko sawa nazo. Hivyo chini ya umbo hilo jipya la kuigiza Mwasi yule Mkuu [Shetani] bado anaendelea na pambano lake dhidi ya Mungu lililoanza kule mbinguni na [sasa] ni karibu miaka elfu sita limeendelezwa duniani humu.

## MAONYESHO YA UWEZO WA MAPEPO

Wengi hujaribu kueleza sababu ya maonyesho ya uwezo wa mapepo [miujiza] kwa kusema kwamba hiyo ni hila na kiinimacho kwa upande wa yule kijumbe. Walakini, japokuwa ni kweli kwamba mara nyingi matokeo hayo ya kiinimacho [mazingaombwe] yamefanywa kwa kutumia hila na kudaiwa kuwa ni maonyesho ya kweli, pia ni kweli kwamba kumekuwako na maonyesho yaliyotendwa yanayoonyesha uwezo usiokuwa wa kibinadamu. Kule kugonga-gonga kwa ajabu ambako kulianzisha Imani hii ya Mizimu ya Kisasa (modern spiritualism) hakukutokana na udanganyifu wala hila za mwanadamu, bali ilikuwa ni kazi ya moja kwa moja ya mapepo [malaika] wale wabaya, ambao kwa njia hiyo walianzisha mojawapo ya madanganyo yaliyofanikiwa sana katika kuziangamiza roho za watu wengi. Wengi watanaswa kwa kuamini kwamba Imani hii ya Mizimu ni udanganyifu tu wa kibinadamu; hapo watakapokutana ana kwa ana na maonyesho ambayo watayafikiria kuwa si kitu kingine bali ni mwujiza, ndipo watakapodanganyika, na kushawishika kuyakubali kama ni uweza mkuu wa Mungu.

Watu hao wanapuuzia ushuhuda wa Maandiko kuhusu maajabu yanayofanywa na Shetani na vibaraka wake. Ilikuwa ni kwa msaada wa Shetani wale wachawi wa Farao waliweza kuigiza [baadhi ya] matendo ya Mungu. Paulo anashuhudia kwamba kabla ya marejeo ya Kristo kutakuwa na maonyesho [miujiza] yanayofanana na hayo yatakayofanywa kwa uwezo wa Shetani. Kuja

kwake Bwana kutatangiwa na "kutenda kwake Shetani, kwa uwezo wote, na ishara na ajabu za uongo; na katika madanganyo yote ya udhalimu." 2 Wathesalonike 2:9,10. Naye Mtume Yohana, akiwa anaeleza juu ya nguvu hiyo itendayo miujiza ambayo itajitokeza katika siku za mwisho, anasema kwa mkazo: "Naye afanya ishara kubwa, hata kufanya moto kushuka kutoka mbinguni uje juu ya nchi mbele ya wanadamu. Naye AWAKOSESHA wale wakaa juu ya nchi, kwa ISHARA zile alizopewa [alizo na uwezo kabisa wa] kuzifanya." Ufunuo 13:13,14. Huo sio udanganyifu tu unaotabiriwa hapa. Wanadamu wanadanganywa kwa miujiza ambayo MAWAKALA WA SHETANI [2 Wakorintho 11:13-15] wanao uwezo wa kuifanya, sio wanayojifanya kuifanya.

## MKUU WA GIZA

Mkuu wa giza, ambaye kwa muda mrefu sana anatomia nguvu zake za akili kufanya kazi ya kuwadanganya watu, kwa werevu anabadilisha majaribu yake kwa wanadamu wa tabaka zote na kila hali. Kwa wasomi na waungwana anawaletea Imani hii ya Mizimu katika hali yake ya kitaalam na kiungwana, naye kwa njia hiyo anafanikiwa kuwavuta wengi katika mtego wake. Hekima inayotolewa na Imani hii ya Mizimu ni ile iliyoelezwa na Mtume Yakobo, ambayo "siyo ile ishukayo kutoka mbinguni, bali ni ya dunia, ya tabia ya kibinadamu, na Shetani." Yakobo 3:15. Walakini, jambo hilo Mlaghai huyu Mkuu hulificha [kwao] anapona kuficha kutamfaa kwa makusudi yake. Yule ambaye aliweza kuonekana amevikwa mavazi ya nuru yanayovaliwa na makerubi walioko mbinguni wakati ule alipomjia Kristo katika nyika ile ya majaribu, anawajia wanadamu kwa njia ya kuvutia kabisa kama malaika wa nuru. Anaishawishi akili kwa kuleta mafundisho makuu yanayowachangamsha sana; anayafurahisha mawazo yao kwa kuwaletea mandhari [matukio] za kuifurahisha mno mioyo yao; naye anayashirikisha mapenzi ya moyoni mwao kwa usemi wake wa ufasaha akionyesha upendo na huruma. Anayachochea mawazo yao yaweze kupaa juu, akiwaongoza wanadamu kujivunia sana hekima yao kiasi cha kumdharau Yule wa Milele mioyoni mwao. Kiumbe yule mwenye nguvu nyingi ambaye aliweza KUMCHUKUA Mkombozi wa ulimwengu huu mpaka juu kwenye kilele cha mlima ule mrefu sana na kuleta mbele yake falme zote za dunia pamoja na utukufu wake, ataleta majaribu yake kwa wanadamu kwa njia ya kuzipotosha fahamu za wale wote ambao hawajalindwa na nguvu ya Mungu.

Shetani anawadanganya watu LEO kama alivyomdanganya Hawa kule Edeni kwa kuwasifu mno, kwa kuamsha tamaa ya kujipatia maarifa yaliyokatanzwa, na kwa kuamsha tamaa nyingi ya kujikweza. Ilikuwa ni kwa njia ya kuyapenda sana maovu haya hata yakasababisha anguko lake [Shetani], na kwa njia ya [maovu] hayo anakusudia kupata ufanisi wa kuwaangamiza wanadamu. "Mtakuwa kama Mungu," anasema kwa nguvu, "mkijua mema na mabaya." Mwanzo 3:5. Imani ya Mizimu inafundisha "kwamba mwanadamu ni kiumbe cha maendeleo, hata mpaka milele ataufikia Uungu." Na tena: "Kila mtu atajihukumu mwenyewe wala sio [mtu] mwingine [kumhukumu]." "Hukumu hiyo itakuwa ya haki, kwa sababu ni hukumu inayotolewa na NAFSI yenyewe... Kiti cha enzi kiko ndani yako." Mwalimu wa Imani hii ya Mizimu alisema hivi wakati "utambuzi wa kiroho" ulipoamka ndani yake: "Ndugu zangu, wote walikuwa nusu-miungu wasioanguka." Na mwingine anasisitiza hivi: "Mtu ye yote mwenye haki na aliye mkamilifu huyu ni Kristo."

Kwa hiyo, badala ya haki na ukamilifu wa Mungu wa milele, ambaye ndiye lengo kuu la ibada; badala ya haki kamilifu ya Sheria yake [Amri Kumi], ambayo ndicho kipimo cha kweli cha mafanikio ya mwanadamu, Shetani ameweka tabia ya mwanadamu mwenye dhambi na makosa kuwa ndilo lengo pekee la ibada, kanuni pekee ya hukumu, au kanuni ya tabia. Hayo ndiyo maendeleo, sio kwenda juu, bali kwenda chini.

## KWA KUTAZAMA TUNABADILIKA

Ni sheria ya maumbile kiakili na kiroho kwamba kwa kutazama tunabadilika. Akili inajirekebisha yenyewe kulingana na mambo inayoruhusiwa kuyawaza kwa muda mrefu. Inafanana na kile ambacho imezoea kukipenda na kukiheshimu. Mtu hatapanda juu zaidi ya ile kanuni yake ya usafi [wa maisha] au wema au kweli. Kama nafsi yake ndicho kipeo chake cha juu sana, basi, hataweza kupata kitu cho chote kilicho bora zaidi kuliko hiyo. Zaidi sana, daima atazidi kuzama chini zaidi na zaidi. Akiachwa hivyo peke yake, ni lazima njia yake [ya maisha] itaelekea chini tu.

Kwa yule anayetimiza tamaa zake za mwili pasipo kujizuia, mpenda anasa, na mwasherati, Imani hii ya Mizimu inaletwa kwake kwa kificho kisichokuwa cha siri sana kama kwa msomi na mwungwana; katika mifumo yake michafu sana wanapata kitu kinachoafikiana na mwelekeo wao. Shetani anajifunza kila dalili ya tabia dhaifu ya kibinadamu, anaziangalia kwa makini dhambi ambazo kila mmoja anaelekea kuzifanya, na kisha anahakikisha kwamba nafasi hazitakuwa chache za kutosheleza mwelekeo huo wa dhambi. Anawajaribu watu kwa kutokuwa na kiasi katika kile ambacho chenye ni halali, akiwafanya, kwa utovu wao wa kiasi, kudhoofisha nguvu zao za mwili, akili, na maadili. Amewaharibu na bado anaendelea kuwaharibu maelfu kwa njia ya kutimiza tamaa zao za mwili, na kwa njia hiyo kuifanya tabia yote ya mwanadamu iwe kama ya mnyama. Na katika kuikamilisha kazi yake hiyo, anatangaza, kwa njia ya mapepo, kwamba "ujuzi wa kweli unamweka mwanadamu juu ya Sheria;" kwamba "cho chote kilichopo, ni halali;" kwamba "Mungu hahukumu;" na kwamba "dhambi ZOTE zinazotendwa hazina ubaya wo wote." Watu wanaposhawishika kusadiki hivyo kwamba tamaa ndiyo sheria ya juu kuliko zote, kwamba uhuru ni ruhusa [ya kufanya watakavyo]; na ya kwamba mwanadamu anawajibika tu kwake mwenyewe, ni nani, basi, awezaye kushangaa kwamba upotovu na tabia zilizoharibika zimezagaa kila upande? Watu wengi sana kwa furaha wanayakubali mafundisho yale yanayowaacha huru kufanya sawasawa na hisia zao zinazotoka katika mioyo yao yenye dhambi. Kamba za kujizuia wameziweka katika shingo ya tamaa mbaya, nguvu zao za akili na roho zimetawaliwa na mwelekeo wa kinyama wa miili yao, na Shetani akiwa anashangilia anawaingiza katika wavu wake maelfu ya wale wanaojidai kwamba ni wafuasi wake Kristo.

Lakini hakuna haja kwa mtu ye yote kudanganyika kwa kuyasikiliza madai ya uongo ya Imani hiyo ya Mizimu. Mungu ameupa ulimwengu huu nuru ya kutosha kuwawezesha [wanadamu] kugundua mtego huo. Kama ilivyokwisha kuonyeshwa tayari, NADHARIA hiyo inayojenga msingi halisi wa Imani ya Mizimu inayapiga vita maneno yaliyo wazi kabisa ya Maandiko. Biblia inatangaza kwamba wafu hawajui neno lo lote, kwamba mawazo yao yamepotea; hawana sehemu

tena katika jambo lo lote linalofanyika chini ya jua; hawajui cho chote kuhusu furaha au majonzi ya wale waliopendwa sana nao waliopo hapa duniani.

## MAWASILIANO YALIYOPIGWA MARUFUKU

Zaidi ya hayo, Mungu kwa makusudi mazima amekataza mawasiliano yote na wale wanaojidai kuwa ni roho za waliokufa. Katika siku zile za Waebrania kulikuwa na kundi fulani la watu waliodai, kama wanavyodai wenye imani ya mizimu leo, kwamba walikuwa na mawasiliano na wafu. Walakini "mapepo" hayo kama walivyoitwa wageni wale hayakutoka katika dunia zingine, yanatangazwa na Biblia kuwa hayo ni "ROHO ZA MASHETANI." (Linganisha Hesabu 25:1-3; Zaburi 106:28; 1 Wakorintho 10:20; Ufunuo 16:14.) Kazi ya kushughulika na "wenye pepo" [wachawi] ilitangazwa kuwa ni CHUKIZO kwa Bwana, tena ilikatazwa kabisa kwa adhabu ya kifo. Mambo ya Walawi 19:31; 20:27. Neno hilo la uchawi siku hizi linadharauliwa. Madai kwamba wanadamu wanaweza kuongea na pepo wabaya yanaonekana kuwa ni hadithi za uongo za Zama zile za Giza. Lakini, Imani hii ya Mizimu [Umizimu], ambayo inawahesabu wafuasi wake kwa mamia ya maelfu, naam, kwa mamilioni, imejipenyeza na kuingia katika mazingira ya wanasayansi, imeyashambulia makanisa, nayo imepata washabiki katika vyombo vya kutunga sheria za nchi, na hata kwenye majumba ya wafalme ----- udanganyifu huu mkubwa sana, katika umbo lake la kujificha, ni kurudi tu kwa uchawi ule uliolaaniwa na kupigwa marufuku hapo zamani.

Kama pasingekuwapo na ushahidi mwingine wa tabia halisi ya Imani hii ya Mizimu, ingetoshwa kwa Mkristo kujua kwamba mapepo hayo hayatofautishi kati ya haki na dhambi, kati ya Mitume adhimu sana na watakatifu wa Kristo na watumishi wale wa Shetani wafisadi mno. Kwa kuwaonyesha watu waliokuwa waovu kupindukia kuwa wako mbinguni na kwamba wamepewa vyeo vikubwa sana huko, Shetani anaiambia dunia hii kwamba: "Si kitu kama wewe ni mwovu kiasi gani, si kitu kama unamwamini au humwamini Mungu wa Biblia. Uishi upendavyo; mbinguni ni nyumbani kwako." Kwa kweli, waalimu wale wa Imani ya Mizimu wanatangaza hivi: "Kila mmoja atendaye dhambi ni mwema machoni pake Bwana, naye anawafurahia; au, Mungu wa hukumu yuko wapi?" Malaki 2:17. Neno la Mungu lasema hivi: "Ole wao wasemao kwamba uovu ni wema, na kwamba wema ni uovu; watiao giza badala ya nuru, na nuru badala ya giza." Isaya 5:20.

Mitume, kama wanavyoigizwa na roho hizo zidanganyazo [mapepo], wanafanywa waweze kusema maneno ya kukanusha yale waliyoyaandika kwa uongozi wa Roho Mtakatifu walipokuwa hapa duniani. Wanakanusha kwamba Biblia haikutoka kwa Mungu, na kwa kufanya hivyo wanaupasua msingi wa TUMAINI LA MKRISTO na KUIZIMA NURU inayoonyesha njia ya kwenda mbinguni. Shetani anaifanya dunia isadiki kwamba Biblia ilikuwa ni hadithi za uongo tu, au kitabu kilichofaa kwa kizazi kile kichanga cha wanadamu [wa mwanzo], lakini kwa sasa kinafaa kuangaliwa kwa juu juu tu, au kutupiliwa mbali kama kitu kilichopitwa na wakati. Na mahali pa Neno la Mungu anaweka MAONYESHO [MIUJIZA] YA MAPEPO. Hapa ndipo ilipo njia iliyodhibitiwa kabisa na yeye [Shetani]; kwa njia hii anaweza kuifanya dunia isadiki cho chote atakacho. Kitabu kile KITAKACHOMHUKUMU yeye na wafuasi wake anakitupa kivulini, mahali anapotaka hasa kiwe; Mwokozi wa ulimwengu huu anamfanya aonekane kuwa sio zaidi ya



mwanadamu wa kawaida tu. Na kama vile askari wale wa Kirumi waliolilinda kaburi lile la Yesu walivyotangaza habari za uongo ambazo makuhani na wazee waliweka kinywani mwao ili kukanusha ufufuo wake [Kristo], ndivyo waumini wa maonyesho [miujiza] haya ya mapepo wanavyojaribu kufanya ionekane kwamba hakuna mwujiza wote unaoweza kuonekana katika matukio yanayohusu maisha ya Mwokozi wetu. Baada ya kutafuta kwa njia hiyo namna ya kumweka Yesu nyuma [ili watu wamsahau], wanawataka watu kuiangalia miujiza yao wakijitapa kwamba hiyo inaipita kabisa ile ya Kristo.

## IMANI YA MIZIMU YABADILISHA SURA YAKE

Ni kweli kwamba Imani ya Mizimu sasa inabadilisha sura yake, na, ikiwa imeficha baadhi ya mambo yake yasiyokubalika, inavaa VAZI LA KIKRISTO. Lakini maneno yake toka jukwaani na katika vitabu vyake kwa miaka mingi yamekuwa mbele ya Umma, na katika hayo tabia yake halisi inaonekana wazi. Mafundisho haya hayawezi kukanwa wala kufichwa.

Hata katika sura yake ya sasa, mbali na kuweza kustahili kuvumiliwa kama zamani, yamekuwa ya hatari kweli kweli, kwa sababu ni udanganyifu ulio mgumu kuutambua kwa urahisi. Hapo zamani [imani hii] ilimshutumu Kristo na Biblia, sasa INAJIDAI kuvikubali vyote viwili. Walakini Biblia inatafsiriwa kwa njia ambayo inapendeza kwa moyo ule usioongoka, ambapo KWELI ZAKE NZITO NA ZA MAANA zinafanywa kuwa ni ubatili mtupu. Upendo unaongelewa sana kuwa ndiyo tabia kuu ya Mungu, lakini unadhaliwa na kuwa hisia duni za tamaa ya mwili, bila kuweka tofauti yo yote kati ya mema na mabaya. Haki ya Mungu, kukemea dhambi kwake, matakwa ya Sheria yake takatifu [Amri Kumi], vyote hivyo wao hawavioni [wanavidharau]. Watu wanafundishwa kuiona Sheria ile ya Amri Kumi kama ni waraka uliokufa [yaani, usiokuwa na kazi]. Hadithi za uongo zinazopendeza zinayashikilia mawazo ya watu na kuwafanya waikatae Biblia kama msingi wa imani yao. Kwa kweli, Kristo anakataliwa kama zamani; lakini Shetani ameyapofusha macho ya watu hao kiasi kwamba udanganyifu huo hauwezi kutambulikana.

Kuna wachache mno ambao wanayo dhana sahihi ya udanganyifu wa nguvu hiyo ya Imani ya Mizimu na hatari ya kujiingiza chini ya mvuto wake. Wengi wanachezacheza nayo tu kwa ajili ya kutosheleza udadisi wao. Hawana imani ya kweli katika hiyo, tena wangejazwa na hofu kuu kuwazia kujisalimisha wenyewe ili watawaliwe na mapepo hao. Lakini wanaukanyaga uwanja ule uliokatazwa, na Mharabu huyo mwenye nguvu nyingi anumia uwezo wake [wa uchawi] juu yao kinyume na matakwa yao. Hebu kwa mara moja tu washawishike kuitoa mioyo yao upande wake [Shetani], atawashikilia mateka. Haiwezekani, kwa nguvu zao, kujinasua na nguvu yake ya uchawi yenye ushawishi aliyowatupia. Hakuna kitu cho chote kinachoweza kuwaokoa watu hao walionaswa, isipokuwa ni uweza wa Mungu utolewao kama jibu kwa maombi ya bidii yaliyojaa imani.

## KWA SHERIA NA USHUHUDA

Asema hivi nabii Isaya: "Na wakati watakapokuambia, Tafuta habari kwa watu wenye pepo na kwa wachawi; waliao kama ndege na kunong'ona; je! haiwapasi watu kutafuta habari kwa Mungu wao? je! waende kwa watu waliokufa kwa ajili ya watu walio hai? Na waende kwa SHERIA na USHUHUDA; ikiwa hawasemi sawasawa na neno hili, bila shaka kwa hao hapana asubuhi." Isaya 8:19,20. Endapo watu wangekuwa tayari kupokea kweli ile iliyoelezwa wazi katika Maandiko kuhusu ASILI YA MWANADAMU na HALI YA WAFU, wangeona katika madai hayo na maonyesho [miujiza] ya mizimu kutenda kwake Shetani kwa uwezo wote, na ishara na ajabu za uongo. Lakini basi, kuliko kuachana na uhuru ule unaoafikiana na moyo usioongoka, na kuzikataa dhambi wazipendazo, watu wengi sana wanafumba macho yao ili wasiione nuru hii, nao wanazidi kusonga mbele, bila kujali maonyo, wakati Shetani naye anatega mitego yake kuwazunguka, nao wanakuwa mateka wake. "Kwa sababu hawakukubali KUIPENDA ILE KWELI [KUITUMIA KATIKA MAISHA YAO], wapate kuokolewa," kwa hiyo "Mungu AWALETEA [HAIZUI] NGUVU YA UPOTEVU; wauamini UONGO." 2 Wathesalonike 2:10,11.

Wale wanaoyapinga mafundisho ya Imani ya Mizimu wanawashambulia, sio wanadamu peke yao, bali Shetani na malaika zake. Wameingia katika pambano dhidi ya falme, na mamlaka na majeshi ya pepo wabaya katika ulimwengu wa roho. Shetani hatakubali kuiachia hata inchi moja ya eneo lake isipokuwa kama amerudishwa nyuma kwa uwezo wa wajumbe wale watokao mbinguni. Watu wa Mungu wangeweza kukabiliana naye, kama alivyofanya Mwokozi, kwa kutumia neno hili: "IMEANDIKWA." Shetani naye anaweza kunukuu Maandiko kama siku zile za Kristo, naye ataweza kuyapotosha mafundisho ili kuendeleza madanganyo yake. Wale wanaotaka kusimama katika siku hizi za mwisho za hatari inawapasa wao wenyewe kuelewa ushuhuda huo wa Maandiko.

Wengi watapambana na roho za mashetani zikija kwao katika umbile la ndugu zao wapendwa [waliokufa] au marafiki zao [waliokufa] na kuwatangazia uzushi wa hatari mno. Wageni hao wataigusa mioyo yetu na kufanya miujiza ili kudumisha uongo wao. Yatupasa kuwa tayari KUWAPINGA kwa kutumia ukweli wa Biblia usemao kwamba WAFU HAWAJUI NENO LO LOTE na kwamba wale wanaokuja katika umbile hilo ni ROHO ZA MASHETANI.

Karibu sana mbele yetu inakuja "saa ya kujaribiwa iliyo tayari kuujia ulimwengu wote, kuwajaribu wakao juu ya nchi." Ufunuo 3:10. Wale ambao imani yao haijazizatiti juu ya Neno la Mungu watadanganyika na kushindwa. Shetani anafanya kazi yake kwa kutumia "madanganyo yote ya udhalimu" ili kuwatawala wana wa wanadamu, na madanganyo yake yatazidi kuongezeka daima. Lakini anaweza kufikia lengo lake tu kama watu wanajitoa wenyewe kwa hiari yao kuingia katika majaribu yake. Wale wanaotafuta kwa bidii KUIJUA KWELI na kujitahidi KUZITAKASA ROHO ZAO KWA KUTII, kwa njia hiyo, wakifanya kila linalowezezana [kwa upande wao] kujiandaa kwa pambano hilo, wataipata NGOME IMARA ndani ya Mungu wa kweli. "Kwa kuwa umelishika NENO la subira yangu, Mimi nami NITAKULINDA" (Fungu la 10), ni ahadi ya Mwokozi. Angeweza kutuma kila malaika kutoka mbinguni kuwalinda watu wake kuliko kumwacha mtu mmoja anayemtumainia kushindwa na Shetani.

Nabii Isaya anaufunua udanganyifu wa kutisha utakaowajia waovu, ukiwafanya wajihesabu kuwa wako salama kutokana na hukumu za Mungu: "TUMEFANYA AGANO NA MAUTI, TUMEPATANA NA KUZIMU; pigo lifurikalo litakapopita, halitatufikia sisi; kwa maana TUMEFANYA MANENO YA UONGO KUWA KIMBILIO LETU, TUMEJIFICHA CHINI YA MANENO YASIYO KWELI." Isaya 28:15. Katika kundi hili linaloelezwa hapa wamo wale ambao kwa kiburi chao cha kutotaka kutubu wanajifariji wenyewe kwa maneno yasemayo kwamba mwenye dhambi hataweza kuhukumiwa; kwamba wanadamu wote, haidhuru wawe waovu kiasi gani, watapandishwa kwenda mbinguni, na kuwa kama malaika wa Mungu. Lakini kwa mkazo zaidi wapo wale wanaofanya agano na mauti na mapatano na kuzimu, wanaozikataa kweli ambazo Mbingu imezitoa kuwa kinga kwa wenye haki katika siku ile ya taabu, nao wanakubali kujificha chini ya uongo [mafundisho potofu] uliotolewa na Shetani badala yake [ile kweli] ----- yaani, madanganyo ya uongo ya Imani ya Mizimu.

Jambo la kushangaza mno lisiloneneka ni UPOFU wa watu wa kizazi hiki. Maelfu wanalikataa Neno la Mungu kuwa halifai kusadikiwa na kwa ujasiri uliojaa shauku kuu wanayapokea madanganyo ya Shetani. Wenye mashaka na wenye dhihaka wanaushutumu ushupavu wa dini wa wale wanaoishindania ile imani ya manabii na mitume, nao wanajifurahisha wenyewe kwa kuyadhihaki maneno mazito ya Maandiko yamhusuyo Kristo na Mpango wake wa Wokovu, na kisasi kitakachowajia wale wanaoikataa kweli yake. Wanajifanya kana kwamba wana huruma nyingi sana kwa watu hao [wa Mungu] wenye mawazo fnyu, duni na ya ushirikina kwa kuyakubali madai ya Mungu na kuyatii matakwa ya Sheria yake [Amri Kumi]. Wanaonyesha kuwa wanayo hakika kana kwamba kweli walikuwa wamefanya agano na mauti na mapatano na kuzimu ----- kana kwamba walikuwa wamejenga kuzuizi kisichopitika, kisichoweza kupenywa kati yao na hasira ya kulipiza kisasi ya Mungu. Hakuna kinachoamsha hofu zao. Wamejitoa kikamilifu kwa yule Mjaribu, wamejifungamanisha karibu sana naye, nao wamejazwa roho yake kikamilifu, hata hawana nguvu wala mwelekeo wa kujinasua kutoka katika mtego wake.

Kwa muda mrefu Shetani amekuwa akijiandaa kwa jaribio lake la mwisho la kuudanganya ulimwengu. Msingi wa kazi yake uliwekwa kwa matumaini aliyompa Hawa katika Edeni kwamba: "HAKIKA HAMTAKUFA." "Siku mtakayokula matunda ya mti huo, mtafumbuliwa macho, nanyi MTAKUWA KAMA MUNGU, mkijua mema na mabaya." Mwanzo 3:4,5. Kidogo kidogo ametayarisha njia ya madanganyo yake ya kilele kwa kuanzisha IMANI YA MIZIMU. Bado hajafikia kipeo cha hila zake anazotaka kuzitekeleza; lakini kitafikiwa katika siku chache za mwisho zitakazobakia. Asema nabii huyu: "Nikaona roho tatu za uchafu zilizofanana na vyura... Hizo ndizo ROHO ZA MASHETANI, zifanyazo ISHARA [MIUJIZA], zitokazo na kuwaendea WAFALME WA ULIMWENGU WOTE kuwakusanya kwa vita ya siku ile kuu ya Mungu Mwenyezi." Ufunuo 16:13,14. Ulimwengu wote utakumbwa na kuingizwa katika udanganyifu huu, isipokuwa wale WATAKAOLINDWA kwa uwezo wa Mungu kwa njia ya IMANI YAO KATIKA NENO LAKE. Watu kwa upesi sana wanalazwa usingizi katika tumaini la usalama utakaowaangamiza, wataamshwa tu kwa ghadhabu ile ya Mungu [Mapigo Saba].

Asema Bwana: "Nami nitafanya hukumu kuwa ndiyo kanuni, na haki kuwa ndiyo timazi; na mvua ya mawe [Ufunuo 16:17-21] itachukulia mbali hilo kimbilio la maneno ya uongo, na maji yatapagharikisha mahali pa kujisitiri. Na agano lenu mliloagana na mauti, litabatilika, tena mapatano yenu mliyopatana na kuzimu hayatasimama; pigo lifurikalo litakapopita, ndipo ninyi mtakapokanyagwa [mtakapoangamizwa] nalo." Isaya 28:17,18.

----- E.G. White, THE TRIUMPH OF GOD'S LOVE, uk.325-331.

Can the Dead Speak to Us?

OR, THE GREAT CONTROVERSY, Sura ya 34, uk. 551-562.

Spiritualism.

CAN THE DEAD SPEAK TO US? (THE TRIUMPH OF GOD'S LOVE)

Please insert the following Scripts under the pictures on the pages indicated:

PICTURE ON PAGE 328

Wengi hawataelewa chanzo na tabia ya nguvu ile inayomfanya  
mtu alale usingizi kwa kupunga mikono mbele ya macho yake  
(Hypnotism or Mesmerism).

PICTURE ON PAGE 330

Ni akina nani hao wanaoletwa na vijumbe vya mapepo  
na kuonekana kwetu?

PICTURE ON PAGE 331

"HAKIKA HAMTAKUFA."

## IMANI MBILI TANGU EDENI

Kuna imani mbili kuu zilizoanza tangu bustani ya Edeni. Asilimia kubwa ya watu duniani huangukia katika mojawapo ya imani hizo. Moja ni ya Mungu; nyingine ni ya Shetani. Imani hii inahusiana na HALI YA WAFU.

Mungu anasema hivi: "BWANA Mungu akamtwa huyo mtu, akamweka katika bustani ya Edeni, ailime na kuitunza. BWANA Mungu akamwagiza huyo mtu, akisema, Matunda ya kila mti wa bustani waweza kula, walakini matunda ya mti wa ujuzi wa mema na mabaya usile, kwa maana siku utakapokula matunda ya mti huo UTAKUFA HAKIKA." Mwanzo 2:15-17. Kwa hiyo, mtu anapokufa anakufa hakika. Shetani akasema, "HAKIKA HAMTAKUFA." Twayapata maneno hayo katika Mwanzo 3:1-4, "Basi nyoka alikuwa mwerevu kuliko wanyama wote wa mwitu aliowafanya BWANA Mungu. Akamwambia mwanamke, Ati! hivi ndivyo alivyosema Mungu, Msile matunda ya miti yote ya bustani? Mwanamke akamwambia nyoka, Matunda ya miti ya bustanini twaweza kula; lakini matunda ya mti ulio katikati ya bustani Mungu amesema, Msiyale wala msiyaguse, msije mkafa. Nyoka akamwambia mwanamke, HAKIKA HAMTAKUFA." Inategemea wewe na mimi tunaamini nini juu ya waliokufa. Aidha uwe upande wa Mungu au upande wa Shetani. Huu ndio UONGO MKUBWA [Yohana 8:44] wa Shetani hadi leo tangu

alipomdanganya Adamu na Hawa kuwa wasingekufa. Hivyo ndivyo anavyowadanganya watu leo ya kuwa wanaokufa hawafi hakika.

Mwanadamu aliumbwa kwa udongo na kupuliziwa pumzi ya uhai. "BWANA Mungu akamfanya mtu kwa mavumbi ya ardhi, akampulizia puani PUMZI YA UHAI; mtu akawa nafsi hai." Mwanzo 2:7. Anapokufa pumzi yake hutoka na udongo [mavumbi] huurudia udongo. "Kwa jasho la uso wako utakula chakula, hata utakapoirudia ardhi, ambayo katika hiyo ulitwaliwa; kwa maana u mavumbi wewe, nawe mavumbini utarudi." Mwanzo 3:19. Pumzi ile ya uhai wakati mwingine huitwa roho. "Nayo mavumbi kuirudia nchi kama yalivyokuwa, Nayo roho kumrudia Mungu aliyeitoa." "Kwa kuwa uhai wangu ukali mzima ndani yangu, Na roho ya Mungu i katika PUA yangu." Mhubiri 12:7; Ayubu 27:3. Hiyo pumzi inayotoka haiwezi kuitwa mtu. Hali ya mtu aliyekufa imeelezwa vizuri sana katika Maandiko. "Pumzi yake hutoka, huurudia udongo wake, Siku hiyo mawazo yake yapotea." Zaburi 146:4. "Siku hiyo mawazo yake yapotea." Aliye hai ndiye anakuwa na MAWAZO. Mfu hana mawazo. Katika kitabu cha Ayubu twasoma maneno haya: "Lakini mwanadamu hufa, huifariki dunia; Naam, mwanadamu hutoa roho, naye yupo wapi? Kama vile maji kupwa katika bahari, Na mto kupunguka na kukatika; Ni vivyo mwanadamu hulala chini, asiinuke; Hata wakati wa mbingu kutokuwako tena, HAWATAAMKA, wala kuamshwa usingizini... Wanawe hufikilia heshima, wala yeye HAJUI; Kisha wao huaibishwa, lakini yeye HANA HABARI zao." Ayubu 14:10-12,21. Mtu aliyekufa amefanana na mto uliokauka. Maji yale yaliyokauka hayawezi kurudi tena. Anaweza kufanyiwa heshima na watoto wake katika mazishi, lakini yeye hana habari. Mtu aliyekufa hawezi kumwona Bwana. "Nalisema, Katika usitawi wa siku zangu nitakwenda kuingia malango ya kuzimu; Nimenyimwa mabaki ya miaka yangu. Nalisema, SITAMWONA BWANA, yeye BWANA, katika nchi ya walio hai; SITAMWONA MWANADAMU tena pamoja na hao wakaoo duniani." Isaya 38:10,11. Kwa hiyo, ni uongo mkubwa kusema kwamba waliokufa wameingia mbinguni.

Biblia inawashauri watu la kufanya kabla hawajafa. "Kwa sababu walio hai wanajua ya kwamba watakufa; lakini WAFU HAWAJUI NENO LO LOTE, wala hawana ijara tena; maana kumbukumbu lao limesahauliwa. Mapenzi yao na machukio yao, na husuda yao, IMEPOTEA yote pamoja; wala HAWANA SEHEMU TENA katika jambo lo lote li[na]lofanyika chini ya jua... Lo lote mkono wako utakalolipata kulifanya, ULIFANYE KWA NGUVU ZAKO; kwa kuwa HAKUNA KAZI, wala SHAURI, wala MAARIFA, wala HEKIMA, huko kuzimu [kaburini] uendako wewe." Mhubiri 9:5,6,10. Kile wanachoweza kufanya wakifanye kwa nguvu zao zote kwa kuwa hakuna kazi, wala mawazo, wala hekima huko kuzimu wanakokwenda. Tunapaswa kuushughulikia wokovu wetu kabla hatujafa. Sadaka au maombi yo yote hayawezi kubadilisha rekodi ya mtu. "Wa hao wanaozitumainia mali zao, Na kujisifia wingi wa utajiri wao; Hakuna mtu awezaye kumkomboa ndugu yake, wala kumpa Mungu fidia kwa ajili yake, Maana fidia ya nafsi zao ina gharama, Wala hana budi kuiacha hata milele; ili aishi sikuzote asilione kaburi. Naam, ataliona, hata wenye hekima hufa; Mpumbavu na mjinga hupotea pamoja, Na kuwaachia wengine mali zao. Makaburi ni nyumba zao hata milele, Maskani zao vizazi hata vizazi. Hao waliotaja mashamba yao kwa majina yao wenyewe. Lakini mwanadamu hadumu katika heshima, Bali amefanana na wanyama wapoteao. Hiyo ndiyo njia yao, ujinga wao, Nao walioko baada yao huyaridhia maneno yao. Kama kondoo wamewekwa kwenda kuzimu [kaburini], Na mauti itawachunga; Watu wanyofu watawamiliki asubuhi; Umbo lao litachakaa, kao lao ni kuzimu, maana atanikaribisha. Usiogope mtu atakapopata utajiri, na fahari ya nyumba yake itakapozidi. Maana atakapokufa hatachukua cho chote; Utukufu wake hautashuka ukimfuata. Ajapojibariki



nafsi yake alipokuwa hai, Na watu watakusifu ukijitendea mema, Atakwenda kwenye kizazi cha baba zake HAWATAONA NURU HATA MILELE." Zaburi 49:6-19.

Mbingu sio mbingu ya wafu. "Yeye si Mungu wa wafu, bali wa walio hai." Marko 12:27. Waliokufa hawawezi kumsifu Mungu. "Sio wafu wamsifuo BWANA, Wala wo wote washukao kwenye KIMYA [KABURINI]." Zaburi 115:17. Hawawezi kumshukuru Mungu. "Maana mautini hapana kumbukumbu lako; Katika kuzimu [kaburi] ni nani atakayekushukuru?" Zaburi 6:5. Hawana msaada wo wote. "Maana nafsi yangu imeshiba taabu, Na uhai wangu umekaribia kuzimu. Nimehesabiwa pamoja na washukao shimoni; Nimekuwa kama mtu asiye na MSAADA. Miongoni mwao waliokufa nimetupwa, Kama waliouawa walalao makaburini. Hao ambao Wewe huwakumbuki tena, Wametengwa mbali na mkono wako.... Wafu je! utawafanyia miujiza? Au waliofariki watasimama na kukuhimidi? Fadhili zako zitasimuliwa kaburini? Au uaminifu wako katika uharibifu? Miujiza yako itajulikana gizani? Au haki yako katika nchi ya usahaulifu?" Zaburi 88:3-5,10-12.

Kuna imani iliyoenea duniani juu ya KUONGEA NA WALE WALIOKUFU. Wengine wanajidai kwamba wanakuja kuomba majina yao wapewe watoto waliozaliwa. Je, mtu aliyekufa anaweza kujua nyumbani kwake? "Mwanadamu siku zake zi kama majani; Kama ua la kondeni ndivyo asitawivyo. Maana upepo hupita juu yake, kumbe haliko! Na mahali pake hapatalijua tena." Zaburi 103:15,16. Je, anaweza kurudi nyumbani kwake tena? "Kama vile wingu likomavyo na kutoweka, Ni vivyo huyo ashukaye kuzimuni [kaburini] hatazuka tena kabisa. HATARUDI tena nyumbani kwake, Wala mahali pake hapatamjua tena." Ayubu 7:9,10. Hivyo tunajua kuwa anayekuja sio yule aliyekufa, kwa sababu aliyekufa hahusiki [hana sehemu] na jambo lo lote linalofanyika chini ya jua. Angalia Mhubiri 9:5,6 [hapo juu]. Tena hajui kwake; wala hawezi kurudi kwake. Kwa hiyo, yule anayerudi si mwingine ila ni SHETANI anayekuja katika sura ya mtu yule aliyekufa kwani anao uwezo wa KUJIBADILISHA. "Maana watu kama hao ni mitume wa uongo, watendao kazi kwa hila, wanaojigeuza wawe mfano wa mitume wa Kristo. Wala SI AJABU. Maana SHETANI MWENYEWU HUJIGEUGA AWE MFANO wa malaika wa nuru. Basi si neno kubwa watumishi wake nao wakijigeuza wawe mfano wa watumishi wa haki, ambao mwisho wao utakuwa sawasawa na kazi zao." 2 Wakorintho 11:13-15. Anafanya hivyo ili kuendeleza uongo wake aliosema tangu mwanzo kwamba "HAKIKA HAMTAKUFA". "Yule Joka akatupwa, yule mkubwa, Nyoka wa zamani, aitwaye Ibilisi na Shetani, AUDANGANYAYE ULIMWENGU WOTE; akatupwa hata nchi, na malaika zake wakatupwa pamoja naye." "Ninyi ni wa baba yenu, Ibilisi, na tamaa za baba yenu ndizo mzipendazo kuzitenda. Yeye alikuwa MWUAJI tangu mwanzo; wala HAKUSIMAMA KATIKA KWELI, kwa kuwa hamna hiyo kweli ndani yake. Asemapo uongo, husema yaliyo yake mwenyewe; kwa sababu yeye ni MWONGO, na BABA WA HUO [UONGO]." Ufunuo 12:9; Yohana 8:44. Anafanya hivyo ili kuitetea hoja yake. Wako majini [mapepo] walioonekana katika sura za watu waliokufa. Hao wanapaswa kukemewa katika jina la Yesu, nao watakimbia. Tunapaswa kuuepuka uongo huo wa Shetani kwa kuzisoma Biblia zetu na kuziamini. Tunasadiki ya kuwa waliokufa wako mavumbini hadi siku ile ya ufufuo. "Waume, ndugu zangu, mniwie radhi, niseme kwa ujasiri mbele yenu habari za baba yetu mkuu, Daudi, ya kuwa alifariki akazikwa, na kaburi lake liko kwetu hata leo. Basi kwa kuwa ni nabii, akijua ya kuwa Mungu amemwapa kwa kiapo, ya kwamba katika uzao wa viuno vyake atamketisha mmoja katika kiti chake cha enzi; yeye mwenyewe akitangulia kuyaona haya, alitaja HABARI ZA KUFUFUKA KWAKE KRISTO, ya kwamba roho yake haikuachwa kuzimu, wala mwili wake haukuona uharibifu. Yesu huyo Mungu alimfufua, na sote tu mashahidi wake. Basi yeye, akiisha kupandishwa hata mkono wa kuume wa

Mungu, na kupokea kwa Baba ile ahadi ya Roho Mtakatifu, amekimwaga kitu hiki mnachokiona sasa na kukisikia. Maana DAUDI HAKUPANDA MBINGUNI...." Matendo ya Mitume 2:29-35 Soma pia Yohana 6:40; 5:28,29.

Parapanda ya Yesu itakapolia ndipo makaburi ya watakatifu yatakapopasuka na wafu watatoka. "Lakini, ndugu, hatutaki msijue habari zao waliolala mauti [waliokufa], msije mkahuzunika kama na wengine wasio na matumaini. Maana, ikiwa twaamini ya kwamba Yesu alikufa akafufuka, vivyo hivyo na hao waliolala katika Yesu, Mungu atawaleta pamoja naye. Kwa kuwa twawaambieni haya kwa neno la Bwana, kwamba sisi tulio hai, tutakaosalia hata wakati wa kuja kwake Bwana, HAKIKA HATUTAWATANGULIA [wala hawatatutangulia] wao waliokwisha kulala mauti. Kwa sababu Bwana mwenyewe atashuka kutoka mbinguni pamoja na mwaliko, na sauti ya malaika mkuu, na parapanda ya Mungu; nao waliokufa katika Kristo watafufuliwa kwanza. Kisha sisi tulio hai, tuliosalia, TUTANYAKULIWA PAMOJA NAO KATIKA MAWINGU, ili tumlaki Bwana hewani; na hivyo tutakuwa pamoja na Bwana milele. Basi, farijianeni kwa maneno hayo." 1 Wathesalonike 4:13-17(18). Ufufuo huo wa kwanza ni wa watakatifu; ufufuo wa pili [utakaotokea baada ya miaka elfu moja tangu ufufuo wa kwanza] ni ufufuo wa waovu. "Heri, na mtakatifu, ni yeye aliye na sehemu katika ufufuo wa kwanza." Ufunuo 20:6.

Biblia inatuonya tusinyoe nywele kwa ajili ya mtu aliyekufa. "Ninyi mmekuwa wana wa BWANA, Mungu wenu; msijitoje miili yenu, wala msifanye upaa katikati ya macho yenu kwa ajili ya aliyekufa." Kumbukumbu la Torati 14:1. Pia asionekane atokaye na kwenda kuwaomba waliokufa. "Asionekane kwako mtu ampitishaye mwanawe au binti yake kati ya moto, wala asionekane mtu atazamaye bao, wala mtu atazamaye nyakati mbaya, wala mwenye kubashiri, wala msihiri, wala mtu alogaye kwa kupiga mafundo, wala mtu apandishaye pepo, wala mchawi, WALA MTU AWAOMBAYE WAFU." Kumbukumbu la Torati 18:10,11. Hatupaswi kwenda kutambika au kuwauliza wafu kwa ajili ya walio hai. "Na wakati watakapokuambia, Tafuta habari kwa watu wenye pepo na kwa wachawi; waliao kama ndege na kunong'ona; je! haiwapasi watu kutafuta habari kwa Mungu wao? je! waende kwa watu waliokufa kwa ajili ya watu walio hai." Isaya 8:19. Hebu turudi na kuamini kauli ya Mungu kuwa WANAOKUFA WANAKUFA HAKIKA. Tusiharibu fedha zetu nyingi kushughulikia waliokufa. Mwisho tusije tukakosana na Mungu na kupoteza uzima wa milele.

----- Somo hili limetayarishwa na Mchungaji Meshack Nyagori.



## MAKABURI YALIYOKO MAJINI

Watu wengi wanayafahamu mazishi yanayofanyika katika nchi kavu. Makaburi hayo huchimbwa, na mwili wa marehemu huzikwa usionekane tena. Mungu ameweka makaburi tayari majini kwa ajili ya mazishi ya marehemu watakaokuwa wanatembea, yaani, watakaokuwa hai.

Kitabu cha Warumi kina maelezo juu ya mazishi hayo ya watu wanaotembea. "Tuseme nini basi? Tudumu katika dhambi ili neema izidi kuwa nyingi? Hasha! Sisi tulioifia dhambi tutaishije tena katika dhambi? Hamfahamu ya kuwa sisi sote tuliobatizwa katika Kristo Yesu tulibatizwa katika mauti yake? Basi TULIZIKWA pamoja naye kwa njia ya UBATIZO katika mauti yake, kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima." Warumi 6:1-4. Tulizikwa naye kwa njia ya ubatizo, na kufufuka pamoja naye kwa njia iyo hiyo ya Ubatizo. Kwa hiyo, UBATIZO maana yake ni KUFA, KUZIKWA, na KUFUFUKA pamoja na Kristo.

Ubatizo wa Biblia uko mmoja tu. "Bwana mmoja, imani moja, UBATIZO mmoja." Waefeso 4:5. Siku hizi kuna ubatizo wa aina nyingi.

Kabla ya kubatizwa kuna hatua tatu za kupitia. Hatua ya kwanza ni kufundishwa. "Basi, enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu; na KUWAFUNDISHA kuyashika yote niliyowaamuru ninyi; na tazama, mimi nipo pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari." Mathayo 28:19,20. Hatua ya pili ni kuyaamini

yale uliyofundishwa. "Akawaambia, Enendeni ulimwenguni mwote, mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe [kila mtu]. AAMINIYE na kubatizwa ataokoka; asiyeamini, atahukumiwa." Marko 16:15,16. Hatua ya tatu ni KUTUBU dhambi zako. "Petro akawaambia, TUBUNI mkabatizwe kila mmoja kwa jina lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu." Matendo ya Mitume 2:38.

Kwa sababu hiyo mtoto mdogo hawezi kubatizwa kwani hawezi kufaulu kuzipitia hatua hizo tatu. Watoto wadogo walipelekwa kwa makuhani KUBARIKIWA kama alivyofanyiwa Yesu alipokuwa mtoto mdogo, na kama Yesu mwenyewe alivyofanya kwa watoto wadogo. "Basi wakamletea watoto wadogo ili awaguse; wanafunzi wake wakawakemea. Ila Yesu alipoona alichukizwa sana, akawaambia, Waacheni watoto wadogo waje kwangu, msiwazuie; kwa maana watoto kama hawa ufalme wa Mungu ni wao. Amini, nawaambieni, Ye yote asiyeukubali ufalme wa Mungu kama mtoto mdogo hatauingia kabisa. Akawakumbatia, AKAWEKA MIKONO YAKE JUU YAO, AKAWABARIKIA." Marko 10:13-16.

Hata hivyo, ubatizo wa Biblia tangu zamani unahitaji MAJI MENGI ili mwili wote uzame. "Yohana naye alikuwa akibatiza huko Ainoni, karibu na Salimu, kwa sababu huko KULIKUWA NA MAJI TELE; na watu wakamwendea, wakabatizwa." Yohana 3:23. "Wakamwendea nchi yote ya Uyahudi, nao wa Yerusalemu wote, wakabatizwa katika mto wa YORDANI, wakiziungama dhambi zao.... Ikawa siku zile, Yesu alikuja kutoka Nazareti ya Galilaya, akabatizwa na Yohana katika YORDANI." Mathayo 1:5,9. "Filipo akasema, Ukiamini kwa moyo wako wote, inawezekana. Akajibu, akanena, Naamini ya kwamba Yesu Kristo ndiye Mwana wa Mungu. Akaamuru lile gari lisimame; wakatelemka wote wawili MAJINI, Filipo na yule towashi; naye akambatiza. Kisha walipopanda kutoka majini, Roho wa Bwana akamnyakuwa Filipo, yule towashi asimwone tena; basi alikwenda zake akifurahi." Matendo ya Mitume 8:37-39. Angalia pia Agano Jipya Kiswahili cha Kisasa [tafsiri ya Wakatoliki na Waprotestanti] maelezo yaliyo chini ya Sura ya 6 ya Warumi. Angalia pia MISALE YA WAUMINI, uk.910, Toleo la 1984.

Yesu anasema kwamba yule ambaye hatabatizwa kwa maji na kwa Roho hawezi kuingia mbinguni. "Yesu akajibu, Amin, amin, nakuambia, Mtu asipozaliwa kwa maji na kwa Roho, hawezi kuingia ufalme wa Mungu. Kilichozaliwa kwa mwili ni mwili; na kilichozaliwa kwa Roho ni roho." Yohana 3:5,6. Ubatizo ni bure; hakuna gharama utakayolipa kwa kubatizwa. "Na katika kuenenda kwenu, hubirini, mkisema, Ufalme wa mbinguni umekaribia. Pozeni wagonjwa, fufueni wafu, takaseni wenye ukoma, toeni pepo; MMEPATA BURE, TOENI BURE." Mathayo 10:7,8. Ubatizo mwingine uko nje ya Biblia [sio ule uliotajwa katika Biblia]. Kama wewe bado hujabatizwa ubatizo wa Biblia [wa kuzamishwa mwili wote majini], basi, jitoe sasa ili upate kubatizwa baada ya kupata mafundisho ya pekee yatokayo ndani ya Maandiko.

----- Somo hili limetayarishwa na Mchungaji Meshack Nyagori.



## KWA NINI SHETANI ALIFUKUZWA MBINGUNI?

Watu wengi hawaelewi kwa nini Shetani alifukuzwa mbinguni. Hili ni jambo la muhimu sana kulijua. Kwa maana tukifahamu kwa nini alifukuzwa itatusaidia kuelewa mikakati yake aliyo nayo ya kutaka kuwafanya wanadamu wote wasifae kwenda mbinguni.

Habari za Shetani zimeelezwa vizuri katika Ezekieli 28:13-19: "Ulikuwa ndani ya Edeni, bustani ya Mungu; kila jive la thamani lilikuwa kifuniko chako, akiki, na yakuti manjano, na almasi, na zabarajadi, na shohamu, na yaspi, na yakuti samawi, na zumaridi, na baharamani, na dhahabu; kazi ya matari yako na filimbi zako ilikuwa ndani yako; katika siku ya KUUMBWA kwako zilitengenezwa tayari. Wewe ulikuwa KERUBI mwenye kutiwa mafuta AFUNIKAYE; nami nalikuweka hata ukawa juu ya mlima mtakatifu wa Mungu, umetembea huko na huko kati ya mawe ya moto. Ulikuwa MKAMILIFU katika njia zako tangu siku ile ulipoumbwa, hata UOVU [DHAMBI] ulipoonekana ndani yako. Kwa wingi wa uchuuzi wako watu walikujaza udhalimu ndani yako, nawe UMETENDA DHAMBI; kwa sababu hiyo nimekutoa KWA NGUVU katika mlima wa Mungu [Ufunuo 12:7-9].... Moyo wako ULIINUKA kwa sababu ya UZURI wako; umeiharibu hekima yako kwa sababu ya MWANGAZA wako; nimekutupa chini...." [Isaya 14:12-15]. Hapa Biblia inasema UOVU [DHAMBI] ulionekana ndani yake.

Dhambi ni nini? Je, iliumbwa na Mungu? Biblia inatoa jibu la hakika kuwa dhambi ni uasi dhidi ya Sheria ya Mungu, yaani, Amri Kumi. "Kila atendaye dhambi, afanya uasi; kwa kuwa DHAMBI NI UASI [UVUNJAJI SHERIA, AJKK au AMRI KUMI]. Nanyi mnajua ya kuwa Yeye [Kristo] alidhihirishwa, ili aziondoe dhambi; na dhambi haimo ndani yake. Kila akaaye ndani yake hatendi dhambi [havunji Amri Kumi]; kila atendaye dhambi [avunjaye amri Kumi] hakumwona Yeye, wala hakumtambua. Watoto wadogo, mtu na asiwadanganye [kuwa Amri Kumi zilisulibiwa msalabani au zimekuwa kuuu]; atendaye haki yuna haki, kama yeye alivyo na haki; atendaye dhambi [avunjaye Amri Kumi] ni wa Ibilisi; kwa kuwa Ibilisi hutenda dhambi [huvunja Amri Kumi] tangu mwanzo. Kwa kusudi hili Mwana wa Mungu alidhihirishwa, ili azivunje kazi za Ibilisi. Kila mtu aliyezaliwa na Mungu hatendi dhambi [havunji Amri Kumi], kwa sababu uzao wake wakaa ndani yake; wala hawezi kutenda dhambi [kuvunja Amri Kumi kwa makusudi] kwa sababu amezaliwa

kutokana na Mungu. Katika hili watoto wa Mungu ni dhahiri, na watoto wa Ibilisi nao. Mtu ye yote asiyetenda haki hatokani na Mungu, wala yeye asiyempenda ndugu yake" (1 Yohana 3:4-10). Dhambi ilianza kwa Shetani; sio kwa Mungu.

Lakini dhambi haiwezi kuhesabiwa pasipokuwapo Sheria [Amri Kumi]. "Maana PASIPOKUWAPO SHERIA [AMRI KUMI], HAPANA KOSA [DHAMBI]." "DHAMBI haihesabiwi ISIPOKUWAPO SHERIA [AMRI KUMI]." Warumi 4:15; 5:13. Kwa hiyo, kama Shetani alifanya dhambi, basi, ni wazi kwamba ALIVUNJA SHERIA [AMRI KUMI]. Na hivyo inamaanisha ya kwamba KUNA SHERIA [AMRI KUMI] mbinguni. Sheria hiyo [ya Amri Kumi] inaitwa SHERIA YA UHURU [wala sio kongwa kama Wakristo wengi wanavyodhani]. Katika Yakobo 2:10-12 twasoma maneno haya: "Maana mtu awaye yote atakayeishika sheria yote [Amri zote Kumi], ila akajikwaa katika neno [amri] moja, AMEKOSA JUU YA YOTE [yaani, Amezivunja Amri zote Kumi]. Kwa maana Yeye aliyesema, USIZINI, pia alisema, USIUE. Basi japokuwa hukuzini, lakini umeua, umekuwa MVUNJA SHERIA [MWENYE DHAMBI]. [Endelea kulinganisha amri mbili mbili katika zile kumi kama hivi: Yeye aliyesema, USIWE NA MIUNGU MINGINE ILA MIMI, pia alisema, IKUMBUKE SIKU YA SABATO, UITAKASE..., na kadhalika mpaka ziishe zote ----- Angalia Kutoka 20:3-17]. SEMENI ninyi na KUTENDA kama watu watakaohukumiwa [hukumu itakayoamua umilele wako na wangu imejengwa juu ya Amri hizo Kumi, basi!] kwa SHERIA YA UHURU."

Shetani aliasi [alivunja] amri mbili kati ya zile kumi. "Ninyi ni wa baba yenu, Ibilisi, na tamaa za baba yenu [kuvunja Amri Kumi za Mungu] ndizo mpendazo kuzitenda. Yeye alikuwa MWUAJI [Kutoka 20:13] tangu mwanzo; wala hakusimama katika kweli [Zaburi 119:142; Yohana 17:17], kwa kuwa hamna hiyo kweli ndani yake. ASEMAPO UONGO [Kutoka 20:16], husema yaliyo yake mwenyewe; kwa sababu yeye ni mwongo, na baba wa huo." Yohana 8:44. Kuchukia ni kuuu. "Kila AMCHUKIAYE ndugu yake ni MWUAJI nanyi mnajua ya kuwa kila mwuaji hana uzima wa milele ukikaa ndani yake." 1 Yohana 3:15. Shetani alipomchukia Yesu aliua. Lakini tunajuaje kwamba Sheria hii [ya Amri Kumi] ilikuwako na bado iko kule mbinguni? Paulo katika Waebrania 9:23 anazungumzia juu ya mambo yaliyokuwa yanafanyika [katika Hekalu la] duniani kuwa yalikuwa NAKALA ya mambo yaliyoko [katika Hekalu lile la] mbinguni. "Basi ilikuwa sharti NAKALA ZA MAMBO YALIYO MBINGUNI zisafishwe kwa hizo, lakini MAMBO YA MBINGUNI YENYEWE [ASILIA (ORIGINAL)] yasafishwe kwa dhabihu zilizo bora kuliko hizo [yaani, kwa damu ya Yesu]."

Wakati Musa alipochukuliwa mlimani ALIONYESHWA baadhi ya mambo yaliyoko mbinguni. "Nao na wanifanyie PATAKATIFU [HEMA/HEKALU]; ili nipate kukaa kati yao. SAWASAWA NA HAYA YOTE NIKUONYESHAYO, MFANO WA [NAKALA YA]MASKANI, NA MFANO WA [NAKALA YA]VYOMBO VYAKE VYOTE, ndivyo mtakavyovifanya. Nao na wafanye SANDUKU... Kisha TIA NDANI YA SANDUKU HUO USHUHUDA [AMRI KUMI ----- Kumbukumbu la Torati 10:1-5] nitakaokupa... Nawe angalia ya kwamba uvifanye kama mfano wake [nakala yake], uliyoonyeshwa mlimani." Kutoka 25:8,9,16,40. Musa alionyeshwa HEMA [HEKALU] lililoko mbinguni, akatengeneza kama alivyoona. Angalia Ufunuo 15:5: "Na baada ya hayo nikaona, na HEKALU la hema ya USHUHUDA [AMRI KUMI] mbinguni lilifunguliwa." Katika Hema hiyo [ya duniani] kulikuwa na SANDUKU, na ndani ya sanduku hilo ziliwekwa mbao mbili za Amri Kumi [mfano au nakala ya zile za asilia zilizoko katika Hekalu au Hema ya mbinguni]. "Hapo BWANA alipokuwa amekwisha zungumza na Musa katika mlima wa Sinai,



akampa hizo MBAO MBILI ZA USHUHUDA [AMRI KUMI], mbao mbili za mawe, zilizoandikwa kwa chanda [kidole] cha Mungu." Kutoka 31:18. Baadaye mbao hizo ziliitwa MBAO ZA AGANO. "BWANA akanipa zile mbao mbili za mawe zimeandikwa kwa kidole cha Mungu.... Ikawa mwisho wa siku arobaini usiku na mchana, BWANA alinipa zile mbao mbili za mawe, nazo ni MBAO ZA AGANO." Kumbukumbu la Torati 9:10,11. Katika sanduku hilo siku zote ziliwekwa mbao mbili [za Amri Kumi]. Angalia 1 Wafalme 8:1,6,9. "Ndipo Sulemani alipowakusanya wazee wa Israeli, na wakuu wote wa kabila... ili walipandishe SANDUKU LA AGANO LA BWANA kutoka mji wa Daudi, yaani, Sayuni.... Makuhani wakalileta Sanduku la Agano la BWANA hata mahali pake, katika chumba cha ndani cha ile nyumba [Hekalu], PATAKATIFU PA PATAKATIFU, naam, chini ya mbawa za Makerubi.... Hamkuwa na kitu ndani ya sanduku ila zile mbao mbili za mawe ambazo Musa aliziweka ndani huko Horebu, BWANA alipofanya agano na wana wa Israeli, hapo walipotoka katika nchi ya Misri." Soma pia maelezo ya ziada katika Kutoka 40:17-21.

Baada ya miaka mingi kupita Mtume Yohana alikuja kuonyeshwa Hema ile ya mbinguni (Hekalu), akaliona SANDUKU LA AGANO ndani yake. "Kisha Hekalu la Mungu lililoko mbinguni likafunguliwa, na SANDUKU LA AGANO lake [AMRI KUMI] likaonekana ndani ya Hekalu lake..." Ufunuo 11:19. Ndani ya Sanduku la agano kulikuwa na AMRI KUMI [ASILIA (ORIGINAL)]. Mungu anawakataa wazikosao Amri Zake [Kumi]. "Umewakataa wote WAZIKOSAO AMRI ZAKO [KUMI], kwa maana hila zao ni uongo." Zaburi 119:118. Shetani alikataliwa.

Yesu aliyebaki mbinguni ni mfano mzuri kwetu wa kutii Amri [Kumi] za Mungu. "Kama vile Baba alivyonienda mimi, nami nilivyowapenda ninyi, kaeni katika pendo langu. Mkizishika amri zangu [kumi], mtakaa katika pendo langu; kama vile mimi nilivyoizishika AMRI [KUMI] ZA BABA YANGU na kukaa katika pendo lake." Yohana 15:9,10. Yesu ametuambia kwamba AMRI ZA MUNGU HAZIBADILIKI. "MSIDHANI ya kuwa nalikuja kuitangua torati au manabii; la, SIKUJA KUTANGUA, BALI KUTIMILIZA. Kwa maana, amin, nawaambia, MPAKA MBINGU NA NCHI ZITAKAPOONDOKA, yodi [ , ] moja wala nukta [ . ] moja HAITAONDOKA, hata yote yatimie. Basi mtu ye yote ATAKAYEVUNJA AMRI MOJA katika hizi zilizo ndogo, na KUWAFUNDISHA watu hivyo [kuwa haina maana yo yote kwa Mkristo, kwa mfano, Amri ile ya Nne inayohusu Sabato], ataitwa MDOGO KABISA [HATAINGIA ----- Ufunuo 21:27] katika ufalme wa mbinguni; bali mtu ATAKAYEZITENDA NA KUZIFUNDISHA [AMRI HIZO KUMI], huyo ataitwa MKUBWA katika ufalme wa mbinguni." Mathayo 5:17-19. Biblia imeandika wazi kwamba UKIVUNJA [AMRI] MOJA UMEVUNJA ZOTE [KUMI]. Soma Yakobo 2:10-12 [imenukuliwa juu]. Kwa hiyo, tunahitaji kujifunza Amri za Mungu kama Mungu mwenyewe alivyoziandika katika Kutoka 20:3-17 ili tusije tukakosea kama Shetani alivyozivunja akafukuzwa.

Yako mafungu mengi yanayotukumbusha sisi kuwa watiifu kwa Amri Kumi za Mungu. Baadhi ya mafungu hayo nitayanukuu hapa. "WOKOVU u mbali na WASIO HAKI, Kwa maana HAWAJIFUNZI AMRI ZAKO." "WANA AMANI nyingi WAIPENDAO SHERIA YAKO, wala hawana la kuwakwaza." "Yeye aligeuzaye sikio lake ASIISIKIE SHERIA, hata SALA yake ni CHUKIZO." "Hapa ndipo penye subira ya WATAKATIFU, hao WAZISHIKAO AMRI [KUMI] ZA MUNGU na IMANI ya Yesu." "Katika hili twajua kwamba twawapenda watoto wa Mungu, TUMPENDAPO Mungu [haitoshi kumpenda jirani yetu tu], na kushika Amri zake [Kumi]. Kwa maana huku ndiko kumpenda Mungu, kwamba tuzishike Amri zake; wala AMRI ZAKE [KUMI]

SI NZITO. "Naye azishikaye Amri zake [kumi] hukaa ndani yake yeye naye ndani yake. Na katika hili tunajua ya kuwa anakaa ndani yetu, kwa huyo Roho aliyetupa." "Na katika hili twajua ya kuwa tumemjua Yeye, ikiwa TUNASHIKA AMRI ZAKE [KUMI]. Yeye asemaye, Nimemjua, wala HAZISHIKI Amri zake [Kumi] ni MWONGO, wala kweli haimo ndani yake." Zaburi 119:155; Zaburi 119:165; Mithali 28:9; Ufunuo 14:12; I Yohana 5:2,3; I Yohana 3:24; I Yohana 2:3,4.

Vita kuu kati ya Shetani na watu wa Mungu [sio juu ya kumwamini Yesu, bali] ni juu ya UTII kwa Amri Kumi za Mungu. Shetani anataka kuwafanya watu wote duniani WAZIVUNJE hizo Amri Kumi za Mungu ili wasiweze kufaa kuchukuliwa mbinguni hapo Yesu atakapokuja mara ya pili. Tafadhali zingatia tabia ya Wakristo wa siku hizi za mwisho ambao Shetani amewakasirikia sana, tena anakwenda kufanya vita juu yao. Shetani hana shida na Wakristo wale wasiokuwa na tabia hiyo ya kuzishika Amri Kumi za Mungu maana hao tayari wako mkononi mwake. Hapigani nao hata kidogo asije akawaamsha katika usingizi wao wa kujidanganya wenyewe. Twasoma maneno haya kutoka katika kitabu cha Ufunuo 12:17: "Joka [Shetani] AKAMKASIRIKIA mwanamke [Kanisa], akaenda zake afanye vita juu ya WAZAO WAKE WALIOSALIA [waumini wake wa siku za mwisho], WAZISHIKAO AMRI [KUMI] ZA MUNGU, na kuwa na USHUHUDA WA YESU (ROHO YA UNABII ----- Ufunuo 19:10). Kanisa la Mungu la siku za mwisho, kama lile la mwanzo la Mitume, litashika Amri Kumi za Mungu na kuwa na karama ya Unabii katikati yake. Kwa hiyo tunapaswa kujifunza Amri za Mungu ili tupate kukubaliwa kurudi mahali pale alipofukuzwa Shetani, yaani, mbinguni kwenye raha ya milele.

----- Somo hili limetayarishwa na Mchungaji Meshack Nyagori.



## VITA YA SHETANI DHIDI YA AMRI KUMI ZA MUNGU

Shetani alipomchukia Mungu alimchukia pamoja na amri zake. Aliposhuka hapa chini, alimfanya mwanadamu pia amchukie Mungu na amri zake. "Kwa maana watu hawa ni watu WAASI, watoto wasemao uongo, watoto wasiotaka kuisikia SHERIA ya BWANA [Amri Kumi]; wawaambiao waonaji, MSIONE; na manabii, MSITOE UNABII WA MAMBO YA HAKI, tuambieni MANENO LAINI, hubirini MANENO YADANGANYAYO; tokeni katika njia, geukeni mtoke katika mapito; mkomesheni mtakatifu wa Israeli mbele yetu." "Wao WAIACHAO SHERIA [Amri Kumi] huwasifu WAOVU; Bali wao waishikao hushindana nao." Isaya 30:9-11; Mithali 28:4. Akawafanya mataifa waishi bila sheria. "Malango yake yamezama katika nchi; Ameyaharibu makomeo yake na kuyavunja; Mfalme wake na wakuu wake wanakaa kati ya mataifa WASIO NA SHERIA [Amri Kumi]; Naam, manabii wake hawapati maono yatokayo kwa BWANA." Maombolezo 2:9. Aliwafanya wanadamu wawe hivyo kwa sababu anajua ya kwamba siku moja watapita hukumuni katika Mahakama ile ya mbinguni. "Kwa maana ameweka siku ATAKAYOWAHUKUMU walimwengu kwa haki, kwa mtu yule aliyemchagua; naye amewapa watu wote uthabiti wa mambo haya kwa kumfufua katika wafu." Matendo ya Mitume 17:31.

Mungu atatumia AMRI ZAKE KUMI kuuhukumu ulimwengu huu. "Hii ndiyo jumla ya maneno; yote yamekwisha sikiwa; Mche Mungu, nawe UZISHIKE AMRI ZAKE, Maana kwa JUMLA ndiyo IMPASAYO [WAJIBU WAKE] MTU. Kwa maana Mungu ataleta HUKUMUNI kila kazi, pamoja na kila neno la siri, likiwa jema au likiwa baya." "Maana mtu awaye yote atakayeishika sheria yote, ila akajikwaa katika neno moja, amekosa juu ya yote. Kwa maana yeye aliyesema, Usizini, pia alisema, Usiue. Basi ijapokuwa hukuzini, lakini umeua, umekuwa mvunja sheria [mwenye dhambi]. Semeni ninyi na kutenda kama watu WATAKAOHUKUMIWA KWA SHERIA YA UHURU [AMRI KUMI]." Mhubiri 12:13,14; Yakobo 2:10-12.

Yesu mwenyewe anasema kwamba ili uweze kuingia mbinguni inakupasa uzishike Amri Kumi za Mungu. "Na tazama, mtu mmoja akamwendea akamwambia, Mwalimu, NITENDE JAMBO GANI JEMA, ILI NIPATE UZIMA WA MILELE? Akamwambia Kwani kuniuliza habari ya wema? Aliye mwema ni mmoja. Lakini UKITAKA KUINGIA KATIKA UZIMA, ZISHIKE AMRI [KUMI]." Mathayo 19:16,17. Upendo wa mwanadamu kwa Mungu unapimwa kwa Amri Kumi za

Mungu. "Mmoja wao, mwana-sheria akamwuliza, akimjaribu; Mwalimu, katika torati [Amri Kumi] ni amri ipi iliyo kuu? Akamwambia, MPENDE BWANA MUNGU WAKO kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa akili zako zote. Hii ndiyo AMRI ILIYO KUU [inayozijumlisha Amri Nne za Kwanza ----- Kutoka 20:3-11], tena ni ya KWANZA. Na ya PILI yafanana nayo, nayo ni hii, MPENDE JIRANI YAKO kama nafsi yako [ambayo inazijumlisha amri sita za mwisho ----- Kutoka 20:12-17]. Katika amri hizi mbili HUTEGEMEA TORATI YOTE na MANABII." "Msiwiwe na mtu cho chote, isipokuwa KUPENDANA; kwa maana ampendaye mwenzake ameitimiza sheria. Maana kule kusema, Usizini, Usiue, Usiibe, Usitamani; na ikiwapo amri nyingine yo yote, inajumlishwa katika neno hili, ya kwamba, MPENDE JIRANI YAKO KAMA NAFSI YAKO. Pendo halimfanyii jirani neno baya [huwezi kumwibia, wala kuzini na mke wake, na kadhalika]; basi PENDO NDILO UTIMILIFU WA SHERIA." Mathayo 22:35-40; Warumi 13:8-10.

Wajibu wa kumpenda jirani hauondoi wajibu wetu wa KWANZA kwa Mungu wa kushika Amri zile Nne za Kwanza (Kutoka 20:3-11). Hapo ndipo Wakristo wengi wanashindwa kuwajibika ipasavyo. Yesu alisema maneno haya: "Mkinipenda, MTAZISHIKA Amri zangu [Amri za Yesu ni zile zile za Baba yake ----- Yohana 10:30; 14:23,24; 16:13-15]." "Mkizishika Amri zangu, mtakaa katika pendo langu; kama vile mimi nilivyozishika AMRI ZA BABA YANGU na kukaa katika pendo lake." Yohana 14:15; 15:10.

Amri Kumi za Mungu zinatuonyesha dhambi zetu na kutuonyesha haja yetu ya kumwendea Mwokozi wetu kwa msamaha na ulinzi wake. "Tusemeje, basi? Torati [Amri Kumi] ni dhambi? Hasha! Walakini singalitambua dhambi ila kwa SHERIA [AMRI KUMI]; kwa kuwa singalijua KUTAMANI, kama torati [amri] isingalisema, USITAMANI. Lakini dhambi ilipata nafasi kwa ile AMRI, ikafanya ndani yangu kila namna ya kutamani. Kwa maana DHAMBI BILA SHERIA [AMRI KUMI] IMEKUFA [HAIPO]... Basi torati ni TAKATIFU, na ile AMRI NI TAKATIFU, na ya HAKI, na NJEMA. Basi je! ile iliyo njema ilikuwa mauti kwangu mimi? Hasha! bali DHAMBI, ili ionekane kuwa dhambi hasa, ilifanya mauti ndani yangu kwa njia ya ile njema, kusudi kwa ile amri dhambi izidi kuwa mbaya mno." Warumi 7:7,8,12,13. Baada ya Amri Kumi kutuonyesha dhambi zetu inatupasa kumwendea Yesu na kuziungama dhambi zetu na kupokea msamaha wake (Soma I Yohana 1:9; Mithali 28:13). Sheria na Neema hufanya kazi bega kwa bega; moja hugundua ugonjwa [dhambi]; ya pili hutupatia tiba [msamaha]. Mtu anayejiona kuwa ni mgonjwa [mwenzaye dhambi] ndiye anayemwendea Tabibu [Kristo].

Amri Kumi pia zinaonyesha kama wewe unamjua Mungu. "Na uzima wa milele ndio huu, WAKUJUE WEWE, Mungu wa pekee na wa kweli, NA YESU KRISTO uliyemtuma." "Na katika hili twajua ya kuwa TUMEMJUA Yeye, ikiwa TUNASHIKA AMRI ZAKE [KUMI]. Yeye asemaye, Nimemjua, wala HAZISHIKI AMRI ZAKE [KUMI], ni MWONGO, wala kweli haimo ndani yake." Yohana 17:3; I Yohana 2:3,4. WATAKATIFU wanatambuliwa kwazo. "Hapa ndipo penye subira ya WATAKATIFU, HAO WAZISHIKAO AMRI [KUMI] ZA MUNGU, na MANI ya Yesu." Ufunuo 14:12. Wale wanaofungwa magerezani huwa HAWAJAVUNJA AMRI ZOTE ZA NCHI. Lakini hata kuvunja amri moja tu inatosha kumfanya mhalifu huyo afungwe. Shetani alicheza na Amri Kumi za Mungu, naye akawakosesha wanadamu wazivunje pia. Mungu hana UPENDELEO wala KIGEUGEU. "Kwa kuwa Mimi, BWANA, sina KIGEUGEU; ndio maana ninyi hamkuangamizwa, enyi wana wa Yakobo." Malaki 3:6. Kwa hiyo, kama ALIMFUKUZA Shetani kwa kuvunja Amri mbili tu, HATAWEZA KUMKUBALI mwanadamu atakayevunja hata

amri moja tu. Kazi aliyofanya Shetani ni KUZIBADILI ili zisifanane na zile zilizoko mbinguni. "Dunia inaomboleza, inazimia; ulimwengu unadhoofika, unazimia; watu wakuu wa dunia wanadhoofika. Tena dunia imetiwa unajisi kwa watu wanaoikaa; kwa maana WAMEZIASI [WAMEZIVUNJA] SHERIA [AMRI KUMI], wameibadili amri, wamelivunja agano la milele [Sabato ni agano la milele ----- Kutoka 31:16]. Ndiyo sababu LAANA imeila dunia, na hao wanaokaa wameonekana kuwa na hatia, ndiyo sababu watu wanaoikaa dunia wameteketee [na wanazidi kuteketea], watu waliosalia WAKAWA WACHACHE TU." "Naye atanena maneno kinyume chake Aliye juu, naye atawadhoofisha watakatifu wake Aliye juu; naye ATAAZIMU KUBADILI MAJIRA [Kutoka 20:8-11] na SHERIA [Kutoka 20:4-6,17]; nao watatiwa mikononi mwake kwa wakati, na nyakati mbili na nusu wakati [Miaka 1260 ----- Ufunuo 12:6,14; 13:5]." Isaya 24:4-6; Danieli 7:25.

Shetani akawafanya wengine wazivunje Amri Kumi kwa makusudi huku wakijifariji kuwa Mungu HAANGALII vitu kama hivyo [ati anaangalia upendo moyoni tu]. Kama ingekuwa hivyo, basi, asingalimfukuza MWIMBAJI WAKE MZURI ambaye alimwekea talanta ya thamani sana ndani yake. Angalia Katekisimu yako na kulinganisha Amri Kumi za Mungu zilizomo humo na zile zilizo katika kitabu cha Kutoka 20:3-17. Katika Katekisimu zingine Amri ya pili inayokataza IBADA YA SANAMU imeondolewa kabisa (Kutoka 20:4-6), na Amri ile ya Kumi inayokataza KUTAMANI (Kutoka 20:17) imegawanywa mara mbili ili zitimie kumi. [Siku hizi kuna Biblia iliyofanyiwa marekebisha ili Amri Kumi za Kutoka 20:3-17 zisomeke kama zile zilizo katika baadhi ya Katekisimu. Biblia hiyo haipatikani kwa urahisi. Wahusika wasipotubu adhabu kali inawangojea siku ya mwisho - Kum. 4:2; Ufu. 22:18,19; Mit. 30:5,6.] Sheria za Mataifa mbalimbali zimetungwa na Mabunge ya nchi zao. Bunge ndilo lililo na uwezo wa KUBADILISHA SHERIA. Iwapo wanadamu wamebadilisha sheria ya Mungu [Amri Kumi] kwenye vitabu vyao vya sala, je! ni nani atakayekwenda KUBADILISHA SHERIA ILE ASILIA (ORIGINAL) YA AMRI KUMI ambayo daima IKO MBINGUNI? Yesu anasema watu wameacha sheria za Mungu na KUYASHIKA MAPOKEO. "Akawaambia, Isaya alitabiri vema juu yenu ninyi WANAFIKI, kama ilivyoandikwa, Watu hawa HUNIHESHIMU kwa midomo ila MIOYO yao iko mbali nami; NAO WANIABUDU BURE, WAKIFUNDISHA MAFUNDISHO YALIYO MAAGIZO YA WANADAMU, Ninyi MWAIACHA AMRI YA MUNGU, NA KUYASHIKA MAPOKEO YA WANADAMU. Akawaambia, Vema! MWAIKATAA AMRI YA MUNGU MPATE KUYASHIKA MAPOKEO YENU." Marko 7:6-9. Ibada yako inaweza kuwa bure kama katika siku ile ya HUKUMU utahukumiwa kwa kuvunja Amri zake Kumi ambapo ulidhani unazitii. Fanya matengenezo haraka kwani baada ya kufa inafuata Hukumu tu. "Na kama vile watu wanavyowekewa KUFA mara moja, na baada ya kufa HUKUMU." Waebrania 9:27.

----- Somo hili limetayarishwa na Mchungaji Meshack Nyagori.

KWA NINI TUSIMWULIZE MUNGU KUHUSU JUMAPILI NA SABATO?

=====

Niambie, Bwana, je, una siku maalum ya kupumzika kwa ajili ya wafuasi wako?

"Nalikuwa katika Roho Siku ya Bwana" Ufunuo 1:10.

Lakini siku ipi ni Siku ya Bwana? Wewe Yesu ni Bwana wa siku ipi?

"Kwa maana Mwana wa Adamu [Yesu] ni Bwana wa Sabato" Mathayo 12:8.

Kuna siku saba katika juma. Siku ipi ni siku ya Sabato?

"Lakini siku ya saba ni Sabato ya Bwana, Mungu wako...." Kutoka 20:10.

Siku ipi ni siku ya saba - Jumamosi au Jumapili?

"Hata Sabato ilipokwisha kupita, Mariamu Magdalene na Mariamu mamaye Yakobo,.... alfajiri mapema, siku ya kwanza ya juma, wakaenda kaburini, jua lilipoanza kuchomoza,.... Wakaingia kaburini wakaona kijana.... akawaambia, Msistaajabu; mnamtafuta Yesu Mnazareti, aliyesulubiwa; amefufuka."... Marko 16:1-6. (Kila mtu duniani anakiri kuwa Jumapili ndiyo siku ya ufufuo. Sabato ilikuwa imepita kulipopambazuka; hivyo ni wazi kuwa Sabato ni

Jumamosi, siku iliyo kabla ya Jumapili.)

Lakini, Bwana Yesu, je! Wewe hukuifutulia mbali sheria ile iliyo na amri ya Sabato?

"Msidhani ya kuwa nalikuja kuitangua torati au manabii; la, sikuja kutangua, bali kutimiliza" Mathayo 5:17.

Sawa. Lakini, je! hukubadili moja ya amri zile kumi ili siku hizi wafuasi wako wafuate siku nyingine na kuiacha siku ile ya saba?

"Kwa maana, amin, nawaambia, Mpaka mbingu na nchi zitakapoondoka, yodi moja wala nukta moja ya torati haitaondoka, hata yote yatimie." Mathayo 5:18.

Lakini, Bwana, Jumamosi sio siku ya Wayahudi? Si kweli kwamba Jumamosi ni Sabato ya Wayahudi?

"Akawaambia, Sabato ilifanyika kwa ajili ya mwanadamu." Marko 2:27. (Sabato ilifanyika na kupewa mwanadamu miaka 1500 kabla ya kuwako Myahudi. Angalia Mwanzo 2:1-3.

Lakini, je! Mtume Paulo hakuwa mara kwa mara anakutana na Wakristo wa mwanzo siku ya Jumapili kutukuza ufufuo? Alikuwa na desturi gani kuhusu siku ya kuabudu?

"Na Paulo, kama ilivyokuwa desturi yake, akaingia mle walimo akahojiana nao kwa maneno ya Maandiko Sabato tatu." Matendo 17:2.



Je! alikutana na Wamataifa walioongoka siku ya Sabato pia? Labda alikutana na Wayahudi siku ya Sabato na Wayunani siku ya Jumapili. Je, hilo nalo ni vipi?

"Akatoa hoja zake katika sinagogi kila Sabato, akajaribu kuwavuta Wayahudi na Wayunani." Matendo 18:4.

Je, hayo ndiyo maelekezo yake kuhusiana na utunzaji wa Sabato?

"Kwa maana sikujipusha na kuwahubiria habari ya kusudi lote la Mungu." Matendo 20:27. (Katika Agano Jipya kuna sehemu zisizopungua 59 zinazotaja sabato. Kitabu cha Matendo kinataja sabato 84 ambapo Mtume Paulo na wenzake walifanya mikutano ya kidini. Wala hakuna hata neno moja katika Biblia linaloidhinisha utunzaji wa Jumapili.)

Bwana, kwani inaleta tofauti gani nikitunza siku yo yote? Siku si ni siku tu?

"Hamjui ya kuwa kwake yeye ambaye mnajitua nafsi zenu kuwa watumwa wake katika kumtii, mmekuwa watumwa wake yule mnayemtii, kwamba ni utumishi wa dhambi uletao mauti, au kwamba ni utumishi wa utii uletao haki." Warumi 6:16.

Sasa nitafanyaje mimi, je! niitii Sabato ya amri ya nne ya Mungu, au niitunze Jumapili iliyowekwa na mwanadamu?

"Petro na mitume wakajibu, wakisema imetupasa kumtii Mungu kuliko wanadamu." Matendo 5:29.

Ee Bwana Yesu, wewe unafikirije juu ya utunzaji wa Jumapili?

"...Mkalitangua Neno la Mungu kwa ajili ya mapokeo yenu,... Nao waniabudu bure, wakifundisha mafundisho yaliyo maagizo ya wanadamu" Mathayo 15:6,9.

Lakini mamilioni ya watu waitunzao Jumapili hakika hawawezi kuwa wamekosea? Kweli inawezekana?

"Ingieni kwa kupitia mlango ulio mwembamba; maana mlango ni mpana na njia ni pana iendayo upotevuni, nao ni wengi waingiao kwa mlango huo. Bali mlango ni mwembamba, na njia imesonga iendayo uzimani, nao waionao ni wachache." Mathayo 7:13,14. (Wachache tu walimtii Mungu katika siku za Nuhu, katika siku za Lutu, na katika siku za Kristo. Wengi walipotua.)

Lakini Mchungaji X ni mtu mwenye hekima; Kwa nini yeye na Wahubiri wengine mashuhuri hawaitunzi Sabato?

"Maana ndugu zangu angalieni mwito wenu ya kwamba si wengi wenye hekima ya mwilini, si wengi wenye nguvu, si wengi wenye cheo walioitwa; bali Mungu aliyachagua mambo mapumbavu ya dunia awaibishe wenye hekima; tena Mungu alivichagua vitu dhaifu vya dunia ili aviaibishe vyenye nguvu." I Wakorintho 1:26,27.

Lakini mimi nimempokea Yesu; ninajua ni Mwokozi wangu; ninajua amenikubali na nimekuwa nikiitunza Jumapili. Hakika sitapotea kama sitaitunza Sabato sasa, au sivyo?

"Basi zamani zile za ujinga Mungu alijifanya kama hazioni; bali sasa anawaagiza watu wote wa kila mahali watubu." Matendo 17:30.

Mimi ninakujua wewe, Bwana; hutanihukumia kifo kwa kutoitunza Sabato, au sivyo?

"Yeye asemaye, Nimemjua, wala hazishiki amri zake, ni mwongo, wala kweli haimo ndani yake." 1 Yohana 2:4.

Lakini si inatosha tu kwamba mimi nampenda Bwana, kisha naishi kwa sheria ya upendo?

"Mkinipenda, mtazishika amri zangu." Yohana 14:15.

Je, usemi huo una maana ya kuzishika Amri zote Kumi?

"Maana mtu awaye yote atakayeishika sheria yote, ila akajikwaa katika neno moja, amekosa juu ya yote." Yakobo 2:10.

Ninafikiri kuwa kama tukijitahidi kumfuata Yesu, hilo tu ndilo lililo muhimu kwetu. Je, hiyo si sawa, Yesu?

"Yeye asemaye kuwa anakaa ndani yake imempasa kuenenda mwenyewe vile vile kama yeye alivyoenenda." 1 Yohana 2:6.

Je, wewe ulienendaje, Bwana? Nini ilikuwa desturi yako?

"Akaenda Nazareti, hapo alipolelewa; na Siku ya Sabato akaingia katika sinagogi kama ilivyokuwa desturi yake, akasimama ili asome." Luka 4:16.

Lakini, Bwana, hayo yalitokea zaidi ya miaka 1900 iliyopita. Kama ungerudi duniani leo, je! usingetunza siku nyingine badala ya Jumamosi?

"Kwa kuwa mimi, BWANA, sina kigeugeu." Malaki 3:6. "Yesu Kristo ni yeye yule, jana na leo na hata milele." Waebrania 13:8.

Je, wokovu wangu unategemea utii katika kuitimiza amri hii ya Sabato?

"Naye alipokwisha kukamilishwa, akawa sababu ya wokovu wa milele kwa watu wote wanaomtii." Waebrania 5:9.

Je, unafikiri ni muhimu kabisa kuzitunza Amri Kumi ili kupata uzima wa milele?

"...Lakini ukitaka kuingia katika uzima, zishike amri." Mathayo 19:17.

Lakini, Bwana, bado sioni kwa nini unasisitiza juu ya siku ya saba, Jumapili si ni nzuri tu kama Jumamosi?

"Mungu akaibarikia siku ya saba, akaitakasa." Mwanzo 2:3. "Kwa maana wewe BWANA, umebarikia, nayo imebarikiwa milele." I Mambo ya Nyakati 17:27.

Ehe! nionavyo mimi, kama nikiitunza siku moja kati ya siku saba za juma bila kujali ni siku ipi, hiyo itakuwa vizuri tu.

"Iko njia ione kanayo kuwa sawa machoni pa mtu; Lakini mwisho wake ni njia za mauti." Mithali 16:25. "Nayo twayanena si kwa maneno yanayofundishwa kwa hekima ya kibinadamu, bali yanayofundishwa na Roho, tukiyafasiri mambo ya rohoni kwa maneno ya rohoni. Basi mwanadamu wa tabia ya asili hayapokei mambo ya Roho wa Mungu; maana kwake huyo ni upuzi, wala hawezi kuyafahamu, kwa kuwa yatambulikana kwa jinsi ya rohoni."

1 Wakorintho 2:13,14.

Lakini Bwana! Bwana! Siwezi nikafanya jambo lingine? Je kukukiri kwangu hakuwezi kunifikisha mbinguni?

"Si kila mtu aniambiaye, Bwana, Bwana, atakayeingia katika ufalme wa mbinguni; bali ni yeye afanyaye mapenzi ya Baba yangu aliye mbinguni." Mathayo 7:21.

Lakini, mbona mimi nasali kila mara?

"Yeye aligeuzaye sikio lake asiisikie sheria, hata sala yake ni chukizo." Mithali 28:9.

Lakini, Bwana, Watazame watu wanaofanya miujiza kwa jina lako. Wengine wanaponya wagonjwa, wengine wananena kwa lugha na kufanya mambo mengi ya ajabu; lakini hawaitunzi Sabato. Hao nao vipi?

"Wengi wataniambia siku ile, Bwana, Bwana, hatukufanya unabii kwa jina lako, na kwa jina lako kutoa pepo, na kwa jina lako kufanya miujiza mingi? Ndipo nitawaambia dhahiri, Sikuwajua ninyi kamwe; ondokeni kwangu, ninyi mtendao maovu." Mathayo 7:22,23.

Ndiyo, sasa najua Sabato ni sahihi; lakini biashara yangu itaathirika kama nikiifunga siku ya Sabato. Ninaweza nikapoteza kazi yangu, inaweza ikanifanya nisiweze kufanikiwa kimaendeleo katika dunia.

"Kwa kuwa itamfaidia mtu nini kuupata ulimwengu wote, akipata hasara ya nafsi yake?" Marko 8:36.

Aa.. Kwa mimi mwenyewe nisingejali; lakini familia yangu, je? Isingekuwa vyema kwangu kufanya kazi tu siku ya Sabato kuliko familia yangu kufa njaa?

"...Kwa sababu Baba yenu wa mbinguni anajua ya kuwa mnahitaji yote. Bali utafuteni kwanza ufalme wake, na haki yake; na hayo yote mtazidishiwa." Mathayo 6:32,33.

Marafiki zangu watanicheka na kunidhihaki.

"Heri ninyi watakapowashutumu na kuwaudhi na kuwanenea kila neno baya kwa uongo, kwa ajili yangu. Furahini, na kushangilia; kwa kuwa thawabu yenu ni kubwa mbinguni; kwa kuwa ndivyo walivyowaudhi manabii waliokuwa kabla yenu." Mathayo 5:11,12. "Iwapo ulimwengu ukiwachukia, mwajua ya kuwa umenichukia mimi kabla ya kuwachukia ninyi." Yohana 15:18.

Lakini je, kama familia yangu isipokubaliana na mimi, niende kinyume na mapenzi yao, jambo ambalo linaweza kuleta mgawanyiko katika nyumba?

"Apendaye baba au mama kuliko mimi hanistahili; wala apendaye mwana au binti kuliko mimi, hanistahili; wala mtu asiyechukua msalaba wake akanifuata, hanistahili." Mathayo 10:37,38. "Basi, kadhalika kila mmoja wenu asiyeacha vyote alivyo navyo, hawezi kuwa mwanafunzi wangu." Luka 14:33.

Ninaogopa, sitaweza kuvumilia maonjo yote haya. Mimi ni dhaifu sana.

"Neema yangu yakutosha; maana uweza wangu hutimilika katika udhaifu... Maana niwapo dhaifu ndipo nilipo na nguvu. 2 Wakorintho 12:9,10. "Nayaweza mambo yote katika yeye anitiaye nguvu." Wafilipi 4:13.

Basi Bwana, kuna zawadi gani ya kuwa mwaminifu kwako na kwa Amri zako?

"Hakika nawaambia, hakuna mtu aliyeacha nyumba, au mke, au ndugu, au wazazi, au wana, kwa ajili ya ufalme wa Mungu, asiyepokea zaidi mara nyingi katika zamani hizi, na katika ulimwengu ujao uzima wa milele." Luka 18:29,30.

Bwana, basi mapenzi yako yatimizwe hapa duniani kama huko mbinguni. Kwa msaada wako, nitaitunza Sabato.

"Vema mtumwa mwema na mwaminifu." Mathayo 25:21.

----- Aliyelitayarisha somo hili hajulikani (anon).



## UJUMBE WA MUNGU WA MWISHO

"Naliona malaika mwingine akishuka kutoka mbinguni, mwenye mamlaka kuu [uwezo mkuu]; na nchi ikaangazwa kwa utukufu wake. Akalia kwa sauti kuu, akisema, Umeanguka, umeanguka Babeli ule mkuu; umekuwa maskani ya mashetani, na ngome ya kila roho mchafu mwenye kuchukiza." "Kisha nikasikia sauti nyingine kutoka mbinguni, ikisema, Tokeni kwake, enyi watu wangu, mshishiriki dhambi zake, wala msipokee mapigo yake." Ufunuo 18:1,2,4.

Maandiko hayo huonyesha wakati ule wa mbele litakaporudiwa tangazo la kuanguka kwa Babeli kama lilivyotolewa na malaika yule wa pili wa Ufunuo 14 (fungu la 8), likiwa na nyongeza ya maovu ambayo yamekuwa yakiingia katika mashirika mbalimbali [ya dini] yanayoiunda hiyo Babeli, tangu ujumbe huo ulipotolewa kwa mara ya kwanza katika kiangazi cha mwaka wa 1844. Hali ya kuogofya sana katika ulimwengu wa kidini inaelezewa hapo. Kila mara kweli inapokataliwa, akili za watu wanaohusika kuzidi kutiwa giza, na mioyo yao huzidi kuwa sugu mpaka wanakuwa wamejizungushia boma la kuwalinda katika ushupavu wao huo wa kikafiri. Kwa ufidhuli wao dhidi ya maonyo aliyotoa Mungu, wataendelea kuikanyaga chini ya miguu yao mojawapo ya Amri zile Kumi, mpaka wataanza kuwatesa wale wanaoishika [amri hiyo] kama ni takatifu. Kristo anakuwa si kitu kwao kwa dharau waliyo nayo juu ya Neno lake na juu ya watu wake. Mafundisho ya mizimu yanapokelewa na makanisa hayo [ya Babeli], kizuizi kilichowekwa juu ya moyo wa asili [ambao haujaongoka] huondolewa, na kule kukiri dini kwao kutakuwa kama vazi la kusitiri maovu mabaya mno. Imani katika ishara za mapepo [miujiza] huzifungulia mlango roho zile zidanganyazo na mafundisho ya mashetani [1 Tim. 4:1], na kwa njia hiyo mvuto wa malaika hao wabaya [mapepo] utasikika katika makanisa hayo [ya Babeli].

Kwa habari za Babeli, kwa wakati ule ulioonyeshwa katika unabii huo, inatangazwa hivi: "Kwa maana dhambi zake zimefika hata mbinguni, na Mungu amekumbuka maovu yake." Ufunuo 18:5. Amekijaza kikombe cha maovu yake, na maangamizi yako karibu kuanguka juu yake. Lakini Mungu bado anao watu wake katika Babeli; na kabla ya kupatilizwa kwa hukumu zake, waaminifu hao [waliomo Babeli] hawana budi kuitwa ili watoke, wasishiriki dhambi zake, wala wa"sipokee mapigo yake." Kwa sababu hiyo lipo tapo [kundi] linalofananishwa na malaika huyo ashukaye kutoka mbinguni, akiiangaza nchi na kulia kwa sauti kuu, akitangaza dhambi za Babeli. Kuunganisha na ujumbe wake huo wito huu unasikika: "Tokeni kwake, enyi watu wangu." Matangazo hayo, yakiunganishwa na Ujumbe wa Malaika wa Tatu, hutoa onyo la mwisho kwa wakazi [wote] wa dunia hii.

Matokeo ni ya kutisha ambayo ulimwengu huu utakabiliwa nayo. Mamlaka [Serikali] za dunia, zikiungana pamoja ili kuzipiga vita Amri [Kumi] za Mungu, zitatoa amri isemayo kwamba "wote, wadogo kwa wakubwa, na matajiri kwa maskini, na walio huru kwa watumwa," (Ufunuo 13:16), watafuata desturi za kanisa kwa lazima kwa kuishika sabato ya uongo [Jumapili]. Wale wote wanaokataa watapata adhabu kwa mujibu wa sheria za nchi, na hatimaye itatangazwa kwamba hao wanastahili kifo [kuuawa]. Kwa upande mwingine, Sheria ya Mungu [Amri Kumi] inayowaamuru

[watu wote] kuitakasa siku ile aliyoiweka Muumbaji [Sabato au Jumamosi], inadai utii na kutishia ghadhabu [mapigo saba - Ufu. 15:1; 16:1-21] dhidi ya wale wote wanaozivunja amri zake [kumi].

Jambo hilo litakapowekwa wazi mbele yake, basi, mtu ye yote atakayeikanyaga Sheria ya Mungu [Amri Kumi] ili kuitii amri ile iliyotungwa kisheria [katika Bunge] na wanadamu atapokea Alama (Chapa) ya Mnyama; ataipokea alama ya utii wake kwa mamlaka ile anayochagua kuitii badala ya [kumtii] Mungu. Onyo kutoka mbinguni ni hili: "Mtu awaye yote akimsujudu huyo Mnyama [Upapa] na Sanamu yake [Uprotestanti Ulioasi], na kuipokea chapa [alama] katika kipaji cha uso wake, yeye naye atakunywa katika mvinyo ya ghadhabu ya Mungu [mapigo yale saba] iliyotengenezwa, pasipo kuchanganywa na maji [kali sana], katika kikombe cha hasira yake." Ufunuo 14:9,10.

Walakini hakuna hata mmoja atakayeteswa kwa ghadhabu hiyo ya Mungu [mapigo saba] mpaka hapo kweli hiyo itakapokuwa imemfikia moyoni mwake na katika dhamiri yake, na kukataliwa. Wako wengi ambao hawajapata nafasi kabisa ya kuzisikia kweli hizo za pekee zinazohubiriwa kwa wakati huu. Uwajibikaji wao kwa ile amri ya nne [Kutoka 20:8-11] haujapata kamwe kuwekwa mbele yao katika nuru yake halisi [inayoeleweka]. Yule anayesoma kila moyo na kulipima kila kusudi la moyoni [Mungu] hatamwacha adanganyike mtu ye yote anayetamani kuijua kweli yake, kwa habari ya mambo yale yanayohusika katika pambano hilo. Amri hiyo [ya Jumapili] haitalazimishwa juu ya watu wakiwa vipofu. Kila mmoja hana budi kupata nuru ya kutosha ili apate kufanya uamuzi wake kwa akili.

## Jaribio Kuu la Utii

Sabato [Jumamosi] itakuwa jaribio kuu la [kupima] utii wetu [kwa Mungu], maana hiyo ndiyo kweli moja inayobishaniwa hasa. Jaribio la mwisho litakapokuja juu ya wanadamu [wote], ndipo mstari wa kuwabagua watu utakapochorwa kati ya wale wamtumikia Mungu na wale wasiomtumikia. Wakati utunzaji wa sabato ya uongo [Jumapili] kwa kuitii sheria ya serikali, kinyume na amri ile ya nne [ya Mungu], kitakuwa ni kiapo cha utii kwa mamlaka ile inayompinga Mungu [Upapa], utunzaji wa Sabato ya kweli [Jumamosi], kwa kuitii Sheria ya Mungu [Amri Kumi] utakuwa ni ushahidi unaoonyesha utii kwa Muumbaji. Wakati kundi moja, kwa kuipokea alama ile ya utii kwa mamlaka [serikali] za dunia, linapokea Alama (Chapa) ya Mnyama [Ufu. 13:16,17], kundi lile jingine, kwa kuichagua ishara ile ya utii kwa mamlaka ya Mungu, watapokea Muhuri wa Mungu [Ufu. 7:1-4].

Mpaka sasa wale waliozihubiri kweli zile za Ujumbe wa Malaika wa Tatu mara nyingi wamefikiriwa kuwa ni wavumishaji wa mambo ya kutisha. Utabiri wao usemao kwamba ukandamizaji wa dini [kutovumilia itikadi za kidini za wengine] utajizatiti tena katika nchi ya Marekani, na ya kwamba kanisa na serikali vitaungana pamoja kwa madhumuni ya kuwatesa sale wanaozishika Amri [Kumi] za Mungu, umetangazwa kuwa hauna msingi, tena ni upuuzi [mtupu]. Imetangazwa kwa ujasiri kwamba nchi hii [ya Marekani] haiwezi kamwe kufanya tofauti na vile ilivyofanya [zamani] ----- yaani, [itaendelea kuwa] mlinzi wa uhuru wa dini. Lakini hoja hiyo ya

kulazimisha utunzaji wa Jumapili inapozidi kusesitizwa mahali pengi, tukio lile lililoonewa mashaka kwa muda mrefu mno na kutosadikiwa sasa linaonekana kuwa linaharikisha sana kuja, na ujumbe ule wa [Malaika yule wa] tatu utaleta matokeo makubwa ambayo usingekuwa nayo kabla ya wakati huo kufika.

=====

PLEASE INSERT HERE DRAWING ON PAGE 356 (TEXTBOOK).

USE SWAHILI EQUIVALENT AND SCRIPT AS FOLLOWS:

GOD'S LAW = SHERIA YA MUNGU

CREATOR = MUUMBAJI UNIVERSE = ULIMWENGU

GOD = MUNGU

Swahili Script: Muhuri Mkuu wa Mungu hupatikana katikati ya Sheria yake

[Amri Kumi] nao unajumuisha jina lake, mamlaka yake, na enzi yake.

=====



Kwa kila kizazi Mungu amewatuma watumishi wake kukemea dhambi, katika ulimwengu na ndani ya kanisa. Lakini watu wanapenda kuambiwa mambo laini, na ile kweli safi, isiyoficha makosa, haikubaliki. Wanamatengenezo ya kanisa wengi, walipoanza kazi yao, walidhamiria kutumia busara nyingi katika kuzishambulia dhambi za kanisa na taifa. Walitumaini ya kuwa, kwa njia ya kielelezo chao cha maisha safi ya Kikristo, wangeweza kuwaongoza watu kurudi katika mafundisho yale ya Biblia. Lakini Roho wa Mungu aliwajia juu yao kama alivyomjia Eliya, alipomsukuma kuzikemea dhambi za mfalme yule mwovu na watu wale waasi; hawakuweza kujizuia wasihubiri maneno yale ya Biblia ----- yaani, mafundisho yale waliyokuwa wanasita kuyatoa. Walilazimishwa kuitangaza ile kweli kwa bidii licha ya hatari iliyokuwa inawatiishia watu. Maneno yale aliyowapa Bwana ndiyo waliyonena, bila kujali matokeo yake, na watu nao wakalazimika kulisikia onyo lile.

### Ujumbe Huo Kutangazwa Kwa Nguvu

Kwa njia hiyo ujumbe huo wa malaika wa tatu utatangazwa. Wakati utakapofika kwa ujumbe huo kuhubiriwa kwa nguvu nyingi mno, Bwana atafanya kazi kwa njia ya vyombo vyake [wajumbe wake] vinyenyekevu, akiyaongoza mawazo ya wale wanaojitoa wakf kufanya kazi yake. Watendakazi hao watafanywa waweze kufaa [watapata sifa zao] kwa msukumo wa Roho wake kuliko kwa mafunzo yale yanayotolewa katika taasisi za maandiko. Watu wale wenye imani na maombi, watabidishwa kusonga mbele kwa juhudi takatifu, wakitangaza maneno anayowapa Mungu. Dhambi za Babeli zitawekwa peupe. Matokeo ya kutisha ya kulazimisha kisheria maadhimisho yaliyowekwa na kanisa kwa kutumia mamlaka ya serikali za kiraia, kujipenyeza [kanisani] kwa imani ya mizimu, maendeleo ya chinichini, lakini ya haraka ya mamlaka ile ya kipapa ----- mambo yote hayo yatafichuliwa. Kwa maonyo hayo ya kutisha watu wataamshwa. Maelfu kwa maelfu, watasikiliza ambao hawajapata kamwe kuyasikia maneno kama hayo. Kwa mshangao wanasikia ushuhuda unaosema kwamba Babeli ni kanisa, limeanguka kwa sababu ya makosa yake [mafundisho yake potofu] na dhambi zake [uvunjaji wa Amri Kumi], kwa sababu limeikana ile kweli iliyotumwa kwake kutoka mbinguni. Watu watakapokuwa wanawaendea waalimu wao wa zamani [wachungaji wao] wakiwa na shauku kubwa ya kuwauliza maswali, wakisema, Je! mambo hayo ndivyo yalivyo? wachungaji wao watawambia hadithi za uongo, yaani, watawahubiria mambo laini laini tu ili kuituliza hofu yao na kuzinyamazisha dhamiri zao zilizoamshwa. Lakini kwa kuwa wengi wao watakataa kuridhika na mamlaka ya wanadamu tu na kudai wapewe neno dhahiri lisemalo, "Hivi ndivyo asemavyo Bwana," ndipo wachungaji wale wanaopendwa sana na watu wengi, kama Mafarisayo wa wale zamani, watajawa na hasira kali wakati mamlaka yao itakapotiliwa mashaka, wataukana katakata ujumbe huo na kusema kwamba unatoka kwa Shetani, kisha watawachochea watu wengi wanaoipenda dhambi ili wawalaani na kuwatesa wale wanaoutangaza ujumbe huo.

### Pambano Kuenea

Pambano hilo litakapoenea katika sehemu mpya na mawazo ya watu yatakapokumbushwa kuhusu Sheria ya Mungu [Amri Kumi} iliyokanyagwa chini, ndipo Shetani atakapochachamaa. Uweza ule unaoandamana na ujumbe huo utawafanya wale wanaoupinga kuwa kama wenda wazimu tu. Wachungaji watatumia juhudi ambayo karibu inapita kabisa uwezo wao wa kibinadamu ili kuifungia mbali nuru hiyo isije ikawaangazia makundi yao [watu wao]. Kwa kutumia kila njia iliyo katika uwezo wao watajitahidi kuzuia kabisa mjadala wo wote juu ya maswali hayo muhimu [nyeti]. Kanisa litaomba nsaada wa mkono wenye nguvu wa serikali [rungu la dola], na katika kazi hiyo wafuasi wa papa na Waprotestanti wataungana [na kuwa kitu kimoja]. Tapo [kundi] hilo linalotaka Jumapili itungiwe sheria Bungeni linapozidi kuwa na ujasiri na kudhamiria kufanya hivyo, ndipo sheria itawekwa dhidi ya hao wazishikao amri [kumi za Mungu]. Watatishiwa kutozwa faini na kufungwa gerezani, na baadhi yao watapewa nafasi zenye uwezo [vyeo], na thawabu nyinginezo pamoja na marupurupu, kama vivutio ili waikane imani yao. Lakini jibu lao thabiti litakuwa ni hili: "Tuonyesheni kosa letu kutoka katika Neno la Mungu" ----- yaani, sababu ile ile iliyotolewa na Martin Luther chini ya mazingira yayo hayo. Wale watakaoshtakiwa mahakamani wataitetea kweli kwa nguvu, na baadhi ya wale watakaowasikiliza wataongozwa kuchukua msimamo wao kwa kuzishika Amri zote [Kumi] za Mungu. Kwa njia hiyo nuru itawekwa mbele ya maelfu ambao vinginevyo wasingejua cho chote juu ya kweli hizo.

Uti wa dhati kwa Neno la Mungu utahesabiwa kama ni uasi. Akiwa amepofushwa macho na Shetani, mzazi atatumia ukatili na ukali wake kwa mtoto wake aaminiye; bwana au bibi [kazini] atamkandamiza mtumishi wake anayezishika amri [kumi za Mungu]. Upendo utageuka kuwa mfarakano; watoto watanyang'anywa urithi wao na kufukuzwa mbali na nyumbani kwao. Maneno yale ya Paulo yatatekelezwa neno kwa neno: "Naam, na wote wapendao kuishi maisha ya utauwa katika Kristo Yesu wataudhiwa [watateswa]." 2 Timotheo 3:12. Wanaoitetea ile kweli wanapokataa kuiheshimu sabato-ya-Jumapili, baadhi yao watatupwa gerezani, wengine watapelekwa uhamishoni, wengine watatendewa kama watumwa. Kwa hekima ya kibinadamu mambo hayo yote kwa sasa yanaonekana kuwa hayawezekani; lakini Roho wa Mungu anayezuia atakapoondolewa kwa wanadamu [walio waovu sugu], watakuwa chini ya uongozi wa Shetani, anayezichukia amri [kumi] za Mungu, hapo ndipo mambo ya ajabu yatakapotokea. Moyo unaweza kuwa mkatili sana hofu ya Mungu na upendo wake vinapoondolewa kutoka humo.

=====

PLEASE INSERT SWAHILI EQUIVALENTS IN THE DIAGRAM ON PAGE 358

AS WELL AS THE SCRIPT UNDER IT AS FOLLOWS:-

ETERNAL LIFE = UZIMA WA MILELE

PERSECUTION = MATESO

BIBLE = BIBLIA

SWAHILI SCRIPT: Katika mizani ile ya milele, utajiri wa duniani, raha,

na mwonekano wa kuwa na amana salama, havina

uzito wo wote. Umuhimu upitao vyote ni ule uaminifu

kwa ile kweli ya Mungu.

=====

Dhoruba inapokaribia, kundi kubwa la wale waliopata kuikiri imani hiyo ya ujumbe wa malaika wa tatu, ila hawakutakaswa kwa kuitii ile kweli, wanaziacha nafasi zao na kujiunga na jeshi la upinzani. Kule kujiunga kwao na ulimwengu huu na kushiriki roho yake, wamekuja kuyaangalia mambo karibu kwa nuru ile ile; na jaribio lile linapokuja, wamejiweka tayari kuchagua upande ule ulio rahisi, yaani, ule unaopendwa na watu wengi. Watu hao wenye kipaji na hotuba zenye kupendeza, ambao hapo mwanzo walipata kuifurahia kweli hiyo, wanatumia uwezo wao kuwadanganya na kuwapotosha watu. Wanakuwa maadui wakali sana wa ndugu zao wa zamani. Wasabato wanapoletwa mbele za mahakama kuitetea imani yao, waasi hao ni vibaraka wa Shetani wanaofanikiwa sana kuwaeleza vibaya na kuwashtaki [ndugu zao wa zamani katika imani], na kwa kutoa taarifa za uongo na kuwasingizia wanawachochea watawala dhidi yao.

Katika kipindi hicho cha mateso imani ya watumishi wa Bwana itapimwa. Wamekwisha kutoa onyo hilo kwa uaminifu, wakimtazama Mungu na Neno lake peke yake. Roho Mtakatifu, akiwa amegusa mioyo yao, amewabidisha kunena. Wakiwa wamechochewa na ari ile takatifu, na mvuto ule wa mbinguni ukiwa na nguvu juu yao, walianza kutekeleza majukumu yao bila kufikiria kwa ubaridi matokeo ya kunena na watu Neno lile alilowapa Bwana. Hawajayaangalia mambo yao ya

maisha yanayowaletea faida, wala kujaribu kulinda sifa ya maisha yao. Walakini dhoruba ya upinzani na shutuma inapowaangukia, wengine, wakiwa wamelemewa na hofu kuu na mshangao, watatamka ghafula kwa mshangao, wakisema: "Laiti kama tungekuwa tumejua mapema matokeo ya maneno yetu, tungekuwa tumenyamaza kimya." Wamezingirwa na dhiki. Shetani anawashambulia kwa majaribu yake makali. Kazi waliyopewa kuifanya inaonekana kuwa inazidi sana uwezo wao kuikamilisha. Wanatiishiwa na maangamizi. Shauku iliyowachochea inatoweka; hata hivyo, hawawezi kurudi nyuma. Wanapojisikia ya kuwa hawana uwezo kabisa, hapo ndipo wanapomkimbilia yule Mwenye Uweza ili kutiwa nguvu. Wanakumbuka kwamba maneno yale waliyonena hayakuwa yao, bali ni yake yeye aliyewaamuru kulitoa onyo lile. Mungu aliiweka kweli yake mioyoni mwao, nao hawakuweza kuvumilia wasiitangaze.

Maonjo yayo hayo yamewapata watu wa Mungu katika vizazi vilivyopita. Wycliffe, Huss, Luther, Tyndale, Baxter, na Wesley, walisisitiza kwamba mafundisho yote ya dini sharti yapimwe kwa Biblia, tena walitangaza kwamba wao wangekiachilia mbali kila kitu [Biblia] ilichokataza. Mateso yaliyoendelea kwa ukali usio na huruma yalielekezwa dhidi ya watu hao; hata hivyo, wao hawakuacha kuitangaza kweli hiyo. Vipindi mbalimbali katika historia ya kanisa vimekuwa na ukuzaji wa kweli fulani ya pekee, inayokidhi mahitaji ya watu wa Mungu kwa kipindi kile. Kila kweli moja moja imepitia katika njia iliyojaa chuki na upinzani; wale waliobarikiwa na nuru yake walijaribiwa na kupimwa. Mungu anawapa watu wake kweli fulani ya pekee wakati ule wa hatari. Nani atathubutu kutoitangaza? Anawaamuru watumishi wake kutoa mwaliko wake wa mwisho wa rehema kwa ulimwengu mzima. Hawawezi kukaa kimya, isipokuwa kwa hasara ya nafsi zao. Mabalazi [wajumbe] wa Kristo hawashughuliki kabisa na matokeo. Ni lazima waitekeleze kazi yao waliyopewa na kuacha matokeo mikononi mwa Mungu.

## Upinzani Unafikia Vilele Vipya

Upinzani unapofikia kilele cha ukali zaidi, watumishi wa Mungu hufadhaika tena; kwa maana kwao inaonekana kwamba wamejiletea hatari hiyo kubwa. Lakini dhamiri zao pamoja na Neno la Mungu huwahakikishia kuwa njia ile wanayoifuata ni sahihi; na japokuwa maonjo yao yanaendelea, wanatiwa moyo kuweza kuyavumilia. Pambano linazidi kusonga karibu nao sana na kuwa kali zaidi, lakini imani yao na ujasiri wao huongezeka, licha ya hatari ile [inayowakabili]. Ushuhuda wao ni huu: "Hatathubutu kulichezea Neno la Mungu kwa kutumia uongo, kuigawa Sheria yake [Amri Kumi] takatifu; kuita sehemu moja kuwa ni ya muhimu na ile nyingine kuwa haina umuhimu wo wote, na kujipatia upendeleo wa [kupendwa na] ulimwengu huu. Mungu tunayemtumikia anaweza kutuokoa. Kristo amezishinda mamlaka zote za dunia [Mathayo 28:18; Yohana 16:33]; basi, je! sisi tuogope ulimwengu huu uliokwisha kushindwa tayari?"

Mateso katika aina zake mbalimbali ni ukuzaji wa kanuni ambayo itaendelea kuwako kadiri Shetani anavyoendelea kuwako na Ukristo unavyozidi kuwa na nguvu ihuishayo. Hakuna mtu ye yote awezaye kumtumikia Mungu pasipo kujiletea mwenyewe majeshi yale ya giza. Malaika wale

wabaya watamshambulia, wakiingiwa na hofu kuu kwamba mvuto wake unapora nyara zao toka mikononi mwao. Watu wabaya waliokemewa kwa kielelezo chake [yaani, mfano mzuri wa maisha yake], watajiunga pamoja nao [mapopo] ili kujaribu kumtenga mbali na Mungu wake kwa kumletea majaribu yanayovutia sana. Hayo yasipofaulu, ndipo nguvu [mabavu] hutumika ili kumlazimisha afanye kinyume na dhamiri yake.

Yesu, Mwombezi wa Mwanadamu

Lakini kadiri Yesu anavyoendelea kuwa mwombezi wa mwanadamu katika patakatifu pale pa mbinguni uwezo ule uzuiwa wa Roho Mtakatifu unaigusa mioyo ya watawala pamoja na watu. Bado unazidhibiti kwa kiwango fulani sheria za nchi [serikali]. Kama sheria hizo zisingalikuwako, hali ya ulimwengu huu ingekuwa mbaya zaidi kuliko hivi ilivyo sasa. Ingawa watawala wetu wengi ni mawakala hai wa Shetani, Mungu pia anao mawakala wake miongoni mwa wakuu katika taifa. Adui anawachochea watumishi wake kupendekeza hatua ambazo zingeweza kuikwamisha sana kazi ya Mungu; lakini wanasiasa weledi wamchao Mungu huongozwa na malaika watakatifu kuyapinga mapendekezo hayo kwa hoja zisizokanushika. Kwa njia hiyo watu wachache tu watauzuia mkondo wenye nguvu wa uovu. Upinzani wa adui wa ile kweli utazuiwa ili ujumbe wa malaika yule wa tatu upate kufanya kazi yake. Onyo la mwisho litakapokuwa limekwisha kutolewa, litayanasa mawazo ya wakuu hao ambao kwa njia yao Bwana anafanya kazi yake hivi sasa, na baadhi yao watalizingatia [onyo hilo] na kusimama pamoja na watu wa Mungu katika kipindi kile cha wakati wa taabu.

Malaika yule anayejiunga kuutangaza ujumbe huo wa Malaika wa Tatu ataiangaza nchi [dunia] yote kwa utukufu wake. Kazi hiyo itakayoenea ulimwenguni kote, itakayofanywa kwa uwezo usio wa kawaida, inatabiriwa hapo. Tapo [kundi] lile la Waadventista la miaka ile ya 1840-44 lilikuwa ni ishara ya uweza wa Mungu uliofanikiwa vibaya sana; ujumbe ule wa malaika wa kwanza ulipelekwa katika kila kituo cha umishonari ulimwenguni kote, na katika baadhi ya nchi palikuwa na mwamko mkubwa wa mambo ya kiroho ambao tangu siku zile za Matengenezo ya Kanisa ya karne ile ya kumi na sita haujatapa kushuhudiwa katika nchi yo yote; lakini hayo yatapitwa kabisa na tapo [kundi] hilo lenye uwezo mkubwa linalofanya kazi yake [hivi sasa] chini ya onyo la malaika huyo wa tatu.

Kazi hiyo itafanana na ile ya Siku ya Pentekoste. Kama vile "mvua ya kwanza [ya vuli]" ilivyotolewa kwa kumwagwa kwa Roho Mtakatifu kwa wingi wakati wa kuanza [kuhubiriwa] injili, kuifanya mbegu ile ya thamani ipate kuchipua, ndivyo "mvua ya masika" itakavyotolewa wakati wa kufungwa kwa kazi hiyo [ya injili] ili kuyakomaza mavuno. "Ndipo tutajua, tukiendelea kumjua BWANA; kutokea kwake ni yakini kama asubuhi: naye atatujilia kama mvua, kama mvua ya masika na ya vuli [ya kwanza] iinyweshayo nchi." Hosea 6:3 (Tafsiri ya KJV). "Furahini, basi, enyi wana wa Sayuni, mkamfurahie BWANA, Mungu wenu; kwa kuwa yeye kuwapa ninyi mvua ya masika, kwa kipimo cha haki, naye huwanyesha mvua, mvua ya masika, na mvua ya vuli, kama kwanza." Yoeli 2:23. "Itakuwa siku za mwisho, asema Mungu, nitawamwagia watu wote Roho yangu." "Na itakuwa kila atakayeliitia jina la Bwana ataokolewa." Matendo 2:17,21.

Kazi hii kuu ya injili haitafungwa kwa ishara pungufu za uweza wa Mungu kuliko zile zilizoonekana mwanzo wake. Unabii ule uliotimizwa wakati wa kumwagwa kwa mvua ile ya kwanza [ya vuli] mwanzoni mwa kazi hii ya injili utatimizwa tena kwa kumwagwa kwa mvua ya masika itakapofungwa [kazi hiyo]. Hapa ndipo zipo zile "nyakati za kuburudishwa [mvua ya masika]" ambazo mtume Petro alizitazamia aliposema" " Tubuni basi, mrejee, ili dhambi zenu zifutwe, zipate kuja nyakati za kuburudishwa kwa kuwako kwake Bwana; apate kumtuma Kristo Yesu." Matendo 3:19,20.

Watumishi wa Mungu nyuso zao zikiangazwa kwa nuru na kung'aa kwa juhudi yao iliyotolewa wakf, wataharakisha toka mahali kwenda mahali pengine kuutangaza ujumbe huo uliotoka mbinguni. Kwa maelfu ya sauti, ulimwenguni kote, onyo hilo litatolewa. Miujiza itafanywa, wagonjwa wataponywa, na ishara na maajabu yatafuatana na wale waaminio. Shetani pia atafanya kazi yake kwa ishara [miujiza] za uongo, hata kufanya moto kushuka kutoka mbinguni uje mbele ya watu. Ufunuo 13:13. Hivyo ndivyo wakazi wote wa dunia hii watakavyofikishwa mahali watakapochagua upande wao watakaosimama.

Ujumbe huo utapelekwa sio sana kwa majadiliano bali kwa mguso wa ndani kabisa wa Roho wa Mungu utakaowasadikisha watu. Sababu zote zimekwisha kutolewa. Mbegu imekwisha kupandwa, na sasa itachipua na kuzaa matunda. Vitabu vile vilivyotawanywa na watendakazi wetu wamishonari vimekuwa na mvuto wenye nguvu, lakini wengi ambao mioyo yao ilikuwa imeguswa wamezuiwa wasiweze kuuelewa kikamilifu ukweli huo au kutoa utii wao. Hivi sasa miali ya nuru inapenya kila mahali, kweli inaonekana katika uwazi wake, na watoto wa Mungu walio wanyofu wa moyo wanazikata kamba zilizowafunga na kuwazuia. Uhusiano wa kifamilia, uhusiano kikanisa, hauna uwezo kabisa kuwazuia sasa. Kweli ni ya thamani sana kwao kuliko mambo mengine yote. Licha ya nguvu zote zilizojikusanya pamoja dhidi ya ile kweli, idadi kubwa wanachagua kusimama upande wa Bwana.

E. G. White, in THE TRIUMPH OF GOD'S LOVE, uk. 355-360,

OR: THE GREAT CONTROVERSY, Sura ya 38, uk. 603-612.

----- (God's Final Message - Kiswahili).

